FIDHI/Shirikiso la Kimataifa Juu ya Haki za Binadamu

# *Taarifa*

## Ujumbe wa Kimataifa wa Kutafuta Ukweli

# Tanzania:
# Adhabu ya Kifo Imerasimishwa?


Dibaji: Uhuhimu wa kuhamasishwa uingaji wa Adhabu ya Kifo..........................................3

Utangulizi.......................................................................................................................... 7

I. Mfumo wa Kisiasa na Kimahakama Tanzania......................................................................8

II. Adhabu ya Kifo/Hukumu ya Kifo na viwango vya Kimataifa........................................14

III. Ukubalifu na Kanuni ya Sheria: Haki imezingirwa..........................................................19

IV. Makosa yatolewayo adhabu ya kifo nchini Tanzania........................................................28

V. Utungaji/uumbaji wa hatia: Safari ipitiwayo na mfumo wa Makosa ya Jinai wa Tanzania..........................................................................................................32

VI. Harakati kuelekea iwenge ufuataji/ ukomeshaji................................................................56

Mapendekezo..........................................................................................................................58

VII. Bibligorafia/Marejeo..........................................................................................................60

VIII. Kiambatanisho...................................................................................................................61

**Yaliyomo**

**Dibaji: Umuhimu wa kuhamasisha upingaji wa adhabu ya kifo..........................................................3**
1. Adhabu ya kifo haiendani kabisa na dhana nzima ya heshima ya binadamu na uhuru wake.................3
2. Adhabu ya kifo haisaidii.......................................................................................................................4
3. Hoja kutoka kwenye sheria za Kimataifa za Haki za Binadamu.................................................................5

**Utangulizi.........................................................................................................................................7**

**I. Mfumo wa Kisiasa na Kimahakama Tanzania...................................................................................8**
1. Kuzaliwa kwa nchi..............................................................................................................................8
2. Mfumo wa sheria wa makosa ya jinai Tanzania......................................................................................11
3. Uridhiwaji wa mikataba ya haki za binadamu.........................................................................................13

**II: Hukumu ya kifo na viwango vya kimataifa......................................................................................14**
1. Mfumo wa Umoja wa Mataifa.................................................................................................................14
2. Mfumo wa Kikanda: Mkataba wa Afrika Juu ya Haki za Binadamu na Watu.........................................16
a. Muundo wa Kisheria..............................................................................................................................16
b. Utendaji wa Nchi jilani...........................................................................................................................18

**III: Ukubalifu na kanuni ya Sheria: Haki imezingirwa.........................................................................19**
1. Mfalme na Serikali, hawafanyi kosa....................................................................................................19
a. Kusita kukubaliana na maamuzi ya mkataba inayoegemea mfumo wa usimamizi....................................20
b. Kutokuwa na imani na Mahakama...........................................................................................................21
2. Mfumo wa jinai uliojengwa katika ulipizaji kisasi..................................................................................22
3. Rushwa ni Tishio kaika mchakato wa marekebisho.....................................................................................27

**IV: Makosa yatolewayo adhabu ya kifo nchini Tanzania......................................................................28**
1. Mauaji ya Kukusudia..............................................................................................................................28
2. Uhaini.....................................................................................................................................................30
3. Mwenendo mbaya wa kamanda au askari yoyote katika uwepo wa adui..................................................31

**V: Utungaji Hatia: Safari katika mfumo wa makosa ya jinai Tanzania...............................................32**
1. Kukamatwa kwa mtuhumiwa...................................................................................................................33
a. Muda wa kuwekwa kizuizini/mahabusu kabla ya mashtaka.......................................................................38
b. Hali ya kizuizi ya walengwa walioko mahabusu.........................................................................................41
2. Hatua za shitaka.......................................................................................................................................44
a. Ubora wa Huduma ya Kutetewa kwa Washitakiwa wasio na uwezo wa kifedha katika kesi za Mauaji Tanzania..........................................................................................................................45
b. Wajibu/ugumu wa kuthibitisha na ushaidi unaokubalika na mahakama....................................................47
c. Rushwa....................................................................................................................................................49
3. Rufaa na msamaha wa Rais.....................................................................................................................50
4. Hatua inayofuata baada ya kuonekana kuna hatia.......................................................................................52

**VI: Harakati kuelekea kwenye ufutaji/Ukomeshaji..............................................................................56**

**Mapendekezo......................................................................................................................................58**

**VII Marejeo.............................................................................................................................................60**

**VIII Kiambatanisho................................................................................................................................61**

**Dibaji**: **Kwanini kuna uhamasishaji wa upingaji wa adhabu ya kifo**

Shirika la FIDH linapinga kwa nguvu zote hukumu ya kifo. FIDH inasisitiza kwamba hukumu ya kifo ni kinyume kabisa na dhana nzima ya heshima ya binadamu na uhuru wake; zaidi ya hapo adhabu ya kifo haisaidii kuwafanya watu waache kufanya maovu. Matokeo yake adhabu hiyo haina sababu zozote za kimsingi au kifasaha zinazoweza kutetea matumizi ya adhabu ya kifo.

**1.Hukumu ya kifo haiendani kabisa na dhana nzima ya heshima ya binadamu na uhuru wake.**

Haki za binadamu na utu wake zimekubalika na mataifa yote kama ambavyo zinaunda misingi ya jumuiya iliyojengeka kisiasa. Adhabu ya kifo ni moja kwa moja inapingana na kanuni hii, na imejengwa katika tafsiri potofu ya haki/sheria.

**Haki imejengwa katika misingi ya uhuru na utu**

Mhalifu anaweza na anapaswa kuadhibiwa kwa sababu amehalifu sheria kwa matakwa/ridhaa yake. Ni kwa sababu hiyo hiyo watoto na watu wasio na akili timamu hawawezi kutiwa hatiani kwa matendo walioyafanya ndani ya mfumo wa makosa ya jinai. Adhabu ya kifo ni dhana inayokingana yenyewe kwani inamaanisha kuwa mara mtu anapotiwa hatiani na kuonekana kuwa alitenda kwa ridhaa yake na akijua anachotenda hapo hapo ananyimwa uhuru wake kwa adhabu ya kifo haiwezi kugeuzwa. ‘Uhuru wa mtu kwa hakika utatafsiriwa kama uwezekano wa mabadiliko na kugeuka kwa tabia ya mtu katika kuishi kwake na katika mfumo wa makosa ya jinai inahusisha uwezekano wa urekebishaji na urejeshaji, mtu katika maisha ya kawaida katika jamii. Kwa kuwa adhabu ya kifo ikishatekelezwa haiwezi kubadilishwa hali hii ni kinyume na dhana nzima ya uhuru na hadhi ya utu.
Hoja ya kutobadilika ina kipengele kingine. Hata katika mifumo ya kisheria ya kisasa kabisa yenye taratibu zenye kinga na tahadhari za kuhakikisha haki inatendeka bado upo uwezekano wa haki kutotendeka au kukosewa kwa adhabu ya kifo huenda ikatekelezwa kwa mtu asiye na hatia. Ni kwa sababu hiyo adhabu ya kifo inaweza kupelekea kunyongwa kwa watu wasiokuwa na hatia, Gavana Rejan aliamua kuanzisha ombi la kukawiza utekelezaji wa hukumu ya kifo huko Illinos baada ya kugundua kuwa wafungwa kumi na watatu waliokuwa wakisubiri kuuwawa/kunyongwa walikuwa hawana hatia ya makosa waliyotuhumiwa. Kwa hiyo mwezi January mwaka 2003 aliamua kubadili adhabu ya kifo kwa watu 167 kuwa adhabu ya kifungo cha maisha. *Ripoti ya tume ilisisitiza kuwa hakuna mfumo katika hali ya kibinadamu na udhalifu uliopo ambao utaweza kufanya kazi kwa uhakika kabisa na kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote asiye na hatia atakayehukumiwa tena kunyongwa.* Kwa hali hiyo basi Robert Badinter Waziri wa sheria wa Ufaransa mwaka 1981 alisema “jamii” katika ujumla wake yaani sisi wote ambao hukumu ilifikiwa kwa niaba yetu tutakuwa na hatia kwa ujumla wetu kwa kuwa mfumo wa haki umesababisha uvunjaji wa haki wa hali ya juu. Kwa jamii nzima kukubali uwezekano wa kuhukumu kifo cha mtu asiye na hatia ni kinyume cha haki za msingi za heshima ya utu na haki.

**Haki imejengwa juu ya misingi ya kuhakikisha haki za binadamu**

uwezekano wa uhakika wa haki za binadamu ni uthibitisho wa mfumo wa haki unaoaminika na wa kihalali. Hasa inajumiisha uhakika wa haki ya shauri kusikilizwa bila upendeleo ukiwemo kukataliwa kwa ushahidi uliopatikana kwa njia ya mateso na aina nyinginezo za matendo ya kudhalilisha. Kutokana na mtazamo huu FIDH inaamini kuwa heshima kamili ya haki za binadamu na kukataa ukatili uliokubalika kisheria ni mambo muhimu katika uhalali wa mfumo wowote wa makosa ya

jinai. Haki hasa katika makosa makubwa kabisa yanapohusika na maisha ya mtu yako hatarini haipaswi kufanyika kwa kubahatisha. Maisha ya mtu yasitegemee vigezo holela kama vile uchaguzi wa jopo la wanasheria/wazee wa baraza, msukumo wa vyombo vya habari na uwezo wa umilisi wa mwanasheria. Kukataa hukumu zisizo za kibinadamu hasa adhabu
ya kifo, ni wazi kuwa inachangia kujenga mfumo wa mahakama uliojengwa kwenye misingi inayokubalika kimataifa ambapo ulipizaji wa kisasi hauna nafasi na watu wote kwa ujumla wanaweza kuamini**.** **"Hali ya kusubiri adhabu ya kifo"** hii ni hali ya kufungwa kwa mtu aliyehukumiwa kifo wakati akisubiri kutekelezwa kwa hukumu yake. Hali ya kawaida ya kifungo hicho ni ile hasa ya muda mrefu kutengwa katika chumba cha pekee, kutokuwa na uhakika wa muda wa hukumu kutekelezwa na kunyimwa kuwasiliana na watu walio nje ya jela na wakati mwingine hata wanafamilia na wanasheria, mara nyingi haya yote kuchangia matendo ya kinyama.

**Haki kimsingi inatofauti kubwa sana na kulipiza kisasi**

Adhabu ya kifo si chochote zaidi ya mfumo wa haki ya jinai uliopitwa na wakati ambao umefikia katika kulipiza kisasi yaani yule atakayeua naye auawe.Ama ndiyo utekelezaji unavyofanyika itamaanisha kuwa mwizi naye aibiwe, mtesaji naye ateswe, mbakaji naye abakwe. Haki imekuwa zaidi ya dhana ya adhabu ya asili kwa kuridhia kanununi za kisheria lakini ziliweka uwiano wa kosa au madhara yaliyofanyika kama vile faini, kifungo, na mengineyo ambayo yanalinda utu wa wote aliyedhuriwa na aliyedhuru.

Zaidi ya hapo **FIDH haiamini ulazima wa kuwepo kwa adhabu ya kifo kama njia malipizi kwa aliyeathirika na jamaa zake.** FIDH inasisitiza kwamba haki ya wahanga ni ya msingi katika mfumo wa haki. Mateso ya wahanga ni wajibu muhimu katika uzuiaji wa haja ya kulipiza kisasi (ukweli wa kimahakama) FIDH inaamini kuwa kuitikia wito wa kutenda haki kwa adhabu ya kifo kunaleta hali ya faraja zilizohitajika kulipiza na haisaidii uletaji wa haki na heshima ya utu (hata ile ya wahanga wenyewe) katika ujumla wake. Kinyume chake, heshima ya utu wa mhanga inapaswa kuwa zaidi ya kulipiza kisasi tu. Utambulisho wa mhanga katika taratibu za makosa ya jinai kunatoa hitaji lake la kutambuliwa kama mtendaji ambapo mchakato huo una umuhimu wa kipekee kwake. Kutoa msaada wa kisaikolojia na fidia kwa waathirika pia kunachangia katika hisia zao kuwa haki inatendeka na hivyo kulipiza kisasi si lazima na haitasaidia kitu. Iwapo hali zilizoelezwa hapo juu hazitoshughulikiwa, haja ya waathirika ya kulipiza kisasi kwa njia ya adhabu ya kifo haina maana.

Vile vile FIDH inatambua kuwa adhabu ya kifo inatumika kiubaguzi kwa mfano Marekani ambapo inawahusu jamii ya watu walio wachache au Saudia Arabia ambapo wageni ndio wana uwezekano mkubwa wa kuhukumiwa adhabu ya kifo.

**2. Adhabu ya kifo haifai (haina nguvu)**

Katika hoja zinazotumika sana kutetea adhabu ya kifo ni kuwa inasaidia kupunguza uhalifu.
Inaelezewa kuwa adhabu ya kifo inalinda jamii dhidi ya watu waliohatari na kuzuia wengine wasije wakafanya uhalifu. Hoja hizi zimethibitishwa kutokuwa na ukweli wowote.
Je adhabu ya kifo inalinda jamii dhini ya uhalifu? Hailekei kuwa hivyo. Jamii zinazotumia adhabu ya kifo hazina ulinzi dhidi ya uhalifu kuliko zaidi ya zile jamii zisizotumia adhabu hiyo. Mahali ambapo kuna adhabu mbadala kama vile kifungo, ulinzi wa jamii, hautegemei kuwaondosha kimwili wahalifu. Zaidi ya hapo, inaweza kuelezwa kuwa tahadhari zinazochukuliwa kuzuia wanaosubiri, kuuwawa kujiua inaonyesha wazi kuwa kumuondosha kimwili mhalifu sio sababu ya msingi ya adhabu ya kifo. Kinachoonekana kuwa cha maana ni kwa adhabu hiyo kufanyika bila ridhaa ya

mfungwa kutokufahamu kwa adhabu hiyo ya kifo na adhabu nyingine za kikatili kumethibitishwa na tafiti mbalimbali. Tafiti zote makini zilizofanyika katika nchi kadhaa tofauti zinaonyesha kwamba adhabu ya kifo haisaidii kupunguza kiwango cha uhalifu Kwa mfano. Katika nchi ya Kanada kiwango cha mauaji katika kila watu 100,000 kimepungua katika kiwango cha juu cha 3.09 mwaka 1975 kabla ya kupiga marufuku adhabu ya kifo kwa kosa la mauaji hadi kufikia 2.41 mwaka 1980. Katika mwaka 2000 wakati Marekani kulikuwa na mauaji 5.5 kwa kila watu 100,000, Kanada kulikuwa na mauaji 1.8 katika kila watu 100,000.

Katika utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Roger Hood, kwa ajili ya umoja wa mataifa katika mwaka 1988 na kutwaliwa (kurudiwa) mwaka 2000 katika majumuisho yake "ukweli kwamba takwimu zinaelekea kule kule ni ushahidi wa ushawishi kuwa nchi zisihofiye kufanya mabadiliko ya dhati katika mtiririko wa makosa iwapo watapunguza kutegemea adhabu ya kifo.[1]

Ni wazi kwamba jambo hili si la kushtukiza. Mhalifu hafanyi kosa kwa kufikiria/kutegemea uwezekano wa adhabu itakayomkabili kwa kudhania ya kuwa atapata adhabu ya kifungo cha maisha na si adhabu ya kifo. Zaidi ya hilo kama alivyo bainisha Beccaria katika karne ya 18, ni kichekesho!! kwamba sheria ni kielelezo cha matakwa ya umma na ambacho kinachukia na kuadhibu muuaji na zenyewe zinatekeleza hilo ("Zinaua/zinatoa adhabu ya kifo") kuwazuia raia kutokana na uuaji lazima watoe amri ya mauaji ya hadhara.
***Hatimaye FIDH inabainisha kwamva adhabu ya kifo aghalabu ni kiashiria muhimu cha heshima ya binadamu katika nchi husika.***

## 3. Hoja kutoka kwenye sheria za kimataifa za haki za za binadamu

Mabadiliko/mageuzi ya sheria za kimataifa yanaelekezwa katika ukomeshaji wa hukumu ya kifo. Hali ya mahakama ya kimataifa ya Rome ya makosa ya jinai na maazimio ya baraza la usalama la umoja wa mataifa lililoanzisha mahakama ya kimataifa ya makosa ya jinai kwa Yugoslavia ya zamani na Rwanda hayatoi hukumu ya kifo kwa vikwazo mbalimbali ingawa mahakama hizo zimeanzishwa kusikiliza mashauri mazito/makubwa. Vyombo maalum vya kimataifa na kikanda vimeridhiwa na ambavyo vinataka uzuiaji wa adhabu ya kifo.

Hati awali ya pili kwenye Umoja wa Mataifa katika mkataba wa kimataifa juu ya haki za raia na kisiasa (ICCPR), Hati awali kwenye mkataba wa Marekani juu ya haki za binadamu kukomesha adhabu ya kifo. (Mashirika ya nchi za Marekani), Hati awali ya 6 na hali awali mpya ya 13 kwenye makubaliano ya Ulaya juu ya haki za binadamu (Baraza la Ulaya) linahiji ukomeshaji wa adhabu ya kifo. Miongozo kwenye sera za EU kuhusiana na nchi za ulimwengu wa tatu juu ya adhabu ya kifo, iliyoridhiwa na Muungano wa nchi za Ulaya ni tarehe 29,Juni, mwaka 1998, husisitiza kwamba lengo moja la EU ni "kufanyia kazi ukomeshaji wa adhabu ya kifo kiulimwengu kama mtazamo wa sera iliyoshikiliwa kwa nguvu zote na kukubaliwa na nchi wanachama wa EU" zaidi ya hayo madhumuni ya Muungano wa Ulaya mahali ambapo bado kuna adhabu ya kifo matumizi yake kuendelea kuzuiwa na kusisitiza kwamba ifanyike kulingana na viwango vya kiwango cha chini (---). EU itafanya madhumuni/malengo haya kujulikana kama sehemu muhimu ya sera zake za kibinadamu. Mkataba mpya wa haki za Msingi ulioridhiwa na EU pia hutamka kwamba "Hakuna yeyote atahukumiwa adhabu ya kifo au kunyongwa".

Katika ngazi ya ulimwengu, hata kama ICCPR inaeleza utoaji wa adhabu ya kifo kama ni haki maalum katika maisha na inazingirwa na kinga kadhaa maalum na maoni ya jumla yaliyoridhiwa na

[1] Roger Hood, The Death Penalty: A worldwide perspective 31 ded [London: Oxford University Press 2002) 214

kamati ya haki za binadamu inatamka wazi kuwa, kifungu cha sita (6) juu ya haki ya kuishi "inarejelea kiujumla kwenye ukomeshaji katika hali ambayo hoja za nguvu zinatoa pendekezo kwamba ukomeshaji ndio unaopendekezwa Hatua zote za ukomeshaji lazima zifikiriwe kama hatua ya kufurahia haki ya kuishi. Zaidi ya hayo katika azimio lake la **1745 la Mei 16 1973, Baraza** la Umoja wa Mataifa la uchumi na jamii.

lilimkaribisha Katibu Mkuu kuwasilisha katika vipindi vya miaka mitano ripoti/taarifa zilizotwaliwa na kuchambuliwa juu ya adhabu ya kifo. Katika azimio lake 1995/57 la tarehe 28 Julai 1995.

Baraza lilipendekeza kuwa ripoti / Taarifa za miaka mitano, za katibu mkuu pia zingeshughulikia utekelezaji wa ulinzi utoao dhamana ya kinga ya wale wanaokabiliwa na hukumu ya kifo.[2] Kila mwaka kuanzia 1997 tume ya umoja wa mataifa juu ya haki za binadamu imetoa wito kwa mataifa yote yale ambayo bado yanaendeleza/yanatekeleza adhabu ya kifo[3] kuanzisha/kufikiria kutoa azimio juu ya unyongaji ukiwa na lengo la kukomesha kabisa hukumu ya kifo tarehe 8 desemba 1977; baraza la umoja wa mataifa pia liliridhia azimio juu ya adhabu ya kifo linalotamka.

"Lengo kuu linalotarajiwa katika nyanja ya adhabu ya kifo ni lile lenye maendeleo ya uzuiaji wa idadi ya makosa ambayo yanayoweza kupelekea adhabu ya kifo kwa mtazamo wa hoja ya ukomeshaji wa adhabu ya kifo.[4]

---

[2] ecosoc RESOLUTION 1984/50 of May, 1984

[3] Angalia hasa resolution 2002/77, 2001/68, 2000/65 na 1999/61

[4] UN General Assembly resolution 32/61, 8 December 1977, aya ya 1.

## Utangulizi

Katika muundo wake wa kujihusisha na kampeni za ukomeshaji wa adhabu ya kifo duniani, FIDH inapeleka ujumbe wa kimataifa wa uchunguzi katika nchi ambazo adhabu hii ya kikatili inatamkwa au hata kutekelezwa.

Ujumbe huu una malengo manne: (1) Kuielezea adhabu hii ya kinyama vinginevyo. Asilimia 80 za nchi zimepiga marufuku adhabu ya kifo kisheria, asilimia 15 imepiga marufuku adhabu hiyo kwa makosa yote isipokuwa kwa makosa maalum kama yote ya kivita na asilimia 23 za nchi zinaweza kuchukuliwa au kufikiriwa kama zimekomesha. Wameibakiza adhabu hiyo kisheria lakini hazijatekelezwa mauaji kwa muda wa miaka 10 au zaidi. (2) Kuonyesha kuwa wafungwa waliopatikana na makosa au walionyongwa duniani pote hawakunufaika kutokana na haki ya hukumu kama ilivyoainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948 na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa 196. Hii inafanya idhini za nchi za kutekeleza adhabu ya kifo kutokubalika. Huu ujumbe wa uchunguzi pia una nia ya (3) Kuweka wazi na kulaani vitendo wanavyotendewa wafungwa wanaosubiri kunyongwa kutoka kushitakiwa hadi hukumu ya kifo; Hali ya wafungwa hawa mara nyingi inapelekea “ukatili, matendo ya kumshushia mtu heshima” iliyokatazwa na sheria za Kimataifa za Haki za Binadamu. (4) Kwa kubeba ujumbe kama huo wa uchunguzi FIDH inahitaji kutoa maoni kwa viongozi na nchi zinazohusika na pia kwenye sekta zinazohusika katika hali ya mazungumzo ili waunge mkono juhudi zao zinazohusika pia kwenye nyingine zinazohusika, katika hali ya mazungumzo ili waunge mkono juhudi zao zinazolenga ukomeshaji wa adhabu ya kifo au hatua ya kwanza kuelekea kukubali azimio la kukomesha hukumu ya kifo.

Katika Tanzania hakuna unyongaji uliofanyika tangu mwaka 1994. Hata hinyo mtu mmoja mmoja mara kwa mara walihukumiwa kunyongwa lakini hakuna takwimu zilizochapishwa juu ya idadi ya hukumu. Kwa hiyo FIDH iliamua kutuma ujumbe wa kimataifa ili kufuta ukweli katika Tanzania, uliolenga katika hukumu ya kifo na uendeshaji wa kesi za jinai. Ripoti iliyopo ni matokeo ya uchunguzi wa ujumbe wa kimataifa ambao ulifanywa na wajumbe wawili wa FIDH, Arnold Tsunga Zimbabwe mwanasheria na Rais wa Zimrights na Eric Mirguet (Ufaransa), wanasheria walifanya uchunguzi huo Tanzania toka tareke 6 hadi 19 oktoba 2004 . Ujumbe huo ulikuwa umetayarishwa kwa pamoja na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambacho ni mwanachama wa FIDH Tanzania ambacho FIDH inatoa shukrani zake za dhati. Ujumbe ulikutana na zaidi ya watu 40 wakiwemo wataalam wa sheria, vyama vya wanachama wa sheria, mawakili, makamu wa mwenyekiti wa tume ya haki za binadamu na utawala bora, mwenyekiti wa kamati ya haki za binadamu ya chama cha wanasheria Tanganyika, Mwenyekiti wa tume ya kurekebisha sheria. Ujumbe pia ulikutana na mkurugenzi wa mambo ya katiba na haki za binadamu (Wizara ya sheria na mambo ya katiba), Mkurugenzi wa makosa ya jinai, wawakilishi wa vyama vya siasa na polisi.

Zanzibar, tume ilikutana na makamishina na wasaidizi wa polisi, kamishina msaidizi wa magereza, Naibu mwenyekiti wa chama cha Wanasheria, Katiba Mkuu Idara ya Katiba na Utawala Bora na naibu mwanasheria mkuu wa serikali, na wanaharakati kadhaa wa haki za binadamu na walitoa maoni yao kwa ujumbe wa FIDH.

FIDH ingependa kuwashukuru viongozi/wakuu wa Tanzania kwa ushirikiano wao na hasa wakuu Zanzibar ambao walijibu kwa wakati maombi yake na kuwaruhusu wajumbe kukutana kwa uhuru na wafungwa waliohukumiwa kunyongwa. Kwa bahati mbaya wakuu wa Tanzania bara wamekuwa na ushirikiano hafifu kwa vile wakuu wa magereza walikataa kutoa fursa ya kuvifikia vyombo mbalimbali vya magereza kwa kudhani kwamba ujumbe kama huo haukuhusiana na uchunguzi,

wazo ambalo FIDH ilikataa kwa nguvu zote. FIDH iliomba kutembelea magereza yafuatayo Gereza la Tanga, Gereza la Dodoma, na Gereza la Morogoro.

Taasisi ya kuzuia rushwa pia ilikataa kuupokea ujumbe mbali ya maombi kadhaa na kuzitembelea mara kadhaa ofisi za Dar es Salaam. Haya ni maamuzi ya kusikitisha ikiwa rushwa ilionekana tishio katika utawala wa sheria kila mahala nchi nzima na wajumbe walifikiria ni muhimu sana taarifa hii kupatikana kutoka kwao.

FIDH pia ingependa kuyashukuru mashirika mengi ya nchini ambayo yamesaidia na kuwaongoza wajumbe katika utafiti wao, na hasa kitengo cha shirika la kimataifa la kutetea haki za wakimbizi ambao limewapatia wajumbe taarifa muhimu na ushauri.

## I. Mfumo wa Kisiasa na Kimahakama Tanzania

Jamhuri ya muungano wa Tanzania iko Afrika ya Mashariki. Upande wa Kaskazini imepakana na Kenya na Uganda, upande wa Mashariki imepakana na bahari ya Hindi, na Kusini imepakana na Msumbiji, Malawi na Zambia, na upande wa Magharibi imepakana na Rwanda na Burundi ziwa Tanganyika na Jamhuri ya Kongo Tanzania inajumuisha visiwa vya Zanzibar na Pemba na visiwa vingine kwenye bahari ya Hindi.

Tanzania ina jumla ya eneo la kilometa za mraba 945,100 na ina idadi ya watu 34,569,232. Kuna makundi ya makabila karibuni 130 katika Tanzania na karibuni lugha zao hufanana na lugha ya kibantu. Watu wenye asili ya kihindi na kiarabu hufanya 1% ya idadi ya watu wote na ambao wengi wao hupatikana Zanzibar. Lugha rasmi ni Kiswahili na Kiingereza hata hivyo Kiswahili ni lugha ya Taifa. Kiswahili ndio lugha itumikayo kufundishia katika shule ya msingi wakati Kiingereza kinatumika katika kiwango cha elimu ya juu.

Mijadala Bungeni huendeshwa kwa lugha ya Kiswahili, wakati mfumo wa mahakama unaendeshwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa mahakama ya mwanzo ambapo mashauri yote lazima yaendeshwe kwa Kiswahili.
Dar es Salaam ni mji mkuu wa nchi wa zamani na sasa ni kituo cha biashara na jiji kubwa kuliko yote katika Tanzania.

Bunge la Tanzania limehamia Dodoma kwenye makao mapya ya shughuli za utawala za serikali mnamo mwaka 1996, lakini ofisi nyingi za serikali bado ziko Dar es Salaam.

### 1. Kuanzishwa kwa Taifa

Tanzania ni Jamhuri ya muungano. Ni muungano wa nchi mbili za zamani. Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya watu wa Zanzibar ambazo zilikuwapo kama nchi tofauti hadi tarehe 26 Aprili 1964 zilipoungana.

Tanganyika sasa inajulikana kama Tanzania bara na ilipata uhuru mnamo 9 Desemba 1961 na mwaka mmoja baadae kuwa Jamhuri.

Zanzibar ambayo inajulikana kama Tanzania visiwani ilipata uhuru tarehe 10 Desemba 1963, mwezi mmoja baadaye, kwenye tarehe 12 Januari 1964 kulikuwa na mapinduzi ambayo yalimwondoa

Sultan, na kupelekea katika kusimaisha katiba. Kwa miaka 15 iliyofuata Zanzibar ilitawaliwa na amri za Rais (Presidental decree).

Muungano ulikubali namna kwamba serikali ya Tanganyika iliondoka wakati ile ya Zanzibar ilibaki kama ilivyokuwa. Kwa hiyo Zanzibar ina Serikali ya peke yake. Rais, Mahakama na Baraza la Wawakilishi likiwa kama Bunge la Zanzibar.

Taasisi za Muungano zinahudumia Tanzania Bara. Mpango huu umefanya Watanzania Bara kupigania mara kwa mara kutaka Serikali tofauti ya Tanganyika na suala hili ni kipengele kimesimama kwenye agenda ya kisiasa.

Katika suala la ulinzi na uimarishaji wa haki za binadamu Tanzania Bara na Zanzibar zina historia tofauti[5].

Wakati wa uhuru 1963, Zanzibar ilibainisha haki za msingi za binadamu na uhuru katika katiba yake kupitia Misingi ya Haki za binadamu. Hata hivyo, katiba hii haikudumu zaidi ya mwezi mmoja. Baada ya mapinduzi ya Januari 12, 1964, ilitupiliwa mbali na kilichofuata ilikuwa ni utawala wa mtu mmoja kwa amri za Rais.

Kwa Tanzania Bara, dhamana ya haki za msingi na uhuru katika sheria za haki za binadamu zilikataliwa na serikali mpya baada ya uhuru.

Wakati wa mapatano ya uhuru kwenye miaka ya 1960, Waingereza walisisitiza juu ya kujumuisha sheria ya haki za binadamu katika katiba ya uhuru wa Tanganyika. Wananchi wakiongozwa na Tanganyika African National Union (TANU) walikataa wakidai kuwa misingi kama hiyo ingezuia serikali mpya katika juhudi zake za kuendeleza nchi. Ni katika muktadha huu aliyekuwa Waziri Mkuu kwa wakati huo, Rashid Kawawa alichukulia misingi ya haki za binadamu kama ni anasa ambazo zinakaribisha mfarakano.[6]

Kulingana na mawazo ya Chris Peter Maina, Profesa wa sheria katika Idara ya Sheria za Kimataifa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuijumuisha misingi ya haki za binadamu katika katiba wakati wa uhuru ungekuwa kama muongozo wa baadhi ya maamuzi mengi yasiyo ya kidemokrasia yaliyofanywa awali na ambazo zilizoimarisha utamaduni wa kutoheshimu misingi ya haki na uhuru na kutofuata utawala wa sheria na katiba kwa chama tawala na serikali yake.[7] Kwa mfano isingewezekana kuamua mfumo wa siasa ya chama kimoja[8] kwa sababu kwamba ingekuwa ni kwenda kinyume na haki ya ushirika wa kisiasa na uhuru wa kujieleza na kutoa maoni.

---

[5] Tazama/Angalia Chris Maina Peter; Human Rights in Tanzania Selectarial Cases and Materials Reudger Coppevertag Koln

[6] Angalia mjadala Bungeni. National Assembly 3rd Meeting, 1088, 28th June 1962.

[7] Ibid, pages 3 - 4

[8] Katiba ya mpito Tanzania, iliyoridhiwa mwaka 1965 iliyotolewa katika kifungu chake cha 3(1) kwamba kutakuwa na chama kimoja cha siasa Tanzania.

Mwanya huu pia ulitoa nafasi kwa serikali iliyokuwepo madarakani wakati huo kufunga msululu wa sheria za ugandamizaji na za kuchukiza.[9] Hizi zilikuwa sheria ambazo zisingeweza kuhimili uthibiti wa katiba mfano wa katiba ambao sheria za haki za binadamu umefungwa katika katiba.

Katiba mpya iliyopitishwa katika mwaka 1977 haikuwa na sheria ya haki za binadamu kama ile iliyotangulia. Ni katiba ya mwaka 1983 tu ambapo mabadiliko yateteayo ujumuisho wa masharti kama hayo katika katiba ulipata nguvu na ikapelekea Marekebisho ya Tano kwenye katiba, katika mwaka 1984 ujumuishaji wa misingi ya haki za binadamu katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mabadiliko haya yalianza kutumika mwezi Machi 1985. Hata hivyo, uwezekano wa kupinga ufungaji wa sheria za nchi kikatiba (hasa zinazohusu/lenga kwenye udhamini wa sheria ya haki za binadamu kikatiba) mbele ya mahakama zilisimamishwa kwa kipindi cha miaka mitatu na sheria ya katiba 1984[10]. Na Mswada ulikuwa na vifungu kadhaa vyenye mapungufu jina lililopewa vifungu hivyo vinahusu uvunjaji wa masharti yaliyowekwa katika Mswada kwa sheria iliyopitishwa na Bunge. (Vifungu hivyo vimejumuisha mchanganuo kama "kutegemeana na sheria husika za nchi", au "bila kuathiri sheria za nchi"[11]).[12]

Mwisho wa kipindi cha miaka mitatu cha usimamishwaji, vifungu hivi havikurekebishwa na serikali na ilikuwa ni kwa Mahakama Kuu kuamua uhalali kikatiba wa sheria mbalimbali.
Hata hivyo, suala lazima hili lifikishwe mbele ya mahakama na mtu anayeshitaki ama wakati mahakama inapoamua yenyewe (Poprio motu) kama njia mojawapo ya kutekeleza mamlaka iliyopewa. Matokeo yake, sheria ambazo hazipingwi mahakamani, vyovyote zitzkavyokua, zitabaki katika sheria.

---

[9] Kwa mfano, sheria ya kuwekwa kizuizini ya mwaka 1962, ambayo inampa Rais uwezo kumuweka kizizini kwa muda usiojulikana "mtu yoyote … aliyemuona mwenyewe kuwa ni hatari kwa amani na utulivu" au mtu yeyote "anayefanya mambo kwa namna ya kuleta madhara katika ulinzi … au usalama wa nchi". Sheria hii inapoka mamlaka ya mahakama, "hakuna amri chini ya sheria hii itakayo hojiwa katika mahakama yoyote". Katika mwaka wake wa mwisho akiwa Rais, Nyerere, wakati akihutubia majaji na mahakimu alisema kwamba: "Katika matukio mengi tumetumia sheria hii kuwakamata wahalifu, au watu wanaoaminika kuwa wahalifu, ambao matendo yao hayaendani na usalama wa nchi. Huu ni utumiaji mbaya wa sheria ya lazima na inaweza kuleta matumizi ya ukwepaji wa matumizi ya mwenendo wa kawaida wa sheria kwa makosa ya jinai. Ni muhimu tujirekebishe sisi wenyewe katika hili, na nina uhakika kwamba mtu wa kwanza ambaye anapaswa kujisahihisha ni Rais". Masharti kama hayo yamo katika sheria ya kuhamisha wahalifu. Sheria zote zinatumika kama ukinzani wa utaratibu wa kawaida wa mahakama.

[10] Pasipo kuzingatia marekebisho ya katiba na hasa masharti ya sheria yanayorandana na haki za msingi, uhuru na wajibu, hakuna sheria iliyopo au masharti mengine yoyote katika sheria yoyote iliyopo ingeweza hadi baada ya miaka mitatu kutoka tarehe ya kuanza kwa sheria, ingetafsiriwa na mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano kama sio ya kikatiba au vinginevyo haiendani na masharti ya katiba.

[11] Haki ya kumiliki mali, uhuru wa kujieleza, uhuru wa dini na uhuru wa kujumuika ukijumuisha vifungu vyenye kuondoa tena haki hizo (claw back clasues). Haki ya kuishi inatamkwa katika hali hiyo hiyo (inatolewa "kwa mujibu wa sheria"), kinyume na sheria za kimataifa. Mwaka jana sheria ilipeleka Bungeni muswada wa marekebisho ya 14 ya katiba, Oktoba 2003, ili kuondoa kutoka kwenye katiba baadhi ya vifungu vya sheria vinavyo toa haki na kuzinyang'anya kwa upande mwingine (claw back clauses). Hata hivyo, vifungu vilivyopendekezwa kutolewa vilikuwa ni vile

[12] Lazima itiliwe mkazo hata hivyo, kwamba mnamo Februari 2005 Bunge lilikusudia kurekebisha katiba na kati ya marekebisho hayo inafikiriwa uondoaji wa vifungu hivyo vyenye utata (claw back clause). Lakini ni katika vifungu 18 hadi 24 tu vya katiba. Vifungu vingine kama vile vinavyotoa sheria ya haki za binadamu na wajibu … vifungu 12 hadi 17 na 25 hadi 29 vitabaki kama vilivyo kwa maana kuendelea kuwa na utata. Sheria yoyote ile ni lazima kwanza iidhinishwe na Rais na kutangazwa kutumika kwake katika gazeti ka serikali na Waziri anayehusika.

Pia, katiba hii mpya ilitoa changamoto katika sheria za nchi: Demokrasia ya chama kimoja, ikiruhusu mikusanyiko ya amani, kujumuika na kujieleza, lakini ikizuia uanzishaji wa chama kingine cha siasa na kuwaweka kizuizini wale wote waliojaribu kuanzisha chama cha upinzani.[13]

Katika marekebisho ya nane kwenye katiba ambayo yalianza kutumika tarehe 1 Julai 1992, Ibara ya 3 ya katiba ambayo iliainisha mfumo wa chama kimoja, na kurekebishwa kuainisha mfumo wa vyama vingi. Ibara ya 10 ambayo ilianisha utawala wa chama kimoja kuwa na mamlaka ya juu kabisa na ukiritimba wa shughuli za kisiasa katika nchi ilifutwa.

Chama tawala kilikuwa (na bado ni) Chama Cha Mapinduzi (CCM). Chama cha Wananchi (The Civil United Front) (CUF) kwa ujumla kinachukuliwa kama chama kikuu cha upinzani hasa Zanzibar. Kwa nyongeza, kuna vyama vingine 14 vilivyosajiliwa kihalali. Vyama hivyo katika mpangilio rasmi wa kusajiliwa, Chama Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Union for Multiparty Democracy (UMD), National Convention for Construction and Reform (NCCR-M), National League for Demecracy (NLD), National Reconstruction Alliance (NRA), Tanzania Demecratic Alliance Party (TADEA), Tanzania Labour Party (TLP), United Democratic Party (UDP), United People's Democratic Party (UPDP), Chama cha Haki na Ustawi (CHAUSTA), Demokrasia Makini (MAKINI), The Forum for Restoration of Democracy (FORD) and Progressive Party of Tanzania na PPT–Maendeleo.

Marais wote wa Tanzania Bara na wa Zanzibar wote ni wanachama wa CCM. Hata hivyo CUF kina nguvu katika visiwa vya Zanzibar. CCM, CUF, TLP, CHADEMA na UDP vyote vinawakilishwa kote kwenye Bunge na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mwaka 1995, uchaguzi wa kwanza wa Rais kupitia mfumo wa vyama vingi katika kipindi cha miaka 31 uliandaliwa, na ulishuhudia ushindi wa Benjamin William Mkapa ambaye bado ni Rais wa Tanzania kwa sasa.

Salmin Amour alishinda uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi Zanzibar. Amani Abeid Karume ni Rais wa Zanzibar kwa sasa tangu uchaguzi wa Oktoba 2000, ambao ulikuwa na hitilafu kubwa kulingana na waangalizi wa kimataifa[14] .Chaguzi nyingine zimepangwa Oktoba 2005.

## 2. Mfumo ya Sheria ya Makosa ya Jinai Tanzania

Mahakama Tanzania zinatumia sheria za kimila sheria, sheria kuu na sheria za Uingereza.

Mfumo wa mahakama za makosa ya jinai yanajumuisha mahakama za mwanzo, mahakama za Wilaya/mahakama za hakimu mkazi, mahakama kuu na mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

---

[13] Baada ya uhuru serikali, ilitunga sheria ya uhamishaji wahalifu ikimruhusu Rais kuamuru mtu yeyote ahamishwe kutoka sehemu yoyote nchini kwenda kwingine "ikionyesha katika kiapo na Rais kuridhishwa na kiapo kwamba mtu kama huyo anaonyesha mwenendo wake kuwa ni hatari kwa amani na utulivu …… au anataka kuchochea uadui kati ya watu wa Tanzania na serikali". Viongozi wengi wa upinzani walipelekwa maeneo ya mbali katika miaka 1960 chini ya sheria hii, ambayo ilitamkwa siyo ya kikatiba mwaka 1991.

[14] Mwenyekiti wa Tume ya Waangalizi wa Umoja wa Mataifa alibaini; "Tunahitaji kuweka kumbukumbu ya huzuni na masikitiko yetu" naamua ambavyo wapiga kura wengi walitendewa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Katika sehemu nyingi uchaguzi huu ni wa vurumai. Sababu ama uwezo wa chini ama jaribio la makusudi la kuharibu sehemu ya uchaguzi huu. Vyovyote vile matokeo yake ni dharau kubwa kwa wazanzibar wa kawaida na shauku yao ya demokrasia". Angalia pia Taarifa ya FIDH kuhusu uchguzi wa Zanzibar, 2000; "Wave of Violence an Electiona Mismanagement and Police Brutality in Zanzibar Publsihed in June 2001. (http://www.fidh.org/artcle.php3?id_article=1000

Mahakama kuu ndiyo mahakama yenye mamlaka ya awali kwa makosa makubwa kama mauaji na uhaini katika uendeshaji wa mashtaka. Jaji katika mahakama kuu anakaa na wazee wa baraza ambao maoni yao maoni yao hayabadili maamuzi. Rufaa inaanzia mahakama ya mwanzo, kupitia Mahakama ya Wilaya na mahakama za mahakimu wakazi mpaka Mahakama Kuu na Mahakama za Rufaa.

Shauri katika Mahakama Kuu haliwezi kuanza kusikilizwa kabla ya uchunguzi wa awali (committal proceedings) kufanyika katika mahakama za mahakimu wakazi, kama iliyvoainishwa kwenye vifungu 178, 243 na 244 vya sheria za mwenendo wa makoa ya jinai ya 1985.

Kifungu cha 173 kinampa madaraka waziri wa sheria kumpa uwezo Hakimu Mkazi yoyote kusikiliza aina yote ya mashitaka ya kikijumuisha mauaji, ambayo kwa kawaida yangesikizwa na Mahakama Kuu. Kifungu 175 cha sheria huweka wazi zaidi kwamba kila hukumu ya kifo iliyopitishwa na mahakama ya chini kwa madaraka iliyopewa chini ya kifungu cha 173 kama/iwapo mshtakiwa hatakata rufaa kwenye Mahakama Kuu itathibitishwa na Mahakama Kuu.

Rufaa dhidi ya hukumu za Mahakama Kuu na zile kutoka kwenye mahakama za chini zilizoongezwa uwezo wa mamlaka ya kisheria zipelekwe Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

Rufaa kutoka Mahakama Kuu ya Zanzibar pia kwenda kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.
Polisi waendesha mashtaka huendesha mashtaka katika mahakama za Hakimu Mkazi. Wanasheria wa serikali wanaendesha mashitaka hayo katika Mahakama Kuu ambayo ndiyo yenye mamlaka ya kushughulikia kesi za mauaji na uhaini.

Kwa makosa makubwa yenye kutolewa adhabu ya kifo kama mauaji na uhaini, mshtakiwa ana haki ya moja kwa moja ya kupata usimamizi wa mwanasheria.

Desemba 2003 Tanzania bara ilikuwa na wanasheria 735 waliokubaliwa uwakili, kati yao 641 walikuwa walikuwa wakijihusisha moja kwa moja na kazi za uwakili. Katika mwaka huo zaidi ya asilimia 80 ya mawakili wafanyao kazi ya uwakili (practicing Advocate), waliweka makazi yao katika jiji kubwa kuliko yote la Dar es Salaam. Kulingana na idadi ya sasa ya watu 34,569,232 kuna wakili mmoja katika kila watu 53,930.

Mawakili hupewa kazi ya kuwawakilisha washtakiwa wasiokuwa na uwezo kwenye Mahakama Kuu na kwenye rufaa. Kifungu 310 cha sheria ya mwenendo wa mashtaka ya makosa ya jinai ya mwaka 1985 inatamka. "Mtu aliyeshtakiwa mbele ya Mahakama ya makosa ya jinai, isipokuwa kwa mahakama ya mwanzo kama haki yake, anawaeza kutetewa na wakili wa Mahakama Kuu. Vinginevyo, sheria ya msaada washeria (mwenendo wa mashtaka ya jinai) ya 1969 inatamka "ambapo katika mashauri yoyote inaelekea kwa mamlaka zinazothibitisha hiyo ni kwamba inafaa katika misingi ya haki, kwamba mshtakiwa angepaswa kupatiwa masaada wa sheria katika utayarishaji na uendeshaji wa utetezi wake au kukata rufaa kama shauri litakavyokuwa na kwamba hana uwezo wa kupata msaada kama huo, wenye mamlaka ya kithibitisha wangethibitisha kwamba mshtakiwa anapaswa kupata msaada wa kisheria na katika cheti kama hicho kikitoka na msajili pale inapowezekana kufanya hivyo, inampatia mshitakiwa wakili kwa madhumuni ya matayarisho na kuendesha utetezi wake au rufaa kama itakavyokuwa (kifungu3).

Mahakama ya watoto ya makosa ya jinai kimsingi inaendeshwa chini ya sheria ya watoto na vijana ya 1937 sura 13.

Zanzibar ina mfumo wake wa sheria za makosa ya jinai.

## 3. Kuridhiwa kwa mikataba ya haki za binadamu.

Tanzania ni mwanachama kwenye mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ikijumuisha (lakini si kikomo kwa):

- Mkataba wa kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa 1966 (The international covenaton civil and political Rights (ICCPR), 1966.
- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Utamaduni wa 1966[15] (The International Covenanton, Economic Social and Cultural Rights (ICESCR) of 1966);
- Mkataba wa Kimataifa wa Ukomeshaji wa Aina Zote za Ubaguzi wa 1972 (The International Convention of the Elimination of All Forms of Recial Discrimination of 1972[16])
- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto wa 1989 (The International Convention on the Rights of the Child of 1989[17]).
- Mkataba wa Roma wa Mahakama za Kimataifa za Jinai (The Rome Statute of the International Criminal Court)[18]
- Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za watu wa 1981 (The African Charter on Human and People' Rights of 1981)[19].

Tanzania ni nchi ya mifumo miwili ya sheria ambapo masharti ya mikataba ya kimataifa hutumika katika sheria za nchi baada ya uridhiaji wa ujumuisho wake katika utungaji wa sheria za nchi[20] sheria kama hizo nchi hazijaridhia hadi leo ingawa ujumbe wa FIDH umetaarifiwa na Bwana Frederic Werema Mkurugenzi wa idara ya mambo ya katiba na haki za binadamu kwenye wizara ya sheria na mambo ya katiba na kwamba kundi la kufanya kazi limeanzishwa juu ya utekelezwaji wa sheria ya Rome ambayo bado kuchukua hatua mahsusi juu ya sulala hilo[21]. Jaji Bahati, mwenyekiti wa Tume ya urekebishaji wa sheria iliwarifu wajumbe kwamba tume pia inafanyia kazi suala hilo lakini kwamba haikutoa pendekezo lolote juu ya mikataba ya haki za binadamu katika hatua hii.

---

[15] Mikataba hii iliridhiwa mnamo tarehe 11 Septemba, 1976.
[16] Uliridhiwa tarehe 26 Novemba, 1972
[17] IUliridhiwa tarehe 10 Julai, 1991.
[18] Uliridhiwa tarehe 20 Augosti 2002
[19] Uliridhiwa tarehe 18 Februari 1984
[20] Hata hivyo katika shauri la Jaji Mwalusanya ilichukuliwa kwamba aliuwa na wazo la kufikiriwa kwamba vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu na maamuzi ya Mahakama ya nchi nyingine ilitoa taarifa muhimu na uongozi katika kutafsiri haki za kimsingi za binadamu katika katiba yetu na hivyo hakimu katika hali yangu iliyopo angeziangalia katika kutafuta jibu/suluhu. Tunahitaji wanachama zaidi wa Idara ya Mahakama wataridhia hali hii/nafasi hii. Angalia mapitio ya Sheria za Tanzania (TLR) = Tanzania Law Review ya mwaka 1994, Ukurasa 151, kwa nyongeza kanuni ya Bangalore (Bangalore Principle) iliyoridhiwa na kundi la maaji wa jumuiya ya Madola, walitambua na kuthibitisha uhalali na umuhimu wa ongezeko la hali ya mahakama kuwa na hoja katika hizi desturi za kimataifa kwa madhumuni ya uamuzi wa mashauri/kesi ambapo sheria za nchi ambazo ni sheria za kikatiba au sheria za kawaida za kila siku si za uhakika au zenye mapungufu. Majaji wa jumuia za madola katika Azimio la Harare la Haki za Binadamu na pia katika uthibitisho wa Banjul uliridhia wazo hilo. Kulingana na ubani dhidi ya Mkurugenzi wa huduma za usalama wa nchi Anor (1999), Mahakama ya Rufaa ya Nigeria ilisema (held) kwamba mkataba wa Afrika juu ya haki za binadamu na watu ni bora/kubwa kwa sheria za mabaraza ya mji (municipal laws) zikiwemo hukumu za kijeshi. Katika Afrika ya Kusini umoja wa ulinzi dhidi ya Waziri wa Ulinzi wa Anors mahakama ya kikatiba ilisema mikata hiyo ni husika kwa tafsiri ya masharti ya kikatiba.
[21] Kushindwa kutekeleza sheria za ICC zilishutumiwa/zilikataliwa na mashirika ya ndani/nchi kwa miaka kadhaa bila ya kuchukua hatua yoyote toka serikali (reaction from Government). FIDH inakumbuka kwamba kulingana na ICC Tume ya Afrika ilizitaka nchi ambazo zimerekebisha sheria za ICC kwa haraka zilijumuisha katika sheria zao za nchi ili kuweza kushiriki kikamilifu na ICC na kutekeleza kanuni za ukamilisho na mahakama zao za kitaifa. Angalia Azimio juu ya urekebishaji wa sheria katika mahakama ya kimataifa za makoa ya jinai na nchi wanachama wa OAU Preteria Afrika ya Kusini May, 2002. (The International Criminal Court by OAU members state, Pritoria South Africa, May 2002).

# II. Hukumu ya kifo na viwango vya kimataifa

## 1. Mfumo wa Umoja wa Mataifa

Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR) lilivyoazimiwa kwa mara ya kwanza, kulikuwa na mjadala mkubwa miongoni mwa nchi wanachama ama kuwepo au kusikuwepo maelezo ya kawaida kwamba nchi wanachama zingeweza kuchukua hatua za ukomeshaji wa hukumu ya kifo au hukumu ya kifo ingejumuishwa kama kielelezo maalumu kwenye haki kuishi. Kama ilivyo karibu nchi zote zilikuwa zikitekeleza hukumu ya kifo wakati ule, maelezo ya kuunga mkono ya kupiga marufuku yalikuwa na nafasi ndogo ya mafanikio.

Makubaliano yaliyoridhiwa ilikuwa tu kubaki kimya katika swala hilo, hivyo ibara ya 3 cha Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu linasema "kila mmoja ana haki ya kuishi uhuru na usalama wa mtu".

ICCPR iliridhiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo 1966 na likaanza kutumika mnamo 23 Machi, 1976. Ibara ya 6 cha Mkataba kinaanza na maelezo kwa kusema kila binadamu ana haki ya kuishi. Halafu kinasema "Haki hii italindwa na sheria. Hakuna yeyote atakayenyimwa uhai wake kiholela".

ICCPR imeanzisha chombo cha ufuatiliaji, kamati ya haki za binadamu ambazo kinatoa mawazo ya jumla katika ufasiri wa mkataba, ikijumuisha haki ya maisha.

Kamati ya Haki za Binadamu imetamka "Uholela" usilinganishwe na "dhidi ya sheria" lakini lazima litafsiriwe kwa mapana zaidi, kujumuisha fikira/mawazo yasiofaa/dhuluma/udhalimu na ukosefu wa ubashiri.[22]

Aya ya 2 ya kifungu cha 6 kinatamka kwamba hukumu ya kifo ingeweza kutumika tu ka "makosa makubwa" hili sharti lilikuwa mara nyingi likipingwa wakati wa maandalizi ya rasmi ya mkataba na baadhi ya wajumbe walitoa hoja kwenye uorodheshaji wa makosa makubwa katika ufasiri wa masharti ya kifunbu cha 6. Kamati ya haki za binadamu ilisema/ilitamka kwamba usemi/neno "makosa makubwa" lazima lisomeke kuimarisha kwamba hukumu ya kifo lazima ilinganishwe na hatua maalumu.[23]

Walinzi wa Umoja wa Mataifa watoe ulinzi kwa wale wote wanaokabiliwa na adhabu ya kifo walioridhiwa na Baraza la Uchumi na Jamii mwaka 1984 na baadaye walipitishwa na Baraza Kuu na kutangaza kuwa mipaka ya neno "makosa makubwa zaidi" isingeenda zaidi/nje ya uhalifu wa kimataifa na kuwa na matokeo/matukio ya hatari sana.[24]

Kamati ikaongeza katika maoni yake ya jumla juu ya kifungu cha 6 kwamba "Pia inafuata kutoka kwenye maelezo ya kifungu cha 6 kwamba inaweza tu kuingizwa "kulingana na sheria zinazotumika kwa wakati ule wa ujumbe wa uhalifu na si kinyume na mkataba".

Hii ina maana kwamba kifungu 14 cha ICCR kinachohusu haki ya hukumu ya haki lazima iheshimiwe kikamilifu katika taratibu zozote zinazoelekea adhabu ya kifo, inayopelekea kuwa

[22] Van Alphen V. The Netherland (No 305/1988) UN Doc. A/45/40.Vol. II, p108.
[23] General Comment 6 (16), UN Doc, CCPR/C/21/Add, 1
[24] ESC Res, 1984/50j GA Res 39/118

kinyume cha sheria kwa juhudi yoyote ya kutekeleza hukumu isiyo halali kama; hali ambapo mtuhumiwa hana usimamizi wa wanasheria, kama mahakama siyo huru na isiyotenda haki, kama hakuna haki ya kukata rufaa au kuna ucheleweshaji usiokuwa na sababu. Kifungu hiki pia kilithibitishwa katika kinga za Umoja wa Mataifa (UN safeguards) ya 1984. Hukumu ya kifo ingetekelezwa tu kutokana na maamuzi ya mwisho yatolewayo na mahakama yenye uwezo baada ya mchakato ambao hutoa uwezekano wa ulinzi kuhakikisha hukumu ya haki angalau sawa na zile zilizopo katika kifungu cha 14 cha mkataba wa kimataifa wa ya haki ya kiraia na kisiasa, ikijumuisha haki ya yeyote anayetuhumiwa/anayeshatakiwa na uhalifu ambapo hukumu ya kifo kuhimizwa/kuwekwa kwa msaada wa kisheria katika hatua zote za uendeshaji.

Katika kesi ya *Reid dhidi ya Jamaika (Reid v Jamaica)* Kamati ya haki za binadamu ya nchi wanachama kuchunguza kwa makini wadhamini wote kwa hukumu halali/haki iliyowekwa katika kifungu 14 cha mkataba ni muhimu.[25]

Vyombo vya Umoja wa Mataifa vinavyotoa ulinzi kwa wale wote wanaokabiliwa na adhabu ya kifo, inategemea na tafsiri ya kamati juu ya uzuiaji wa uthibiti wa uhalifu na taarifa ya miaka mitano ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Kamati ya udhibiti wa makosa ya jinai imetoa mwongozo zaidi. Katika mwaka 1988, ilisema ya kuwa ulinzi ulitolewa katika ulinzi 5 inaweka wazi kwamba mashauri ya adhabu ya kifo lazima itume kiwango cha uthibitisho ambacho kinaenda zaidi ya ulinzi utolewao katika mashauri yasiyo ya hukumu ya kifo. Inashauriwa kwamba kungekuwa na umri wa mwisho wa utekelezaji wa hukumu ya kifo na pia kwamba wagonjwa wa akili kutokana na mtindio wa ubongo au wenye uwezo wa nchini sana wa akili "wasipewe kwenye adhabu ya kifo".

Mkataba wa nyongeza wa ICCPR iliridhiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1989 na ulianza kutumika mwaka 1991. Katika zile nchi ambazo zilirekebisha, mkataba ulitaka nchi wanachama kukomesha adhabu ya kifo, na kuzia utekelezaji wake, isipokuwa katika mazingira ya wakati wa vita. Hadi leo nchi 52 zimerekebisha hati 29 awali (protical) zikiwemo nchi sita za Afrika.[26]

Suala la hukumu ya kifo linabakia kuwa jambo/kitu cha kawaida katika ajenda ya Tume ya Umoja wa Mataifa ya haki za binadamu. Katika Azimio 2004/67[27] Tume ilitoa wito kwa nchi/mataifa yote ambayo bado yanaendeleza hukumu ya kifo kuendelea kuzuia/kupunguza idadi ya makosa ambayo yanaweza kupewa hukumu ya kifo, na angalau isiendeleze matumizi yake kwenye makosa ambayo kwa sasa hayatumiki kukomesha hukumu ya kifo kabisa na kwa wakati huo huo kuanzisha ukawizaji wa unyonyaji na kufanya taarifa ziwepo kwa uma juu ya kuwepo kwa adhabu ya kifo na ratiba

---

[25] Reid V. Jamaica, communication No. 355/1989 UN Doc. CCPR/C/51

[26] Mozambique (21 July 1993), Sey Chelles (15 Desemba 1994) Namibia (28 Novemba 1994), cape Vercle (19 May, (2000) Afrika Kusini (28 Augusti 2002) na Djbouti (5 Februari 2003) lazima ifahamike kwamba Saw Tomie na Principle (6 September 200) na Guinea Bisscau (12 Septemba 2000) ni signatories to the protocol wamesaini mkataba .

[27] Tume ya Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binadamu iliridhia Azimio 2004/67 juu ya suala la hukumu ya kifo tarehe 21 Aprili 2004 kwenye kikao cha Tume cha 60 nchini Geneva. Lilikuwa ni Azimio la nane kama hilio lililoridhiwa na Tume juu ya haki za binadamu tangu 1997, nchi 76, nchi moja zaidi kuliko mwaka uliotangulia/uliopita ulioidhamini Iraki, Kirbati, Samoa na visiwa vya Solomon vilidhamini azimio kwa mara ya kwanza kwa pamoja. Azimio liliridhiwa kwa rekodi ya kura za nchi 29 dhidi ya kura za nchi 18 na 10 hazikupiga kura. Bhutan na Gabon walipigia kura azimio kwa mara ya kwanza. Korea ya kusini ambayo ilipiga kura kupinga/dhidi ya azimio mwaka 2003 haikupiga kura mwaka 2004.

yoyote ya unyonyaji. Kama January 2005 kulikuwa na jumla ya nchi 118 zilizoacha kisheria au kimatendo adhabu ya kifo na 78 zilizozuia.[28]

## 2. **Mfumo wa Kanda: Mkataba wa Africa wa Haki za Binadamu na Haki za watu**.

### a. Mfumo wa sheria.

Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za watu ulikubaliwa mwaka 1981 na Umoja wa Afrika, hausemi juu ya adhabu ya kifo.

Hata hivyo, kama ilivyo kwa mikataba mingi ya Afrika Mkataba wa Afrika unatambua haki ya kuishi na ibara ya 4 inasema "Binadamu wana heshima." Kila binadamu atakuwa na haki ya kuheshimu kwa uhai wake na kuheshimiwa utu wake. Mtu awae yote yule asinyimwe haki hii kiholela.

Kulingana na uchambuzi wa William schabas[29], tafsiri ya ibara ya 4 ya Mkataba wa Afrika (African Charter) na marejeo yake "kwenye unyimaji holela wa maisha, anarudia ibara ya 6 ya na ya 1 ya mkataba wa kimataifa wa haki za raia na kisiasa na utumiaji holela ya adhabu ya kifo. Anaongeza kwamba ingekuwa busara kwamba ibara ya 4 ya mkataba wa Afrika ingefasiriwa kwa namna ile ambayo ingejumuisha taratibu kama zile zilizowekwa katika ulinzi wa umoja wa mataifa (UN safe guard) uhakikishao haki ya wale wanaokabiliwa na adhabu ya kifo[30].

Kwa nyongeza katika kikao chake cha kawaida Novemba 1999, Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki watu, iliridhia "Azimio ikizitaka nchi kufikiria ukomeshaji wa adhabu ya kifo". Azimio linaeleza wasiwasi wake kwamba baadhi ya nchi wanachama kwenye mkataba wa Afrika wameweka adhabu ya kifo bila kuheshimu haki kwenye hukumu halali iliyodhaniwa.

Aya za utendaji (operative) za Azimio zinasomeka kama ifuatavyo;

1. Inawataka vyama vyote vya nchi kwenye katiba ya Afrika juu ya haki za binadamu na Watu zile ambazo bado zinaendeleza adhabu ya kifo zikubaliane kikamilifu na masharti chini ya mkataba na kuhakikisha kwamba mtu aliyetuhumiwa kwa makosa ambayo hukumu ya kifo ndio hukumu inayofaa/wanapewa udhamini wote katika katiba ya Afrika.
2. Inatoa wito kwa nchi wanachama ambazo bado zinaendeleza adhabu ya kifo[31]. (a) Waweke kikomo cha uwekaji wa adhabu ya kifo kwa yale makosa makubwa tu. (b) Kufikiria kuanzisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa hukumu ya kifo. (c) Kuangalia juu ya uwezekano wa kukomesha/kuacha adhabu ya kifo.

Tume ya Afrika pia ilizitaka nchi wanachama kutuma waangalizi wa Umoja wa Mataifa katika nchi ambazo adhabu ya kifo hazijakomeshwa[32].

---

[28] Ona http://web.amnesty.org/pages/deathpenalty-countries-eng

[29] Schabas William. The abolition of death enalty in International Law (Cambridge press, London 2002).

[30] Azimio la ESC 1984/50 lililopitishwa kama azimio la mkutano mkuu 29/118 [ESC Resolution 1984/50 subsequently endorsed as Genral Assembly Resolution 39/1181].

[31] Azimio lililozitaka lililonasihi nchi kuangalia ucheleweshaji wa hukumu ya kunyongwa, Ripoti/taarifa ya 13 ya Tume ya Afrika juu ya haki za Binadamu na watu. {Activity Report of the African Commission of Human and People's Rights} OUA. DOC: Attal Dec. 153 (xxxvi) Annex iv.

[32] Angalia Azimio la Ouagadougou na mpnago juu ya kuharakisha, mageuzi ya magereza na adhabu katika Afrika Septemba 2002. {See the Ouagadougou Declaration and Plan fo Action an acceleration prisons and penal reform in Africa Septemba 2002.

Vyombo vya ufuatiliaji utekelezaji masharti ya mkataba wa Afrika ni Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu. Wananchi wanachama kwenye mkataba huo wanatakiwa kuwasilisha ripoti za vipindi kwa tume ingawa utekelezaji wake si wakawaida na taarifa zinazowasilishwa ukweli zimelenga suala la adhabu ya kifo[33].

Kwa bahati mbaya utaratibu wa ombi la mtu mmoja mmoja utolewao na katiba sio wenye nguvu kama vile mtu angetaka uwe[34]. Hata hivyo mashauri mengi yamekua yakilenga masuala yanayohusiana na adhabu ya kifo. Moja kati ya haya mashauri yanahusu mauaji ya mtetezi wa haki Ken Saro-wiwa Nigeria Novemba 1995.

Kulingana na Kifungu cha 4 cha mkataba, Tume iliangalia kwa makini: "Kwamba hukumu ambayo inaamuru adhabu ya kifo yenyewe inakiuka kifungu cha 7, baadaye utekelezaji wowote wa hukumu inapelekea unyimwaji wa maisha kiholela na inakiuka kifungu cha 4 …… Ulinzi wa haki ya kuishi katika kifungu cha 14 pia kinajumuisha wajibu kwa nchi kutoruhusu kwa makusudi mtu afe wakati akiwa mahabusu. Hapa angalau maisha ya mmoja wa wahanga yalikuwa katika hatari kubwa kwa kukosa matibabu wakati akiwa kizuizini. Hivyo kuna ukiukaji wa kila aina ya kifungu cha 4". Tume iliamua kwamba kulikuwa na ukikwaji wa vifungu vya 4 na 7 "Katika uhusiano kwenye mashauri ya adhabu ya kifo kwa wahanga"[35].

Katika mkataba wa nyongeza wa mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu katika uanzishaji wa mahakama ya Afrika juu ya haki za binadamu na watu iliyoridhiwa Ouagadougou, Bukina Faso tarehe 9 Julai 1998 ilianza kutumika tarehe 25 Januari 2004 mwezi mmoja baada ya marekebisho kwa nchi ya 15 Komoro tarehe 26 desemba 2003. Matarajio kuhusu mamlaka ya mfumo wa haki za binadamu ni mkubwa. Mkataba wa nyongeza unaruhusu watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuweza kufikia mahakama, sio moja kwa moja kupitia Tume ya Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu au moja kwa moja kama nchi husika inakubali rekebisho kama hilo kwa kufanya mkataba chini ya ibara ya 34 aya 6 ya mkataba wa nyongeza.

Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto ambao ulipitishwa 1990 lakini ulianza kutumika mnamo tarehe 29 Novemba 1999, umetamka kuwa "adhabu ya kifo haipitishwi kwa makosa yanayofanywa na watoto" (kifungu cha 5 aya 3).

---

[33] Katika taarifa yake kipindi cha tarehe 1993, juu/ihusuyo ukomeshaji wa adhabu ya kifo kwa usafirishaji wa dawa za kulevya ushughulikiaji wa mazao ya mafuta ya petroli kinyume cha sheria na kughushi/kutengeneza fedha za bandia na kubadilisha kifungo cha maisha. Nchi nyingine hazifanyi rejea zozote katika hukumu za kifo kwenye taarifa zao. Nigeria, in its periodic report elated 1993 refered to the abolition of the death penalty for drug trafficking un-lawful dealing in petroleum products and counterfeiting of currency and its replacement with life impresinment. Other states make no reference at all to the death penaltly in their repots.

[34] Ucheleweshaji unuwai kwa uchunguzi wa mawasiliano mara nyingi ni mrefu toka miaka miwili hadi minane. Makamishna mara nyingi hupenda makazi ya amani kwa gharama ya ufanisi. Mbali ya uharaka/umuhimu wa mashauri yaliyoletwa kwako. Ucheleweshaji pia hurefusha/huongezewa muda unaopita kati ya upokeaji wa mawasiliano na uamuzi juu ya kukublika, ukusanyaji wa mawasiliano yanayohusiana na nchi yenyewe, mawasiliano, utaratibu usio sahihi, vikao visivyofupishwa kwa ukosefu wa vyanzo vya pesa, ucheleweshaji katika utekelezaji wa taarifa za ujumbe na uhitimishaji wa taarifa na ukosefu wa watumishi katika Secretariat ya Tume. Kama maamuzi ya tume katika mawasiliano yanayovutia na ya maendeleo kulingana na ulinzi wa haki za binadamu, hawana athari yoyote kwa sababu kwa kawaida haikutekelezwa na nchi husika. Kwa undani zaidi, angalia muongozo juu ya mahakama ya Afrika juu ya haki za binadamu na watu , funguo 10 za kuelewa na kutumia Mahakama ya Afrika juu ya haki za binadamu na watu Novemba 2004 (www.fidh.org See FIDH Guide on the Africa Court on Huma and People's Rights: 10 keys to understand and used the African Court on Human peoples Rights, November, 2004. (www.fidh.org )

[35] International pen, constitution rights project, Intergights on behalf of Ken Saronuiwa Jr. and civil liberities organization v. Nigeria (Comm. No. 137/94, 139/94, 154/96 and 16/97), Tulelth Activity report of the African Common on Human and People's Rights. (1998 – 1999) Paragraph 103 -104.

Kifungu cha 2 kinafafanua mtoto kama "Kila binadamu chini ya umri wa miaka 18". Kifungu cha 17 kinatamka kwamba watoto hawapaswi kuwekwa kwenye matendo yasiyo ya kibinadamu au udhalilishaji, na kwamba msingi wa mfumo wa haki za mhalifu ni uendelezaji wa urudishaji tena kwenye familia na urekebishaji.

Kamati ya Wataalam ya Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto imepewa kazi ya kufuatilia utekelezaji wa sheria (Kifungu cha 32 na kuendelea).

Mkataba unaruhusu kamati ya wataalamu kupokea mawasiliano haya yanaweza kupelekwa na mtu yeyote, kundi, au Shirika lisilo la Kiserikali linalotambulika na OAU/AU, Nchi mwanachama au Umoja wa Mafaifa.[36]

Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki Watu, katika kikao chake cha kawaida cha [mwezi] Mei 2003, pia kilipitisha muongozo wa Hukumu za Haki na Msaada wa Sheria katika Afrika[37], ikiona kwamba kila jitihada ifanywe ili zijulikane pote katika Afrika na kutoa wito kwa nchi kuziheshimu na kuzijumuisha katika utungaji wa sheria za nchi zao. Miongozo hiyo pia lazima ihusishe kesi za adhabu ya kifo.

## b. Utendaji wa nchi Jirani

Mwaka 1990 Cape Verde ilikua ni nchi pekee ya kiafrika ambayo haikuweka adhabu ya kifo katika sheria zake. Katika mwaka 1995 mahakama ya katiba ya Afrika ya Kusini ilitamka kuwa adhabu ya kifo ni kinyume cha katiba ya mpito ya nchi hiyo.[38]

Nchini Malawi, ingawa adhabu ya kifo imo katika vitabu vya sheria, adhabu hiyo haija tekelezwa tangu mwaka 1992 na Rais Muluzi alifanya maamuzi yake pekee kutotia saini amri ya adhabu ya kifo akiwa ofisini. Alibadilisha adhabu za vifo mara nyingi. Kwa mfano mnamo tarehe 9 April 2004 alibadilisha huhumu 79 za adhabu za vifo.

Rais Mwanawasa wa Zambia alifanya maamuzi kama hayo kwa kutotia saini amri za hukumu za vifo na mwezi Februari 2004 alibadili hukumu za vifo vya askari 44 ambao waliohukumiwa kifo kutokana na kuhusika kwao katika mapinduzi yaliyoshindwa ya 1997 na alitangazia umma kuwa hakutakuwa na utekelezaji wa adhabu ya kifo wakati wa urais wake. Alisema, "kwa muda wote nitakao kuwa Rais, sitatakeleza adhabu ya kifo.[39]

Hakuna utekelezaji wa adhabu ya kifo uliofanyika nchini Kenya tangu katikati ya miaka ya 1980 na Februari 2003, Rais Kibaki alibadili hukumu za vifo 195. Tanganzo lilikuja mara baada ya waziri wa

---

36 Kifungu 44 cha Mkataba wa Afrika cha Haki na Ustawi wa Mtoto 1990

37 Kikao cha 33 cha kawaida cha Tume ya Afrika juu ya haki za binadamu na watu kilichofanyika Niamey Niger toka tarehe 15 hadi 29 Mei 2003 Angalia Taarifa za shughuli za mwaka ya Tume juu ya haki za Binadamu na watu XVI ukurasa 14 -15. 33rd ordinary, session African commission an human and peoples" rights, held in Niamey Niger from 15th to 29 of may 2003 see XVth Annual Activity Report of the African commission an Human and peoples" Right pages 14-15.

38 Afrika ya kusini dhidi ya Makwanyane 1995 (3) SA 391. {South Africa V. Makwanyane 1995 (3) SA 391}

39 Shirika la Kimataifa linalotetea haki za wafungwa SA Kanada Taarifa za Adhabu ya kifo June 2004 inapatikana http:// www amnesty. Ca /resource centrel reports/ view . php? Load = arc view x article = 1707x C= Resource + centre + Report.

(Amnesty international Canada Death penalty news, June 2004 accessed at http://www.amnesty.org Cal resource centre/ reports/ view. Php load= arc view x article =1707 x C= Resource + centre + Report.

Mambo ya Ndani na Urithi wa Taifa, Moudy Awoori, alipotembelea magereza kadhaa na kutoa hadharani masikitiko yake kuhusiana na hali ya vizuizini".

Kamishna wa magereza. Abraham Kamakili, alisifia tukio hili la kihistoria lisilo na mfano, akisema kwamba adhabu ya kifo ingefutwa kwa sababu inagharimu maisha yasiyo na hatia. Katika gazeti la Nation alisema "Tuna hamu kuona siku ambayo Bunge letu litafutilia mbali adhabu ya kifo kutoka katika katiba yetu.

Waziri wa Sheria, Kiraitu Murungi, pia aliunga mkono hatua ya kutaka kubatilisha adhabu ya kifo na alifanya ushawishi kwa hilo kama mbunge katika majaribio mawili yaliyotangulia katika mwaka 1994 na 2000 kujaribu kukomesha adhabu ya kifo, ambayo yalikataliwa na serikali iliyopita. Hatia za mauaji na wizi wa kutumia silaha zinabeba hukumu ya adhabu ya kifo nchini Kenya ambayo ilitekelezwa kwa mara ya mwisho mwaka 1987.

## III. Ushabihiano wa Utawala wa Sheria: Haki katika Utata

Wakati wa ziara ya ujumbe wa FIDH nchini Tanzania, ulibaini mambo mabaya katika mfumo wa Sheria Tanzania, ambao unaelekea kuwa tishio kwenye utawala wa Sheria na kikwazo kwenye mageuzi. Msisitizo wa marekebisho kutoka ujumbe wa FIDH ulikuwa hasa katika matatizo makuu mawili:

1. Kutokuwa tayari kwa serikali kupingwa kwenye maamuzi yake katika uendeshaji wa mahakama; na
2. Ukweli kwamba mfumo wa haki katika jinai kimsingi ni wa ulipizaji kisasi kwa wahalifu.

FIDH inashawishika kuona masuala haya mawili lazima yashughulikiwe na ufumbuzi upatikane ili kuyatatua. Uwezekano wa kupinga maamuzi ya serikali katika uendeshaji mahakama na kuleta mfumo wa adhabu uliojengwa juu ya imani kwamba wahalifu wanaweza kuelimishwa, kurekebishwa na kujiunga tena na jamii ni mambo muhimu katika kujenga jamii yenye amani na utawala wa sheria.
Pia kuwepo kwa rushwa ambayo kama haitakabiliwa kwa dhati huleta tishio kubwa kwenye utawala wa sheria.

### 1. Mfalme na Serikali hawafanyi kosa

Kama ilivyojadiliwa hapo juu baada ya uhuru, Bunge liliamua kupitisha katiba bila ya vifungu vya haki za binadamu, hadi baada ya miaka ishirini na tatu ndipo vifungu hivyo vilipojumuishwa katika katiba ambapo bado vilifungwa na vikwazo vya muda katika matumizi yake na vipingamizi kadaa (angalia hapo juu).

Mwanzo wa kutoamini mahakama na majukumu yake katika kusimamia matumizi ya nguvu za serikali upo hadi leo. Imetolewa mifano katika ngazi ya kimataifa kwa kusita kuridhia mikataba ya haki za binadamu ikiwemo utaratibu wa usimamizi wa mikataba katika kiwango cha ndani, kwa kutoihusisha mahakama na udhibiti mkubwa juu ya uendeshaji wa mahakama wenye kupinga serikali.

**a. Kusita kuridhia mikataba inayotoa usimamizi wa haki.**

Kwanza, ingawa serikali ya Tanzania imeridhia mikataba kadhaa ya haki za binadamu na bado inasita kuridhia mikataba mingine inayoruhusu ukataji wa rufaa na upelekaji wa malalamiko wa mtu mmoja mmoja. Kama ilivyo mambo haya hayakuridhiwa labda kwa sababu maalum.

- Kwenye Mkataba wa nyongeza kimataifa juu ya Haki za Kiraia na Kisiasa ambao huruhusu mtu mmoja mmoja kupeleka malalamiko yake kwenye kamati ya umoja wa Mataifa ya haki za binadamu.
- Mkataba wa nyongeza wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake ambao huruhusu mtu mmoja mmoja au kikundi kuwasilisha malalamiko kwenye kamati ya uondoaji wa ubaguzi dhidi ya wanawake.
- Mkataba wa makubaliano dhidi ya mateso na ukatili mwingine wa kinyama au matendo ya kushusha hadhi huruhusu wahanga kuwasilisha mawasiliano kwenye kamati dhidi ya mateso kama serikali inayoshitakiwa kuwa imefanya ukiukaji imekubali mamlaka na maamuzi ya kamati (kifungu 22).
- Mkataba wa nyongeza wa hati za awali kwenye mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu juu ya uundaji wa mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ambao utaruhusu watu binafsi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kupata fursa ya kwenye mahakama sio moja kwa moja ila kupitia Tume ya Afrika juu ya haki za binadamu na watu au moja kwa moja kama tu nchi husika imekubali marekebisho kama hayo kwa kufanya azimio chini ya kifungu cha 34 cha mkataba.

Kwa nyongeza, serikali inaonekana kudharau uchunguzi uliofanywa na mwandishi maalum wa Umoja wa Mataifa juu ya haki za binadamu. Kwa mfano, kwa barua ya tarehe 8 – Octoba 2003 Mwandishi maalum juu ya mateso na ukatili mwingine, unyama au matendo ya kushusha hadhi au adhabu iliikumbusha serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania idadi ya mashauri yaliyoletwa mwaka 2001 na 2000 ambapo hakukuwa na jibu lililopatikana. Kwa nyongeza serikali ya Tanzania bado hajakutoa msimamo wake kwenye taratibu maalum za umoja wa mataifa.

Ushirikiano na vyombo vya usimamizi vya Umoja wa Mataifa, hauridhizi, na kwamba taarifa zipatazo 15 bado hazijawasilishwa. Kati ya hizo kuna taarifa ya mwanzo chini ya ICESCR (Toka 1990), hali kadhalika taarifa za vipindi chini ya ICCPR (Toka 2002), CEDAW (Toka 1998) na CERD (Toka 1987). Mtazamo huu unaonesha serikali inaepuka uchunguzi ama kutoka kwa raia wake, watu wa idara ya mahakama au vyombo vya ufuatiliaji wa haki za binadamu vya kimataifa.

FIDH inafikiria kwamba uhusiano kama huo wa utaratibu wa kiutendaji ni muhimu sana, kwa vile unafungua majadiliano yanayojenga kati ya serikali na vyombo vya usimamizi vya Umoja wa Mataifa ambavyo vina matokeo mazuri katika utekelezaji wa utawala wa sheria na heshima kwa haki za binadamu.

Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria,jaji Bahati na Mkurugenzi wa mambo ya Katiba na Haki za Binadamu, Wizara ya Sheria na mambo ya Katiba Bwana Werema aliwaambia wajumbe wa FIDH kwamba Tanzania inatafakari kuongeza ufungamano wake na makubaliano ya kimataifa ya haki za binadamu na kuridhia zaidi mikataba ya kimataifa vya haki za binadamu. FIDH inaamini kuwa dhana hii itafanyiwa kazi na serikali.

### b. Kutokuwa na Imani na Idara ya Mahakama

Katika matukio kadhaa, Rais aliyepita Mwl. Nyerere alieleza wasiwasi wake kuwa mahakimu walikuwa wanahusika kushughulikia hukumu zinazohusu matendo ya uhalifu au hali ya kutokuwepo na utulivu kwa raia. Kipindi kilichopita Tanzania ilikumbana na wimbi la uhalifu kama vile wizi wa ng'ombe (ambao ulipelekea vikundi vya sungusungu), wizi wa mali za umma au matendo ya wale waliojulikana kama walanguzi na wahujumu uchumi ambao ulipelekea kuwepo uanzishaji wa vifungu vinavyo kiuka haki (ouster clauses) na mabaraza ya kiutawala.

Mwaka 1983 Rais aliyestaafu alitamka kwamba "Nawataka mahakimu kutusamehe kama tunasita kuwapeleka wahalifu katika mahakama ya sheria. Kuna wakati walanguzi walikuwa wakipelekwa kwenye mahakama ambapo walikuwa wakipewa hukumu nyepesi au walikuwa wakiachiwa huru. Katika mahakama matepeli/walanguzi waliweza kutumia pesa zao walizopata visivyo halali kuweka mawakili au kutumia pesa zao kupindisha sheria ili ziwapendelee".

Matokeo yake serikali ilibuni vyombo mbadala ili kuepuka udhibiti wowote wa kimahakama wa shughuli na maamuzi ya serikali.

Mbinu mbili zimeridhiwa: (1) Kwa kuiondia mahakama katika kushughulikia mashauri yanayochukuliwa kama ni ya muhimu sana na nyeti kisiasa. (2) Kwa kuepuka marejeo ya kimahakama kwa kuweko vizuizi vikali katika mwenendo wa upingaji wa matendo ya serikali.

**Kusahaulika na kuwekwa pembeni kwa mahakama kumesababishwa na yafuatayo:**

- Matumizi ya vifungu vinavyominya haki katika sheria.
  Hivi ni vifungu vya sheria ambavyo ni vinavyozuia kupata nafuu nyingine kwenye mahakama za sheria ukiacha matumizi kwa ridhaa: Marekebisho kwenye mahakama za sheria.[40] Wanafanya utawala kuwa kinga kwenye mapitio ya hukumu. Tendo kama hilo limekuwa likipingwa kwa kauli moja na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu.[41]
- Uanzishaji wa vikundi vya ulinzi kufanya doria mitaani na kupambana na uhalifu (mfano mmojawapo maarufu ni Sungusungu) ambao hudhaniwa unakaribia maisha halisi.[42]
- Sheria ya hukumu ya chini: Serikali inaweka kiwango cha juu cha chini katika hukumu ili kupunguza matumizi ya uhuru wa mahakama na kuhakikisha kwamba hukumu nzito zinatekelezwa.
- Uidhinishwaji wa sheria zilizopitwa na wakati kugeuza maamuzi ya mahakama. Mwenendo huu unapingwa na watumiaji wa sheria/wanasheria kadhaa walioonana na ujumbe wa FIDH. Kama wanavyosema "unapopingana na serikali ya Tanzania unaweza ukashinda kwa upande mmoja lakini watatumia upande mwingine kukushinda". Chris Maina Peter alitoa mfano wa sheria ya

---

[40] Kwa mfano sheria ya kizuizini ya 1962 inasema "Hakuna amri inayotolewa chini ya sheria hii itahojiwa katika mahakama yoyote ingawa inamruhusu Rais kumuweka mtu yoyote kizuizini maish aiwapo anaelekea kuwa ni hatari kwa amani na utulivu au mtu yeyote ambaye mwenye tabia yenye hatari kwa ulinzi … au usalama wa nchi. Sheria hii ilirekebishwa mwaka 1985 kuruhusu Mahakama Kuu kuchunguza maamuzi.

[41] Angalia constitution Rights and civil liberties organization v. Nigeria com. 143/95, 150/96, "katika mashauri yote haya hapo juu, Tume imegundua kwamba vifungu viivyoachwa (outer clauses). Vinafanya marekebisho yaliyozoweleka yasiwepo hayana nguvu au yasiyo halali. Inaanzisha hali ya sheria ambamo mahakama inaweza kufanya kusiwepo na ukaguzi kwenye mafaili ya uendeshaji wa serikali. Vifungu viivyoachwa vinaukiukwaji wa kifungu 7. Tume lazima ichukue nafasi hii sio tu kurudia thibitisho/hitimisho kwa lililokwishafikiwa na kuomba katiba na taratiubu za mahakama maalum zinakiuka kifungu 7(1)(a) na (c) na 20, lakini hupendekeza juu ya kumaliza mazoea ya kuondoa maeneo yote ya sheria kutoka kwenye mahakama ya kisheria ya mahakama ya kawaida.

[42] Rais Nyerere aliripotiwa kusema kwamba Sungusungu wako katika nafasi nzuri kuliko polisi na mahakama kujua ni akina nani walikuwa wezi na matapeli. Angalia Sunday News 25th May, 1986.

ufukuzaji nchini ya mwaka 1921 ambayo imetamkwa na Mahakama Kuu kuwa si ya kikatiba na batili. Kama alivyosema "ianachekesha kuona serikali imepeleka mswada Bungeni ukiwa na madhumuni ya kurekebisha sheria ambayo imetamkwa batili".[43] Jaji Mwalusanya alikiita hiki kitendo cha serikali ni zoezi lisilokuwa na manufaa kwa vile kwa akili za kawaida huwezi kurekebisha sheria ambazo hazipo (kwa sababu zilishatamkwa na Mahakama Kuu kwamba si za kikatiba).

– Matumizi ya vitisho dhidi ya watendaji wa mahakama. Ulidhihirishwa kwa wajumbe wa FIDH kwamba Jaji Mwalusanya ambaye maamuzi yake yananukuliwa katika taarifa hii alilazimika kujiuzulu kutokana na vitisho. Kama matukio kama haya yanaweza kutokea kwa Jaji wa Mahakama Kuu anayeheshimika tunaweza kueleza hofu kwamba watumishi wa mahakama katika ngazi za chini wanakumbwa na hali kama hiyo. Hii pia inatoa tahadhari zaidi kwa mahakimu wanaotoa maamuzi ya muhimu, hasa miongoni mwa wafanyakazi na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

**Uthibiti mahsusi wa taratibu za kupinga mwenendo wa serikali:**

– Matumizi ya vifungu vinavyominya haki Iliyojumuishwa katika mkataba wa haki za binadamu "kwa mujibu wa sheria". Matumizi hayo yanaruhusu serikali kutunga au kuendeleza matumizi ya vifungu ambavyo vinapinga haki za binadamu.
– Ruhusa yakuishitaki serikali kulingana na sheria ya mwaka 1967.
  Kulingana na sheria hii mtu akitaka kuishitaki serikali alikuwa kwanza anatakiwa kuomba ruhusa serikalini yenyewe kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali. Hili lilipelekea dhuluma nyingi kama ilivyoonyeshwa kwenye kesi ya Scarion Bruno. Aliyepigwa na mhojiaji wakati akiwa chini ya ulinzi wa askari wa usalama alifungwa mwaka mmoja bila ya kupewa fursa ya dhamana na alinyimwa huduma ya matibabu. Miaka mitatu baadaye aliomba kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuishitaki idara ya mahakama na afisa wa polisi ambaye aliyemuumiza kwa madhara. Alikufa miaka mitatu baadaye akiwa bado anangoja jibu kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ingawa sheria hiyo imefanyiwa marekebisho hivi karibuni inabaki ni kikwazo halisi juu ya upatikanaji. Marejeo ya maamuzi ya serikali chini ya sheria (iliyorekebishwa) namba 30 ya mwaka 1994 (Sheria Namba 30 ya 1994) kifungu cha 2 aya ya 2 mkataji rufaa lazima aseme nia ya kufanya hivyo siku 90 kabla ya kutoa ombi la lalamiko lake[44].

- Utekelezaji wa sheria ya Haki za msingi za Kikatiba na Wajibu ya mwaka 1994, inajieleza kwa kusema "mahakama kuu badala ya kutamka sheria au tendo kuwa batili au si la kikatiba ina uwezo na uamuzi katika shauri lifaalo kuruhusu Bunge au mamlaka nyingine zinazohusika vyovyote itakavyokuwa kusahihisha upungufu wowote katika sheria zenye mashaka au matendo katika kipindi maalumu, kulingana na hiyo hali kama itakavyobainishwa, sheria au tendo hilo litahesabiwa kuwa sahihi hadi sahihisho lifanywe au kumalizika kwa muda uliowekwa na Mahakama Kuu.

## 2. Mfumo wa jinai uliojegwa katika ulipizaji wa kisasi.

Nchini Tazama kuna imani ya jumla kwamba uhalifu ni kosa la mhalifu bila kujali na hakuna kujali mali ya mazingira ya kijamii.[45] Badala ya kujaribu kuelimisha na kurekebisha wakosaji, njia

---

[43] Angalia Chris Maina Peter: Human Rights in Tanzania, uk. 743- 745

[44] Hakuna shitaka dhidi ya serikali litakalopokelewa na kusikilizwa isipokuwa tu mlalalmikaji alishawahi hapo nyuma kulipeleka kwa Waziri wa Serikali Idara au afisa anayehusika na taarifa isiyopungua siku tisini ya nia yake ya kushitaki serikali. Akieleza bayana msingi wa lalamiko lake dhidi ya serikali na atatuma nakala kwa mwanasheria mkuu wa serikali.

[45] Kwa mfano katika mwaka 1969 maelezo ya kiserikali yaliyotlewa juu ya ongezeko la kiwango cha uhalifu sababu kuu tano. Kwanza baadhi ya watu wamezuliwa uhalifu, pili muungano tofauti, tatu malezi mabaya, nne anemia na tano uvivu (Hansard session, October, in the Penal System: Retibution or correction fo offender Prof. Leonard P. Shaidi). Ingawa hii ni msimamo tena wa serikali utendaji unaonesha kwamba mawazo kama hayo bado yanavutia.

iliyowekwa ni kwamba adhabu matumizi ya nguvu dhidi ya wahalifu na unyanyapaa wa tabia za wahalifu bila ya kujali mazingira ya kijamii ambamo unaishi[46] Hukumu lazima ipitishwe na kila mmoja lazima ajue juu ya hilo.

Hili linatolewa mfano katika nyanja mbili: Kutoa adhabu ziwekazo alama kwenye mwili wa mhalifu na kutoa mamlaka ya adhabu kali uridhiaji wa hukumu kali za vifungo.

**Adhabu ya viboko na Adhabu ya kifo**

Adhabu zote za viboko na kifo zimeanzishwa na utawala wa kikoloni. Adhabu hizo zinaendelezwa hadi leo. Ingawa sio lengo la moja kwa moja la taarifa hii suala la adhabu ya viboko ni muhimu kuelewa kwa jinsi gani linavyochukuliwa Tanzania.

Kutokana na kiwango cha uhalifu katika nchi na kutokuwa na uhakika na mahakama serikali, ikaamua kutunga sheria inayoweka kiwango cha kati cha kifungo.

Serikali ilianza na uridhiaji wa sheria ya mwaka 1963. Serikali ilihalalisha sheria kutokana na ongezeko la wizi katika ofisi za serikali, wizi wa mifugo, uvunjaji wa nyumba, wizi wa nyumbani, unyang'anyi wa kutumia nguvu na rushwa. Ilikuwa ni wazo la serikali kwamba mahakama zilikuwa na huruma katika hukumu zao, mara nyingi hutoa hukumu chini ya kiwango kikubwa kilichowekwa kwenye sheria.

Sera za mwanzoni za serikali zilikuwa kali sana: Hukumu ya chini sana ya kifungo cha miaka miwili na viboko ishirini na nne kila mwaka. Adhabu ya viboko ilikuwa ikitekelezwa kwa awamu ya viboko sita kila miezi mitatu. Kulingana na Waziri wa Mambo ya Ndani kwa wakati huo hata kama mtu akifungwa kwa miaka kumi atachapwa viboko sita kila miezi mitatu kwa kipindi chote.[47]

Kwa ushirikiano kutoka kwa wabunge [48], muswada wa adhabu ya viboko uliridhiwa na kupitishwa kuwa viboko ishirini na nne. Adhabu hii itekelezwe kwenye awamu mbili zilizo sawa, awamu ya kwanza mwanzoni mwa kifungo na ya pili siku ya mwisho ya kifungo.

Na wakati huo huo, Waziri wa mambo ya Ndani alitangaza hali ya gerezani iwe mbaya zaidi, kwa mfano alisema wafungwa wasingekuwa na matandiko tena na idadi ya mablanketi na mashuka ipungue na badala yake wangepewa mkeka mmoja na blanketi moja na wangelala sakafuni.

Utekelezaji wa adhabu ya viboko uliongezeka haraka katika miaka iliyofuata: wakati ambapo ni kesi 13 tu za adhabu ya viboko zilitekelezwa katika mwaka 1958, ziliongezeka mpaka 1,508 mwaka 1963 na 3,511 mwaka 1965, ambapo baada ya hapo hesabu za serikali hazikuweza kuoneshwa tena kwa umma.

---

[46] Jaji Mwalukasa alieleza waziwazi serikali haifichwi ukweli kwamba karibu watu wote masikini huuawa wakati wa wizi wa kutumaji nguvu kwa sababu ya hali duni ya maisha na ugawaji usiokuwa sawa na mkakati wa taifa. Hali ya umaskini na njaa unapelekea uhatali kwa sababu uchumi umesimamiwa vibaya na serikali. Baada ya nchi/sekta kufichua kwamba masikini hufa kwa sababu ya umasikini. Inasemekana kwamba muuaji hana uadilifu/ameondolewa uadilifu.

[47] Hansard, 6th Session, April 1963.

[48] Baadhi pia hutoa wazo uchapaji wa viboko ungefanywa hadharani wengine wasingekutwa mikono. Badhi pia walipinga masharti yaliyomo kwenye sheria ambayo yaliyowatoa wanawake, watoto na wazee kwenye adhabu ya viboko. Kauli pekee kinyume ilitoka kwa wabunge wawili wanawake waliosema. Taifa linalojiheshimu lisingeona fahari sheria ya hali hii.

Utafiti uliofanywa mwaka 1967 ulionesha kwamba mahakama ilikuwa ikisita sana kuyatumia masharti haya makali. Utafiti huo ulifichua kwamba mahakama imeona sheria hii kuwa si nzuri na kuamua kuzuia matumizi yake pale inapowezekana.[49]

Hata hivyo, serikali iliamini kuwa sera hii ilikuwa sahihi, kama ilivyoelezwa na Waziri Mkuu wa wakati huo. “Lazima tuwafanye watu kutambua kwamba kufanya kosa dhidi ya taifa au raia yeyote yule ni kitu kiovu ambacho ni aibu na fedheha kwa mtu akifanyaye. Iwapo mtazamo huu utaridhiwa kiujumla, tutaweza kufikiria upya mbinu za kushughulikia wahalifu lakini hadi hapo tutakuwa hatuna huruma wala msamaha. [50].

Profesa Shaidi alieleza wasi wasi wake kwa wajumbe wa FIDH kwamba adhabu ya viboko bado inatumika Tanzania, ingawa hakuna takwimu za kiserikali zinazooneshwa kwa umma. Hata hivyo Bwana Rweyongeza, wakili wa utetezi, aliuambia ujumbe wa FIDHI kwamba adhabu hiyo hutekelezwa mara chache.

Sheria ya adhabu ya viboko ya 1970 hvi karibuni ilirekebishwa mwaka 1998 na uridhiwaji wa sheria ya makosa ya kujamiiana (kama ilivyobainishwa bayana) sheria ya mwaka 1998. Sheria hii mpya inarekebisha adhabu iliyotangulia ya ubakaji ambayo iliweka *“hukumu ya kifungo cha maisha na viboko au bila ya viboko”.* Kifungu kipya cha 131 cha cha kanuni za adhabu kinatamka *“kifungo cha maisha na katika hali yoyote ile kifungo sio cha chini ya miaka 30 na viboko na faini na kwa nyongeza utaamriwa kulipa fidia ya gharama itakayoamriwa na mahakama kwa mtu kulingana na aliyefanyiwa kosa na madhara yaliyosababishwa kwa mtu huyo”.* Matumizi ya adhabu ya viboko imetokea kuwa ni lazima kwa kesi za ubakaji.

Orodha ya majedwali mipango ni tatu (I, II, na III) zilizounganisha kwenye sheria ya adhabu ya viboko ya 1970 imeorodhesha makosa mengi ambayo yanastahili adhabu ya viboko kwa watu wazima chini ya sheria.

FIDHI inarudia tena kusema kwamba adhabu ya viboko hakika inakiuka viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Inapingana na ibara ya 1 ya mkataba wa Kimataifa dhidi ya Ukatili, na ibara ya 7 ya mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa, tamko la kulinda watu wote dhidi ya ukatili na mateso. Maandishi maalumu ya Umoja wa Mataifa juu ya mateso inafikiria kwamba adhabu ya viboko haiendani na uzuiaji wa mateso na ukatili mwingine wa kinyama au matendo ya udhalilishaji au adhabu iliyoainishwa pamoja na mambo mengine katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Azimio la Kimataifa la Kinga ya watu wote kutokana na mateso ya ukatili mwingine wa kinyama au matendo ya kudhalilisha[51]. Katika mapendekezo yake ya ujumla mwandishi maalumu alisema “Sheria itoayo adhabu ya viboko inajumuisha utoaji wa adhabu za kupindukia lazima ikomeshwe.[52]

Kwa nyongeza kamati ya Umoja wa Mataifa ya haki za binadamu imethibitishwa kwa uchechefu kwa nyakati mbili ambazo ukatazaji juu ya mateso na ukatili, unyama au matendo ya udhalilishaji au

---

[49] Stephan Huber Statutory Interpretation and Judicial Discrtion (1967)2. Deming Law Journal 99

[50] Acted in James Read. Minimum Sentence in Tanzania (1965) Journal of African Law 22 - 23

[51] Report of the special Rapporteur New, Nigels Rodley submitted pursuant to commission on Human Rights Resolution 1995/37, E/CN 4/1997/7 (Djaweai) 1997

[52] General Recommendations of the UN special Rapporter or Torture, paragraphic set http/www.ohchr.org/english/issue/torfere/rapporteur/index.htm

adhabu iliyopo katika kifungu 7 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Raia na kisiasa zilizoendeleza kwenye adhabu ya viboko.[53]

Kwa nyongeza, ibara ya 5 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu inakataza mateso na ukatili mwingine wa kinyama au matendo ya udhalilishaji.[54] Na Tume ya Afrika juu ya haki za binadamu na watu imesema waziwazi kwamba "Hakuna haki kwa mtu mmoja mmoja na hasa serikali ya nchi kutumia nguvu kwa watu kwa makosa, haki kama hiyo ni sawa na kuidhinisha makosa ndani ya mkataba na ni kinyume na hali ya mkataba huu wa haki". Na kwa hiyo waliiomba serikali ya Sadan kurekebisha sheria yake ya makosa ya jinai ya 1991 haraka ili iendane na wajibu wake ndani ya Mkataba wa Afrika na mikataba mingine ya kimataifa na kukomesha adhabu ya viboko bila ya kujali kosa husika[55].

Hali kadhalika, mambo kama hayo pia yameonekana si ya kikatiba katika nchi nyingine kama vile Zimbabwe, ambapo mahakama Kuu iliona kwamba "namna ambavyo inatekelezwa ni kama ilivyokuwa enzi za ukoloni kulipokua na vituo vya kuchapia. Ni adhabu ambayo si ya kinyama tu na ukatili kwa kuwa inaleta maumivu hasa ya kimwili, lakini zaidi anayepokea adhabu hiyo inamuondolea hadhi yake yote na kujiheshimu kwake…..Inafanya mtekelezaji na kupita kwake, jamii kujiweka katika kiwango cha mhalifu[56]".

FIDH inatoa wito kwa serikali ya Tanzania kuzifanya sheria za nchi ziendane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu na kukomesha adhabu ya viboko katika hali zote.

## Hukumu za chini (ndogo) zinaendelea kuongezeka

Kama ilivyojadiliwa hapo juu mazoea ya kuridhia sheria za hukumu za chini (ndogo) zilianza ghafla baada ya uhuru, na wakati huo serikali iliamini kwamba majaji walikuwa na huruma sana katika kuwa hukumu wahalifu. Sera hii inaelekea kutokuwa na mwisho kwa sababu hukumu zimekuwa zikiendelea kuongezeka.

Sheria ya hukumu ya chini ilirekebishwa mwaka 1989, na kuongeza kupindi cha kifungo kwa unyanganyi wa kutumai silaha kutoka kifungo cha miaka 7 hadi 30. Na ule unyanganyi wa kutumia nguvu miaka 15. Sheria imerekebishwa tena mwaka 1998 kwa kipindi cha kifungo cha chini kwa ubakaji na jaribio la ubakaji kuongezeka hadi kifungo cha miaka 30 na viboko. Kifungu cha 156 cha Kanuni ya Adhabu, pia kimerekebishwa na adhabu ya chini kwa shambulio la aibu hadharani iliongezeka kutoka kifungo cha miaka 7 hadi kifungo cha maisha.

Kifungu cha 10 kiliongezwa kwenye sheria ya adhabu ya kifungo cha chini, kikisema kwamba "hakuna kitu chochote katika sheria hii kitakachotafsiriwa kuzuia mahakama kutoa adhabu ya kifungo kulingana na makosa yaliyoainishwa kutoa zaidi ya kipindi cha kifungo cha chini kilichowekwa kwenye sheria hii kwa kosa husika.

---

[53] General comments 7(16) and 20(44)

[54] Kifungu cha tano cha katiba ya Afrika kinasomeka "kila mtu atakuwa na haki kwenye kuheshumu hadhi/heshima iliyorithiwa na binadamu na utambuzi wa hali yake ya sheria. Aina zote za unyonyaji na udhalilishaji wa watu hasa utumwa, biashara ya utumwa mateso, ukatili, unyama au adhabu za uzalilishaji wa matendo yatakatazwa.

[55] Communication 236/2000, *Curtis Francis Doebbler v. Sudan*, 15-29 mai 2003,16 rapport annuel d'activité de la Commission africaine des droits de l'Homme et de peuples, 2002-2003, p 56-61.

[56] Supreme court of Zimbabwe Judgement No.S.C. 156/87 of 1987.

Ukichukulia kwamba nyingi kati ya hizo hukumu za chini zimewekwa kifungo cha miaka thelathini, ni vigumu kufikiria namna jaji angeweza kufikiria adhabu kali zaidi. Profesa Shahidi aliuambia ujumbe wa FIDHI kwamba kwa sasa adhabu ya chini ya miaka thelathini inaungwa mkono na Bunge na watu wengi. Kamishna wa kwanza Mtanzania wa Magereza alisema katika taarifa ya Magereza ya mwaka 1963 kwamba "kazi ya utawala wa magereza ni kuendeleza sera mpya iendane sawa na mawazo yaliyoendelea kuifanya si tu kwa madhumuni ya kuadhibu lakini kwa umuhimu iwe urekebishaji".

Ilikuwa imeamuliwa kwamba urekebishaji wa wakosaji liwe ni lengo la msingi la kifungo. Kama ilivyo kifungu cha 62 cha sheria ya magereza ya 1967 kinasema kwamba " kila mfungwa aliyehukumiwa kifungo na wafungwa walioko kuzuizini apewe ajira/mafunzo, … na kutendewa katika hali ambayo kamishna atavyoamua na kwa madhumuni hayo mfungwa wakati wote atafanya kazi kama hiyo kazi na wajibu mwingine kama zitakavyogaiwa kwake na maafisa wengine wasimamizi". Kifungu cha 63 kinafanya rekebisho hilo hilo kwa mafunzo ya wafungwa wanawake.

Hata hivyo ni vigumu mtu kuona aina hii ya urekebishaji katika kifungo cha miaka thelathini. Hukumu hii inadhamiria kumuondoa mtu kutoka katika jamii na kama mtu kusalimika na adhabu hiyo,[57] basi atabaki na doa lisilofutika katika maisha yake.

Utendaji wa utoaji adhabu wa kiwnago cha chini, hauonyeshi tu mashaka ya serikali ya Tanzania juu ya mahakama. Lakini inaweza kuchukuliwa kuwa uvunjaji wa sheria ya mgawanyo wa madaraka, kwani, bunge linaweka adhabu na kulazimisha matumizi ya utumiaji wa umakini katika mahakama.

Kwa kuwa adhabu hizo kali za kiwango cha chini haziruhusu upimaji wa hali ya mshitakiwa[58], inaweza kupelekea adhabu isiyowiana na kosa lililotendwa. Kwa hali hiyo, adhabu ya kiwango cha chini cha miaka 30 jela inaweza kuchukuliwa kama udhalilishwaji wa utu wa mtu na hivyo ukiukaji wa ICCPR, Mkataba wa Afrika na Katiba ya Tanzania.[59]

Adhabu hizo nzito za kiwango cha chini zinzonesha ukweli kwamba mfumo wa haki wa makosa ya jinai Tanzania umeegemea kwenye kulipiza visasi kwa kusababisha mateso kwa mkosaji ambaye amevunja sheria. Kwa kawaida kosa la jinai lilichikuliwa kama kosa la moja kwa moja dhidi ya mamlaka, na kwa hiyo inastahili adhabu nzito na ya kuonekana wazi, yaani adhabu ya kifo, adhabu ya viboko au kifungo cha maisha isiyopungua kipindi cha miaka 30.

---

[57] Mtu anapaswa kufikira kwamba umri wa binadamu Tanzania unakadiriwa kuwa miaka 46. Kulingana na Shirika la Afya Duniani katika World Health Report 2004 (annex 9)

[58] Kama mfano, wizi wa kutumia silaha wanapewa adhabu ya kiwango cha chini ya miaka 30, hata kwa wizi wa kisasi kidogo cha shilingi 500 za Kitanzania.

[59] Kama utatumia jaribio lisilo linganifu (jaribio hili litaeleza uholela huo usio wa kawaida au adhabu zisizowiana na kosa lililofanywa ambalo linashitua dhamiri ya umma, kwamba ni dhamiri ya mtu anayefaa/mtu anayefikiri sawa, imezuiliwa). Tunaweza tu kufikia kwenye hitimisho hilo. Jaribio hili lilitumiwa na Mahakama ya juu kabisa ya papua katika rejea la Kikatiba na serikali ya jimbo la Morobe (mwaka 1985 na Mahakama ya juu ya Zimbabwe katika kesi ya Nchi dhidi ya Uarabu (1990). Na hivi karibuni Mahakama Kuu ya Namibia ilitangaza kupinga Sheria ya Risasi/Baruti ya mwaka 1996 kuwa isiyo ya kikatiba ambayo iliagiza adhabu ya kiwango cha chini ya miaka 10 jela. Majaji waliamua kwamba "Kama aina Fulani ya adhabu inaidhinishwa kwa sheria inaweza kusemwa vizuri kuwa ya kinyama inayohusisha thamani ya hukumu na mahakama mabayo lazima ikaisi kaida za wakati ule ule, hamu, matarajio na unyeti/hisia wa watu wa Namibia kama inavyoelezwa katika taasisi za taifa na katika katiba. Pia makubaliano yaliyofikiwa ya thamani katika jumuiya iliyoendelea ya kimataifa jaribio ambalo lingefaa ni kwamba mahakama isingejiingiza katika hukumu labda, imedhihirika wazi kuwa kubwa mno kwamba hakuna mtu mwenye akili zake/affaye angetoa adhabu hiyo". Adhabu ya kiwnago cha hcini ya miaka 10 ni kubwa na haiwiani wakati inaonekana katika mwanga wa rushwa kamili pana – S. 29 (1)(a) hizo zinaweza kutokea mahakama isilazimike kutamka tu S. 38(2)(a) kutotekelezwa katika kesi mara moja, lakini katika kesi zote. Mwendo ufaao ni kupinga maneno hayo, yasiyo chini ya miaka kumi, lakini kutoka S. 38(2)(a) ya sheria" Angalia Nchi dhidi ya likuwa (1999) ICHRL 41 (ya tarehe 24 Machi, mwaka 1999.

Mtazamo huu kwa wahalifu katika uhalifu wa jinai ni ukumbusho wa Zama za Giza, kama ilivyoelezwa na Mbunge,[60] na kwa kweli, hauna nafasi katika haki za jinai za hivi sasa. FIDH inaamini kwamba Tanzania haiwezi kulinda amani na usalama wa umma kwa kupitia utaratibu huo, ambao unaendeleza chuki na vurugu katika jamii yote.

## 3. Rushwa: Tishio katika mchakato wa marekebisho

Katika mahojiano yote yaliyofanywa na ujumbe wa FIDH, rushwa imekuwa neno kuu linaloambatanisahwa katika utendaji mbaya ---- wa mahakama ambapo inapelekea ukiukwaji wa haki za binadamu. Rushwa imetapakaa kote na takwimu rasmi zinaonyesha kwamba polisi na mahakama inaongoza kwa kiwango kikubwa katika ushindani huu wa kuaibisha.

Ilionekana kwamba wajumbe wa FIDH kwa haraka sana walihitaji kujadili mada hiyo na mamlaka inayohusika. Kwa hakika ilikuja mara moja kwamba wajumbe wa FIDH kwa haraka sana walihitaji kujadili mada hiyo na mamlaka zinazohusika na tatizo, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (*TAKURU*). Kwa bahati mbaya, licha ya kujaribu mara mbili na baada ya kusubiri saa chache katika chumba cha mapokezi cha *TAKURU*, ujumbe haukuweza kumpata yeyote aliye tayari kujibu maswali hayo au angalao aweze kutoa taarifa sahihi na takwimu.

Hata hivyo, FIDHI wameweza kukusanya taarifa muhimu kutoka kwenye mikutano ya waandishi wa habari, vichwa vya habari katika magazeti na usahili.

Maelezo ya hali katika nchi yaliyofanywa na Ibrahimu Seuchi, Mkurugenzi wa Transparency International's Global Consultant katika Tanzania yanatisha. Tabia ya rushwa ya wanasiasa katika jamii inapelekea ulaghai na ubadhirifu unaogharimu mamilioni ya shilingi za watu wa Tanzania kila mwaka. Watu wanataka kuteuliwa vyeo vya ngazi za juu za umma aghalabu watalipa kulinda nafasi zao au kupatia mdhamini kutoka kwa watu matajiri. Ibrahimu Seuchi alibainisha kwamba vitendo vya rushwa vinavyofanywa vimestawi katika ngazi za juu za siasa katika Tanzania na wanadumaza mabadiliko na vita dhidi ya hongo na kipimo/skeli kikubwa cha rushwa.[61]

Kuhusiana na *TAKURU* hukumu bado ni mbaya. "*TAKURU* lazima wasaidiwe kikamilifu na serikali na lazima wawe na uwezo wa kuchunguza na kufuatilia kesi zote. Leo *TAKURU* hawajajizatiti vya kutosha siyo kwa ujuzi wala kwa vifaa.

Wazo hili lililotolewa mwaka 2002 bado lina kashfa yenye ukweli. Hasa katika suala la haki ni ya wazi. Christina John Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa, wakati alipokuwa akiwasilisha mada katika warsha ya Uzuiaji wa Rushwa uliofanyika Dar es Salaam tarehe 22 Desemba 2003, alitoa taarifa kwamba, miongoni mwa idara zote za serikali, polisi imeelekea kuwa na kiwango kikubwa/idadi kubwa ya tuhuma za rushwa, vile vile idaray nyingine zilizotuhumiwa ni mahakama na serikali kuu.[62]

---

[60] Kwenye hatua za upenyo/kuona, bwana hati inaweza kuturudisha nyuma, Enzi za Giza, lakini kwamba kwa usahihi ni hoja kwa matakwa yake. Kama ilivyo ukali wa adhabu katika kipindi cha Ujerumani ilikuwa kigingi kifaacho kwa Tume ya Makosa ya aina chini ya kuipitia tena hati. Gurudumu limegeuka mzunguko mzima. Haya ni maneno ya Mheshimiwa Mbunge Bajaj, ilidondolewa na Profesa Shaidhi katika mfumo wa kutoa adhabu: Adhamu au masahihisho ya wahalifu.

[61] Kauli iliyotolewa mwaka 2002 wakati Ripoti ya Mwaka ya Uwazi kimataifa ilipotolewa.

[62] Polisi waongoza kwa Rushwa; Nipashe ya tarehe 3 Desemba 2003. Tuliambiwa na mamlaka ya polisi Zanzibar kwamba suala lipo katika agenda, na tulionyeshwa ishara/dalili zinasema kwamba huduma za polisi ziko huru/hazihusiki, zilizotumwa katika kila kituo cha polisi. Pia kanuni zilieleza kwamba afisa wa polisi na mbaye amemweka yeyote jela haweza kutoa amri ya kuachiwa huru kwake, ili kukwepa biashara seli,. Hata hivyo majaribio haya yanaonekana

Wakati ujumbe wa FIDH ulipokuwa nchini, Gazeti liliripoti kwamba Taasisi ya Kuzuia Rushwa katika Wilaya ya Korogwe wamemtia mbaroni Hakimu Mkazi, Masengwa Innocent Mihayo, kwa kutaka/kuomba na kupokea hongo ya shilingi 50,000/= za Kitanzania.[63]

Rushwa imeripotiwa kuwa imeenea katika kufungua majalada ya kesi, kupanga tarehe za kusikiliza kesi, kutafuta majadala ya kesi, kuidhinisha hati ya muda ya mahakama ya kusitisha utekelezaji na kusubiri hukumu, kutoa nakala za hukumu na mashauri ya mahakama, utoaji idhini ya dhamana, kutoa kiambatanisho chenye amri ya mahakama, kutoa maombi mbalimbali mahakamani (kwa ajili ya kusikiliza kesi zisizohitaji kusikilizwa hadharani), malipo ya washauri wa mahakama n.k. vitendo hivi vinahatarisha kwa kiasi kikubwa maisha ya wasio na hatia ambao wanaweza kuhukumiwa adhabu za vifo kwa sababu katika hatua moja ya taratibu hawakupatiwa nyaraka muhimu, au wameshindwa kutumia haki zao kwa sababu wameshindwa kupata shilingi 50,000/= za Kitanzania[64] zilizoombwa/takiwa na hakimu mkazi mla rushwa au afisa wa polisi.

Serikali ya Tanzania lazima ifanye zaidi kuliko tu kuchunguza rushwa kwamba itasababisha matatizo katika mfumo wa haki na kupanga vizuri mipango ya hadi mwaka 2025.[65] Wanahitaji kufanya zaidi kuliko kuanzisha namba ya simu ya kuzuia rushwa, inayoonekana kutofanya kazi kabisa[66], na Taasisi ya Kuzuia Rushwa ambayo haifikiwi na wananchi walio wengi. Kwa kurahisisha, hali ilivyo inahitaji kwa pamoja fedha za kutosheleza, bidii ifanywe mara moja. Hata hivyo, hairidhishi kuona rushwa imefikia kiwango hicho katika nchi ambayo inaridhiya/inafuata sheria, mitazamo ya umma na imani lazima zibadilike, katika taswira hiyo, utetezi, ushawishi na kazi ya kukuza uelewa juu ya suala la rushwa lazima iendelezwe.

## IV. Makosa yanayoadhibiwa kwa adhabu ya kifo nchini Tanzania

Kuna makosa matatu yanayoadhibiwa kwa adhabu ya kifo katika mfumo wa Sheria Tanzania. Makosa haya ni kuua kwa kukusudia, uhaini na mwenendo mbaya wa makamanda/utendaji ulio kinyume na maadili ya makamanda au askari yeyote katika uwepo wa adui.

### 1. Kuua kwa kukusudia

Sura ya 16 ya kanuni za adhabu inaeleza katika Kifungu cha 196 kwamba “Mtu yeyote ambaye amefanya makosa kwa kudhamiria akasababisha kifo cha mtu mwingine kinyume cha sheria au kutojali ana hatia ya kuua kwa kukusudia”. Kifungu cha 197 kinaeleza kwamba “Mtu yeyote mwenye hatia ya kuua kwa kukusudia atahukumiwa kifo”.

Adhabu hii ni lazima ikieleza kwamba ikithibitika bila shaka yoyote kwamba mshitakiwa ametenda kosa la mauaji.

---

kutotosheleza kutokana na ripoti iliyochapishwa kwenye magazeti.

[63] Hakimu mkazi atiwa mbaroni kwa hongo ya shilingi za Kitanzania 50,000/- Daily News, ya tarehe 9 Oktoba mwaka 2004.

[64] Sawa na Euros 4.5 kwenye mwezi Oktoba mwaka 2004.

[65] Waziri wa Haki/Adili alisema kwenye mkutano wa waandishi wa habari uliofanyika Dar es Salaam tarehe 9 Oktoba mwaka 2004 juu ya Dira ya kurekebisha agenda 2025 kwamba, mbali na ukosefu wa uadiifu na uhalali wa mfumo wa sheria. Rushwa lilikuwa tatizo lingine linalozuia usimamiaji mzuri wa haki katika nchi.

[66] Wajumbe wa FIDH walijaribu mara kadhaa kupiga namba 113 ya uzuiaji rushwa tarehe 10 Oktoba mwaka 2004 pasipo kumpata yeyote.

Kiutendaji, mara nyingi uendeshaji wa mashitaka kwa kesi za mauaji zinapelekea hukumu ya kuua bila kukusudia, ambayo haiadhibiwi kwa adhabu ya kifo. Kifungu cha 195 kinasema kwamba, Mtu yeyote ambaye kinyume cha sheria au kwa kutotimiza wajibu amesababisha kifo cha mtu mwingine ametenda la kosa la jinai liainishwalo kama kuua bila kukusudia".

Kifungu cha 211 kinaeleza kwamba "Mtu yeyote ambaye amefanya jaribio lisilo halali kutaka kusababisha kifo kwa mtu mwingine ametenda kosa la jinai, na adhabu yake kisheria ni kifungo cha maisha.

Kulingana na takwimu za mwezi April mwaka 2003, katika magereza ya Tanzania bara, washitakiwa 549 ambao walishitakiwa kwa kuua kwa kukusudia mwishoni walikutwa na hatia ya kuua bila kukusudia. Mwezi April 2003, kulikuwa na wafungwa 370 ambao walikutwa na hatia ya kuua kwa nia na walihukumiwa kifo.[67]

Licha ya kitendo cha kufifisha kinachofanyika katika kushughulikia hukumu ya uuaji wa bahati mbaya, hukumu ya lazima inahifadhiwa katika kitau cha sheria cha bado inatolewa katika kanuni ya adhabu za Tanzania. Kamati ya haki za binadamu ya Umoja wa Mataifa pamoja na mahakama za nchi mbalimbali duniani kote zinachukulia ya kifo kama ukiukaji wa haki ya kuishi.

Kamati ya Haki za Binadamu ilieleza katika kesi ya *Everslye Thompson dhidi ya St-Vicent na Grenadines* kwamba "Mfumo kama huo wa adhabu ya kifo ingeweza kumnyima mtungaji wa haki kubwa za msingi, haki ya kuishi, bila kuzingatia kama aina hii pekee ya adhabu inafaa katika mazingira ya kesi yake".[68]

Kamati ilieleza kwamba uwezekano wa msamaha au uwezekano wa kupunguziwa adhabu hakutabadilisha matokeo, hivyo kwamba "Uwepo wa haki ya kuomba msamaha/ na kupunguziwa adhabu…… hailindi vya kutosha haki ya kuishi, kwani hatuahizi zenye uamuzi wa watendaji zina eneo kubwa la mambo mengine ukilinganisha na uchunguzi wa mahakama katika vipengele vyote vya kesi za jinai".

Katika kesi ya Edwards na wengine dhidi ya Bahama, Tume ya Amerika ilikuta kwamba uwekaji wa lazima wa adhabu ya kifo kunakiuka masharti mengi ya Azimio la Amerika juu ya Haki na Wajibu wa Mtu.[69]

Mahakama ya Rufaa ya Carribean Mashariki iliamua kwamba uwekaji wa lazima wa adhabu ya kifo ilikuwa kinyume cha katiba, kwani inachangia utendaji usio wa kibinadamu na adhabu ya kudhalilisha.[70] Uamuzi huu hususan unafaa hapa, kwani uamuzi huu una nguvu ya sheria katika nchi sita za Jumuiya ya Madola. Mahakama pia ilitoa uamuzi juu ya "Ibara inayonyima haki. Ibara hiyo ni sawa na zile zilizomo katika katiba ya Tanzania.

---

[67] Hotuba iliyowasilishwa bungeni kipindi cha bajeti 2003/2004 uk. 52 na Mheshimiwa Omari Mapuri (Mbunge) Waziri wa Mambo ya Ndani.

[68] Eversley Thempson dhidi ya Santavisent na Grenadini, mawasiliano No. 806/1998, UN. DOC. CCPR/C/70/D/806/1998(2000).

[69] Ripoti namba 48/01 (ya tarehe 4 Aprili 2001), Ripoti ya mwaka ya Tume miongoni mwa Amerika juu ya Haki za Binadamu (IACHR) 2000.

[70] Peter Hugues na Newton Spence dhidi ya The Queen, tarehe 2 April 2001, Mahakam aya Rufaa ya Karibiani Mahsariki, Rufaa ya Jinai ya tarehe 17/1997 na tarehe 20/1998. Kamati ya Mahakama ya Baraza la siri (Mahakama ya mwisho ya rufaa kwa nchi za Jumuiya ya Madola karibiani) ilirudisha jambo hilo/kesi hiyo kwenye mahakama ya mashariki kufikiria na kuamua juu ya ulazima wa adhabu ay kifo kwa mujibu wa kikatiba.

Licha ya ukweli kwamba majaji mara nyingi hawatoi adhabu ya kifo juu ya mashitaka ya mauaji ya kukusudia (na pasipo msukumo fulani, kama Jaji Bahati alivyowaambia wajumbe wa FIDH, jaji wa zamani wa Mahakama Kuu, sasa ni Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria ya Tanzania), Tanzania inaendelea kutenda kazi kinyume na viwango vya Kimataifa na inatakiwa ifikirie kufuta adhabu ya kifo na kutoa mwanya katika hukumu hiyo.

## 2. Uhaini

Katika vifungu vya 30 na 40 ya Kanuni ya Adhabu, uhaini unaadhibiwa kwa adhabu ya kifo. Hata hivyo, maneno "akipatikana na hatia atahukumiwa kifo" Imefasiriwa na Mahakama za Tanzania kama kuweka tu kikomo cha juu, badala ya hukumu ya lazima.

Hakuna mtu aliyehukumiwa kifo kutokana na sababu za uhaini toka uhuru.[71] Hata hivyo, FIDH inachukulia kwamba kuendelea kuwepo kwa kosa hili katika Kanuni ya Adhabu ya Tanzania kunakiuka viwango vya kimataifa. Ibara ya 6(2) ya ICCPR inaeleza kwamba: "katika nchi ambazo hazijaondoa adhabu ya kifo, hukumu ya kifo inaweeza kutolewa tu kwenye makosa makubwa ya jinai. Maoni ya jumla yaliyoridhiwa na kamati ya Haki za Binadamu ni kwamba: "Kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 6(2) mpaka (6) nchi wanachama hazijafanya hazijalazimishwa kuondoa kabisa adhabu ya kifo badala yake wametoa kikomo cha utumizi wake na hususani kuiondoa kwenye makosa yasiyo makubwa sana".

Zaidi ya hayo, vyombo vya Umoja wa Mataifa umeanisha kwamba: "… *adhabu ya kifo inaweza tu kutolewa kwa makosa makubwa kabisa, inaeleweka kwamba kikomo chake kisiende kinyume na makosa ya kudhamiria inayohusiana na kifo au madhara mengine yenye hatari kubwa mno*".

Dhana ya makosa ya jinai haijumuishi makosa kama uhaini, ambayo yana chanzo cha kisiasa. Mjumbe mahsusi wa Umoja wa Mataifa kuhusu taratibu zilizo nje ya mahakama/nje ya sheria, muhtasari au kunyonga kwa hiari/atakavyo, ilieleza kwamba "Masharti haya hayajumuishi uwezekano wa kutoa adhabu ya kifo kwa makosa ya kiuchumi na mengine yanajulikana kama makosa yasioathiri, vitendo vinavyohusiana imepatikana inashinda maadili mema au shughuli za kidini au yenye asili ya siasa – ikijumiisha sheria za uhaini ujasusi au vitendo vingine vinafafanuliwa kama vinavyoleta mashaka/kutia hofu kwa kawaida vinaelezwa kama "makosa *dhidi ya nchi*".[72]

Viongozi fulani wa Tanzania waliwaambia FIDH kwamba kosa hili lingeweza kuondolewa kwenye Kitabu cha sheria. Kwani hakuna mtu yeyote amewahi kuhukumiwa kifo kwa shitaka hili. FIDHI wana maoni kwamba lazima ifanyike ghafla/papo hapo kulingana na Vyombo vya Haki za Binadamu Kimataifa, ambavyo vimeweka bayana masharti juu ya Serikali ya Tanzania.

---

[71] SMZ dhidi ya Machano Khamis Ali na wengine kumi na wane, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, Maombi ya jinai Na. 8 ya mwaka 200, tarehe 3, April 2000 (haijaripotiwa). Ilichukuliwa na Mahakama ya Rufaa kwamba uhaini ni kosa dhidi ya Muungano tu, na kwa ivyo haiwezi kuelekezwa, kama dai katika mashitaka, dhidi ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kiongozi wa Serikali wa Zanzibar. Hivyo majaji walibatilisha shitaka, kama elementi/msingi wa kosa ya kosa haikufanyika/haikufanyika nje.

[72] Angalia Raia na haki za Siasa, ikijumuisha swala la kutoweka na Muhtasari wa kunyonga. Ripoti ya Mwandishi/Katibu maalumu kuhusu taratibu nje ya mahakama/iliyo nje ya sheria, muhtasari wa hiari ya kunyonga/unyongaji hiari, Bi Asma Jahangir, aliwasilisha ukimbizaji/ufukuzaji kwa Tume juu ya Azimio la Haki za Binadamu 2001/45 UN DOC.E/CN.4/2002/74

## 3. Mwenendo mbaya wa Makamanda au Askari yeyote katika uwepo wa adui

Jedwali/ratiba ya kwanza kwa Sheria ya Ulinzi wa Taifa na. 24 ya mwaka 1996 inaruhusu utoaji wa adhabu ya kifo kwa usaliti unaofanywa na makamanda au askari yoyote katika uwepo wa adui. Adhabu ya kifo chini ya masharti haya siyo ya lazima (Angalia Ibara ya 11, 12, 13, 14, 16 na 17 ya jedwali/hati kwa sheria ya Ulinzi wa Taifa Na. 24 ya mwaka 1966).

Sheria hii haijawahi kutumiwa. Hata hivyo, hoja zinazotolewa kuhusu uhalifu ni sawa kutumika kwa kosa hili na sharti lazima kwa hiyo liondolewe.

**Kundi la Waathirika**

Kwa mujibu wa viwango vya Haki za Binadamu kimataifa, mtu mwenye umri chini ya miaka 18 wakati anafanya kosa hawezi kuhukumiwa kifo, wakati adhabu ya kifo haiwezi kufanyika kwa wanawake wajawazito au wanaotarajiwa kuwa akina mama na watu ambao wamekuwa vichaa.[73]

Katika sheria za Tanzania, imeelezwa katika aya ya 2 ya kifungu cha 25 cha kanuni za adhabu kwamba; "Adhabu *ya kifo haiwezi kutangazwa au kurekodiwa dhidi ya mtu yeyote ambaye, kwa moni ya mahakama* ***ana umri chini ya miaka kumi na nane***".

Pia kuna utata kuwa tamko haliko bayana kama kiwango hiki cha umri kinarejelea muda wa kosa lilipofanika tu (kama elezwa kwenye viwango vya kimataifa) au juu ya hukumu.

Katika kesi ya *Jamhuri ya Tanzania dhidi ya Lubasha Maderenya na Tegai Lebasha*[74] Mahakama Kuu ilikataa kutoa adhabu ya kifo juu ya mmoja wa washitakiwa ambaye alikuwa na umri chini ya miaka 18 wakati kosa (mauaji) lilipofanyika. Kuhusu rufaa, Mahakama ya Rufaa ilitupilia mbali hukumu, uamuzi kama huo unakiuka viwango vya kimataifa na inalaumiwa kwamba ni matokeo ya uamuzi uliopitishwa na mahakama ya juu katika mfumo wa Sheria wa Tanzania. Inatia matumaini, uamuzi huu ni wa pekee na utabaki kama ukumbusho wa kinyume cha haki .

Suala la **wanawake wajawazito** lilitiiwa maanani chini ya sehemu ya 197 ya Kitabu cha Sheria kiwekea sharti kwamba "kama mwanamke ana hatia ya kosa liadhibiwalo kwa kifo inadaiwa ni mjamzito, mahakama itadadisi na kama itathibitishwa kwa utoshelevu wa mahakama hiyo kwamba ni mjamzito adhabu itakayopitishwa itakuwa kifungo cha maisha badala ya adhabu ya kifo.

Hali ya mshitakiwa **kuumwa akili** ni tatizo zaidi. Kitabu cha Sheria cha makosa kinaeleza katika sehemu ya 12 kwamba "Kila mtu anafikiriwa kuwa na akili timamu, na kuwa ana akil timamu na anachukuliwa kwamba ana utimamu wa akili muda wowote atakapohitajika mpaka ithibitike vinginevyo". Inaanzisha dhana ya kisheria kuwa kila mshtakiwa alikuwa na akili timamu wakati anapodaiwa kutenda kosa kwamba ni nguvu kubisha/kukanusha.[75]

---

[73] ICCPR, kifungu cha 6, aya ya 5, vyombo vya Ulinzi vinahakikisha ulinzi wa haki wa wote wenye adhabu ay kifo (iliridhiwa na baraza la Uchumi wa Jamii Azimio la mwaka 1984/50 ya tarehe 25 Mei 1984), kifungu cha 3, makubaliano juu ya Haki za Mtoto, mwaka 1989, kifungu cha 37 (a).

[74] Mahakama Kuu (mwanza) Kiindi cha Kesi ay Jinai Na. 143 y amwaka 1977.

[75] Hii imechukuliwa kutoka uamuzi wa kesi ya R.v. Mc Naghten (1843) 10 CL. Na F. 200 ambayo inadhania kwamba/inakisia kwamba kila mtu ni timamu /ana akili timamu labda ithibitishwe kwamba kama matokeo ya ugonjwa wa akili kwa wakati muhimu alipokuwa hana uwezo wa kuelewa nini anachokifanya au alikuwa hana uwezo wa kujua kwamba anakifanya ni makosa.

Kanunu ya adhabu chenye makosa na adhabu zake kinaeleza "mtu hawajibiki kijinai kwa tendo au kutotimiza wajibu kama kwa wakati huo aliofanya kosa au alipoacha kutimiza wajibu alikuwa anasumbuiwa na ugonjwa wowote ulioathiri akili yake. Kushindwa kuelewa nini anachofanya, au kujua kwamba hakupaswa kufanya kitendo hicho au kutotimiza wajibu" lakini kinaongeza kwamba "mtu atawajbika kwa kosa la jinai kwa tendo au kutotimiza wajibu ingawa akili yake imedhuriwa na ugonjwa, kama ugonjwa huo kwa kweli hauletei akili yake moja au nyingine ya madhara/matokeo yaliyotajwa juu kuhusu kitendo hicho au kutotimiza wajibu.

Kiutendaji, washitakiwa kadhaa wamehukumiwa kufa ingawaje wataalamu wa ugonjwa wamethibitishia mahakama kwamba mtu alikuwa na ugonjwa mkubwa wa akili, lakini mahali ambapo haikuthibitishwa hivyo ungojwa huu umeathiri akili yake kiasi cha kumfanya kushindwa kuelewa nini anachokifanya. Katika kesi ya *Said Abdallah Mwamwindi dhidi ya Jamhuri*[76], mtuhumiwa alihukumiwa kifo (na hukumu hiyo ilitekelezwa), licha ya kwamba Doktari daktari anayeaminika wa magonjwa ya akili Dk. W. S. Pendaeli alithibitisha kwamba mshitakiwa alikuwa na ugonjwa wa akili ujulikanao kama wazimu.

Wengi wa Majaji wa Mahakama ya Rufaa wana utambuzi wa udhalimu huu na wa ukweli kwamba vifungu hivi limepitwa na wakati, lakini hakuna hata mmoja wao anaonekana kuwa tayari kukataa matumizi ya sharti hilo.

Maoni/mawazo haya yalielezwa kwa uwazi na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania katika kesi ya *Agnes Doris Liundi dhidi ya Jamhuri* ambapo ilisemwa "Inawezekana kwa kweli inaelekea kamba sheria zetu katika suala la kudhuru afya ni kuu kuu na limepitwa na wakati. Bunge, katika hekima yake linaweza kurekebisha hili tawi mahususi la sheria na kuliweka katika mstari/mwelekeo na maarifa ya kisiasa ya tiba juu ya suala hili".[77]

Mpaka leo, serikali haijachukua ari yoyote kurekebisha sheria hiyo na kuweka katika mwelekeo/mstari na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

## V. Utungaji wa hatia: Safari katika mfumo wa makosa ya jinai wa Tanzania.

*"Uwezekano wa makosa ya mahakama, kwa sababu yoyote, inafikiria kwa sababu adhabu ya kifo isiyobadilika, ni mwisho wa shauri na haiwezi kukabilishwa. Na ikumbukwe, hatia baada ya mauaji kimakosa (baada ya kukata rufaa), siyo mara chache" Jaji Mwalusanya.*[78]

Uchunguzi huu utaangalia tu juu ya watu walioshitakiwa kwa mauaji ya kukusudia, kwani hili ni kosa kuu linalopelekea adhabu ya kifo. Makosa haya mahususi kwa kweli yako mbali na jambo la pekee katika usimamiaji wa kesi za jinai; kwani tarehe 1 Aprili mwaka 2003, wafungwa 7090 waliokuwa mahabusu katika magereza ya Tanzania bara walishitaiwa kwa uuaji wa kukusudia kati ya jumla ya wafungwa 19,117 waliokuwa mahabusu.[79] ( 37% ya wafungwa wote).

---

[76] Saidi Abdallah Mwamwandi dhidi ya Jamuri, mwaka 1972 H.C.D. Na. 212. Matokeo ni sawa na yale ya R.V. Asha Mkwizu Hauli, ambapo wataalamu wawili mashuhuri wa Saikatria Dokta K. F. Rugeiyamu na Dokta W. S. Pendael walithibitisha kwamba washitakiwa walikuwa wanaumwa akili. Katika kesi ya D.P.P dhidi ya Leganzo Nyange, wataalamu wa Saikatria walithibitisha kwamba washitakiwa wana wazimu wa paranoid schizopherenia na bado walihukumiwa kifo.

[77] Ripoti ya Sheria Tanzania, 46 (1980)

[78] Jamhuri dhidi ya Mbushuu Alias Dominic Mnyanje na Kalai Sangula (1994) TLR 154.

[79] Chati Na. 11 kutoka kwenye hotuba ya Waziri wa mambo ya ndani, Omar Ramadhani Mapuri (Mbunge) iliyowasilishwa mbele ya bunge wakati wa makadirio ya bajeti kwa mwaka 2003/2004 uk. 52

## 1. Kukamatwa kwa mtuhumiwa.

Mara kosa lifanywapo na uhalifu kuripotiwa polisi, polisi watafanya uchunguzi utakaoonyesha kama kuna haja ya mtuhumiwa kukamatwa.

Kama Uchunguzi utamdhihirisha mtuhumiwa muhimu katika shauri, mtuhumiwa huyo kwa kawaida atakamatwa katika kesi ya makosa ya kukamatwa, kama vile mauaji ya kukusudia. Kukamata kunaweza hata kufanywa kwa mtu, ambaye yupo kwenye uwepo wa mtuhumiwa kwa makosa yoyote yaliyoorodheshwa katika sehemu ya 14 ya Sheria ya Taratibu za Makosa ya Jinai.

Ujumbe wa FIDH hasa ulionana na wahalifu wawili, Ndugu Emmanuel na M. Geredje, katika gereza la Kilimani kati, Zanzibar, katika kesi zao, kosa lilitendwa Oktoba mwaka 1998 na wote walikamatwa Novemba mwaka 1998.

Kwa mujibu wa Taratibu za makosa ya Jinai Tanzania, mtuhumiwa lazima apelekwa mbele ya Jaji ndani ya saa 24. Kwa bahati mbaya kulingana na idadi ya mashahidi walioonana na Tume ya FIDH, sheria hii inatekelezwa mara chache. Watu ni mara nyingi wanawekwa mhabusu ya polisi kwa siku kadhaa kabla ya kupelekwa mbele ya Jaji. Katika kesi ya ndugu Emmanuel, kwanza aliwekwa mahabusu kwa siku chache kisha aliachiwa, na kukamatwa tena siku chache baadaye, ambapo alishikiliwa siku nyingine mbili katika mahabusu ya polisi kabla ya kupelekwa mbele ya Jaji. Utendaji huu wa kukamatwa, kuachiwa na kukamatwa tena inatumika sana katika vituo vya polisi, kama FIDH walivyoambiwa na mawakili watendaji. Wakati mwingine hili linaweza kuhusisha uachiliwaji wa dakika 10, kama muda wa kutembea nje ya kituo cha polisi kabla hawajakamatwa tena na kadhalika. Kwa kawaida Jaji hajulishwi kabisa juu ya mwenendo huu, hivyo haielekei kwamba kutakuwa na marekebisho yoyote.

Uwezo/madaraka makubwa ya kukamata yanapingwa na mawakili wa nchini[80] pamoja na asasi za haki za binadamu nchini na za kimataifa[81]. Tume ya kurekebisha Sheria ya Tanzania inachukulia kwamba “Inaonekana kwamba madaraka ya polisi ya kukamata ni makubwa zaidi”. Ukamataji unaofaa/ulio bora lazima ufanyike baada tu ya uchunguzi kukamilika ama mara tu baada ya kosa kutendeka. Inawasilisha kwamba upotoshaji mwingi wa haki unafanyika katika ngazi hii ya kwanza ya mfumo wa haki/mfumo wa kesi.[82]

Wafungwa walitoa taarifa juu ya utendaji wa polisi wa kukamata na kifungo katika jela ya ndugu au marafiki, ikijumuisha watoto na wake wa watuhumiwa wakati watuhumiwa wanapotoroka kukwepa kukamatwa.[83] Utendaji huu unachangia **adhabu ya pamoja**, ni ukiukwaji dhahiri wa hulka ya mtu/tabia ya mtu ya wajibu wa mhalifu. Inapingana/inakinzana na dhana ya mchakato upasao. Masharti ya UDHR na ICCPR kuhusu haki ya shitaka halali inayoegemea kwenye kanuni kwamba wajibu jinai/wajibu wa mhalifu ni wa mtu pekee – siyo kabisa wa pamoja.

---

[80] Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania ya mwaka 2002, uk. 11.

[81] Angalia sea ya kulinda haki za binadamu, uchunguzi wa utendaji wa polisi katika nchi za Jumiya ya Maendeleo ya Afrika Kusini, mwaka 1997 – 2000, Machapisho ya Amnesty Internationa, 2002 (AFR 03/004/2002): “Ukamataji holela na kifungo kinyume cha sheria ni kunaynyaswa kwa kawaida kwa karibu eneo lote. Polisi aghalabu hukamata watu kabla ya kujenga ushahidi wowote. Wnakwepa wajibu chini ya shria za kitaifa la kuwapeleka wafungwa mbele ya mahakama ya sherai ndani/kwa kipindi cha muda kiichoainishwa.

[82] Angalia Tume ya kurekebisha Sheria ya Tanzania, Nakala ya mjadala juu ya Mtiririko wa Haki/mwenendo wa haki mwaka 2003.

[83] Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Tanzania, Ripoti maalumu kuhusu/juu ya Tanzania Bara.

Katika Tanzania, hatua ya uchunguzi kwa kawaida huanza baada ya kukamatwa ni kawaida kwa maafisa polisi kuomba kuahirishwa kutokana na mazingira kwamba uchunguzi haujakamilika. Kwa nyongeza, kwa mujibu wa ushahidi uliokusanywa, **ukamataji holela** ni wa kutishia mtu na kumshurutisha (Nitakukamta kama hautanilipa) mpaka malipizi binafsi (mashitaka ya uongo ya uuaji wa kukusudia yanaweza kupelekea adhabu ya jela) hadi mamlaka ya juu wanawakamata watu juu ya mashitaka ya uongo, ambayo baadaye yatamalizika.

Mhamasishaji wa Haki za Binadamu Ally Saleh[84] wa chama cha Haki za Binadamu Zanzibar aliiambia FIDH kwamba ukamataji holela ni kitendo cha kawaida Zanzibar ambapo katika kipindi cha uchaguzi na uteuzi wa kisiasa, wapinzani wananyamazishwa kwa miezi michache. Alitegema njia/mbinu hii itatumika miezi ijayo kwani uchaguzi umepangwa kufanyika katika muungano katika mwaka 2005. Mfano mwingine unaweza kuonekana Tanzania bara, kwenye tarehe 16 Julai 2003, viongozi sita wa CHADEMA[85] katika vijiji walikamatwa pasipo kupewa sababu. Baadaye walishitakiwa kwa wizi wa umilikaji usio halali wa silaha, mashitaka waliyoyapinga. Walifungiwa kaika ofisi ya CCM, ambapo walipigwa vibaya pasipo sababu.[86]

Utumiaji mbaya wa masharti ya sheria yaliyopo na matumizi mabaya ya madaraka siyo tatizo pekee tu linalotokea katika hatua hii ya awali ya mashauri ya makosa ya jinai. Hali ya kizuizi katika vituo vya Polisi inatisha/ogofya katika sehemu nyingi. Kwa mfano, mwezi Novemba mwaka 2002, wafungwa 17 walikosa hewa hewa hadi kufa katika kituo cha polisi Mbarari Mbeya. Waliokufa walikuwa miongoni mwa mahabusu watuhumiwa 112 ambao walifungwa/waliwekwa pamoja katika chumba kidogo chenye uwezo wa kushikilia watu 30 tu.[87]

Watuhumiwa wa makosa ya jinai waliripotiwa kubanana katika seli/chumba kidogo huko Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Morogoro, ambayo haina madirisha kwa wafungwa kupata hewa. Kutokana na hali hii, tarehe 25, Juni, 2003 wafungwa katika mahakama hii[88] walikataa kuingia katika chumba hicho kidogo.[89]

---

[84] Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Haki za Binadamu Zanzibar.

[85] Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha upinzani kinachowasilishwa katika bunge na Baraza la Wawakiishi la Zanzibar.

[86] Haki za Binadamu Tanzania, 2003, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (KSHB/LHRC). Hakuna hatua ziizochukuliwa dhidi ya wakosaji wa kupiga kwa sababu Kamishna wa Wilaya wa eneo aliamuru polisi wasifuate matukio hayo.

[87] Haki za Binadamu Tanzania, 2003 Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (KSHB/LHRC) uk. 13. Ripoti iiyotolewa tarehe 31, Januari 2003 juu ya vifo vya Mbeya, ilitibitisha kwamba serikali imekua na uzembe wa wazi katika kushughulikia wafunga walioko mahausu. Ripoti ilieleza kwamba vyombo vya utekeleaji sheria ikijumuisha mahakama, ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Polisi na idara ya Magereza, haijadhukua vitendo hadaa/laghai kushughulikia matatizo a nyezo thawabu. Idara ya Magereza imewajibika kwa sababu imekiuka maadili ya weledi wake kwa kusonganisha mahabusu katika seli za magereza. Ripoti ilikaripia mahakama kwa kile walichotaja kama ufidhuli kwa kukataa kuulizwa na kamati ya uchunguzi. Hii ni moja ya ripoti maalumu inayorejelea kwa kula njama ya mahakama katika kushughulikia vibaya watuhumiwa kwa kushindwa kuchukua uangalizi ufaao kuwalinda na maonevu, ukatili au mateso. Hata hivyo, ingawa wajibu bayana wa mamlaka nne zinazohusika na uangalizi wa wafungwa, hakuna kiongozi kutoka katika ofisi hii waliochunguzwa au kufutiliwa. Maafisa wa ngazi ya chini ya gereza tu walishitakiwa kuhusiana na tukio. Angalia Ripoti ya haki za Binadamu Tanzania ya mwaka 2003. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

[88] Kwa kawaida wafungwa wnachukuliwa kotini tarehe iliyopangwa kwa kutajwa au kusikilizwa ya kesi zao na wanarudishwa katika sehemu zao za kizuizi mpaka itakaposikilizwa tena.

[89] << Sakata la Mgomo wa mahabusu mahakama sasa yasalimu mari >> (The detainees demonstrations saga, the court has now surrendered – Majira ya tarehe 2, Julai mwaka 2003).

Hali kama hii ya kizuizi inadhihirisha wazi unyama na utendewaji wa udhalilishaji unaozuiwa na viwango vya kikanda na kimataifa.[90]

Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Afrika, katika kesi ya Saro–Wiwa ilieleza; “ulindaji wa haki ya kuishi katika kifungu cha 4 inajumuisha wajibu wa nchi siyo kwa makusudi kumwachia mtu afe wakati yupo katika mahabusu/kifungo yake”.[91] Tume iliweka bayana kwamba wajibu wa serikali unazidishwa (kiwango) katika kesi ambayo mtu yupo katika mahabusu/kifungo chake na *kwa hiyo yeyote ambaye uadilifu na ustawi unategemea kabisa kwenye vitendo vya mamlaka (aya ya 112).*

Sehemu nyingine ya kuhusika zaidi ni matumizi ya nguvu ya maafisa kadhaa wa polisi. Hii inaanzia kutoka ukatili wa polisi katika seli za kizuizi hadi uuaji nje ya mahakama. Mfano wa nguvu hii inaweza kutajwa ile iliyofanywa katika kesi inayohusisha maafisa watatu wa polisi ambao walipigwa risasi mwezi Mei mwaka 2003 na waliodaiwa kuwa majangili katika eneo la Kawe, Dar es Salaam. Polisi ilimkamata Emmanuel Lugema (mwenye umri wa miaka 27), ambaye alifikiriwa kuwa alibuni/aliongoza uuaji wa maafisa. Baada ya kukamatwa kwake, pingu za Lugema ziliondolewa/ziifunguliwa na iliripotiwa alijaribu kukimbia. Afisa wa polisi alimpiga risasi na kuua pale pale.[92] Polisi ilitetea mauaji hayo kwa kuripoti kwamba mwathirika alipigwa risasi katika mashabulio ya risasi za pande mbili. Hata hivyo watetezi wa Haki za Binadamu wanaamini kwamba baadhi ya wanaodaiwa/wanaotuhumiwa kuwa wahalifu walipigwa risasi hadi kufa kwa makusudi na katika mazingira ambayo yasingeleta hatari yeyote kwa maisha ya polisi.

Kukataa kushirikiana na wachunguzi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Tanzania inasikitisha katika hali hizi. Ukataaji kama huo umekanwa wazi na Makamu Mwenyekiti wa Tume, Balozi Ramia Abdiwawa. Kwa mfano, afisa polisi wa kanda alikataa kufika kwa wachunguzi katika seli za polisi Lindi.

Maoni ya polisi ni kwamba Tume inafanya kazi zake kuwa ngumu zaidi, ambazo zinaonyesha tatizo hasa la kuelewa la mamlaka ya polisi. Kama mwenyekiti wa Kamati ya Haki za Binadamu ya Chama cha Sheria cha Tanganyika, ndugu Francis Stolla amesema “ Kwa polisi kila mtuhumiwa ni mhalifu. Mtazamo kama huo unatoa mwanya kwa mashambulio na ukatili wa polisi”. Matumizi ya nguvu dhidi ya wafungwa walio mahabusu ni tatizo kubwa.

Matumizi ya shurutisho la nguvu ili kupata ungamo kabla mtuhumiwa kupelekwa mbele ya Jaji ni jambo la muda mrefu.[93] Mtazamo wa mfumo wa polisi na ya serikali kuzuia mabadiliko yoyote. Mamlaka ya polisi Tanzania bara ilikataa kuwepo kwa tatizo lolote kama hilo.[94] Tamko la zamani la Rais Mkapa, anaonya wahalifu kutojaribu kabisa kuua askari polisi[95] na kutoka kwa Waziri Mkuu,

---

[90] Kanuni za msingi za Umoja wa Mataifa kwa utendewaji wa wafungwa (United national Assembly Resolution. 45/111 ya tarehe 14 Desemba mwaka 1990). Resolution 43/1973 ya tarehe 9 Desemba 1988). Sheria ya Kiwango cha chini ckwa utendewaji wa wafungwa (ECOSOC Resolution 663C(XXIX) ya tarehe 31 Julai mwaka 1957 na 2076 (LXII) ya tarehe 13 Mei mwaka 1977).

[91] Communications 137/94, 139/94, 154/96 na 161/07 International Pen, Constitutional Rights Project. Interights on behalf of Ken Saro – Wiwa Jr. na Civil Liberties Organization dhidi ya Nigeria aya ya 103.

[92] Polisi yawapiga risasi watuhumiwa wa uuaji wa maafisa wa polisi, imebamba wawili zaidi, The Guardian, ya tarehe 2, Juni mwaka 2003.

[93] Na kupeleka hali ya kurudi nyuma katika Mahakama, kama ilivyohusisha FIDH na ndugu Francis Stolla wa Chama cha Sheria cha Tanganyika.

[94] Mamlaka ya polisi ya Zanzibar imenyesha kuhusika zaidi juu ya suala/jambo hilo, walikiri kwamba baadhi ya matatizo yalishughulikiwa.

[95] Salam za mwaka mpya za Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Benjamin, William Mkapa kwa raia tarehe 31 Desemba, 2003.

akihutubia Bunge na kutamka kwamba serikali itaendelea kushughulikia kwa ukali wahalifu na kwamba nguvu zitatumika, kuacha/kusamehe nguvu dhidi ya wafungwa.

Ukweli kwamba mamlaka ya polisi imejumuisha katika kazi zake za mafunzo habari/taarifa juu ya masuala ya haki za binadamu[96] haitoshi kama haitasaidiwa na utashi wa kutafakari kubadilisha hali iliyopo.

Bodi ya kanuni kwa ulinzi wa watu wote wenye aina yoyote ya kizuizi cha kifungo ya Umoja wa Mataifa inaeleza: "Hakuna mtu aliye kwenye aina yoyote ya kizuizi au kifungo atakayeteswa au kufanyiwa ukatili, unyama au utendaji wa udhalilishaji au adhabu. Hakuna mazingira kwa hali iwayo yote ile yanaweza kusihi kama uhalali kwa mateso au ukatili mwingine unyama au utendewaji wa udhalilishaji au adhabu" (katika kanuni ya 6). Utendaji mbaya wa wafungwa pia inapingana na kifungu cha 7 na 10 cha ICCPR[97] ambayo inalazimisha kufuatwa na Tanzania. Zaidi ya hayo, inapingana na kifungu cha 2 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya mateso, ambayo Tanzania bado haijaridhia.

Kifungu cha M (7) (b) ya miongozo juu ya Haki ya shitaka halali Afrika inasema kwamba "Nchi lazima zihakikishe kwamba hakuna mtu, kisheria ananyang'anywa uhuru wake, kwa uelekeo wa mateso au ukatili, unyama au utendewaji wa udhalishishaji au adhabu". Sehemu (e) inaongeza "hakuna mfungwa wakati anahojiwa atafanyiwa nguvu, atatishiwa au mbinu ya mahojiano, ambayo inadhoofisha uwezo wake wa maamuzi au hukumu yake". Bodi ya Kanuni ya Umoja wa Mataifa inaeleza, "hakuna mtu aliye kwenye aina yoyote ya kizuizi au kifungo iataelekea kuteswa au ukatili, unyama au utendewaji wa udhalilishaji au adhabu. Hakuna mazingira/hali iwayo yote ileinaweza kuruhusu uhalali kwa mateso au ukatili mwingine, unyama au utendewaji wa udhalilsihaji au adhabu" (Kanuni ya 6).

Juu ya suala hilo hilo la nguvu juu ya kukamata, uanzishaji wa mgambo kuzuia uhalifu uhalifu katika mitaa ya miji mingi katika Tanzania na kimya cha mamlaka ya polisi kusimamia na kuzuia vitendo vya nguvu vinavyofanywa na makundi haya ya utaratibu binafsi ni tishio kamili kwa mchakato ufaao wa sheria.

Utendaji huu ulioanzwa na vikundi vya *Sungusungu.* Kundi la kwanza lilianzishwa mwaka 1982 katika mkoa wa Shinyanga na mtu anayejulikana kama Kishosho Man'gombe, "Mrejeshaji wa ngombe". Makundi haya yalianza katika eneo la ng'ombe wengi na lengo lao kuu lilikuwa ni kutoa ulinzi dhidi ya wezi. Aliyeongoza uungaji mkono wa Sungusungu alikuwa Rais Nyerere, mwenyekiti wa kwanza wa Chama Cha Mapinduzi (CCM). Alisema amevutiwa na chanzo cha chini cha makundi hayo na aliyaelezea kama nguvu ya kimapinduzi katika ngazi ya kijiji, ambayo lazima watiwe moyo na haitabughudhiwa. Katika matukio kadhaa, aliombwa kuachiwa kwa watu waliokamatwa wa kundi la Sungusungu kama ilivyo katika maoni yake. "Sheria ambayo kwayo walishitakiwa ilikuwa sheria mbaya kwa sababu ilifanya kazi kinyume na maslahi ya watu na ilikuwa inaunda mgogoro kati ya watu na nchi".[98]

---

[96] Kwa msaada wa pamoja wa kimataifa (UNDP na Kituo cha Haki za Binadamu cha Danish) na cha nchini (Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu) ilishiriki katika uchanganuzi wa kitabu cha kufundishia cha haki za binadamu kinachotumiwa katika shule za polisi.

[97] Kifungu cha 7 "Hakuna yeyote atakuwa na mwelekeo wa kutesa au ukatili, unyama au utendewaji wa udhalilishaji au adhabu".

[98] Angalia Sunday News (Tanzania) ya tarehe 25, Mei mwaka 1986.

Shughuli za makundi haya kwa haraka yaliendelea kuwa mfumo sambamba kwa usimamiaji wa haki, ambayo kwayo haki za msingi hasa hazikujaliwa. Chris Maina Peter alitoa mfano wa Busangi, katika Wilaya ya Kahama, ambapo Sungusungu walianzisha mfumo wao wa mahakama na katalogi ya makosa na ikilinganishwa na adhabu.[99]

Jaji Mwalusanya alieleza kwa undani masharti ya *sheria kwa utendaji wa jeshi la kabila* katika Mkoa wa Mara, na kwa nguvu zote alilaani uanzishaji na mwenendo wa makundi haya: " Wote ambao wanatetea majishi ya makabila lazima waendelee kufanya kazi nje ya utawala wa sheria wangefanya vizuri kutafiti na kubadilisha dhamiri zao juu ya suala/jambo".Alirejelea kwamba "kushuguhulika na wahalifu nje ya taratibu zilizowekwa na makosa kutambuliwa na sheria zetu ni kosa la jinai" na kutupiliwa mbali kwa rufaa za wanajumiya nane wa jeshi ambalo walikata rufaa dhidi ya hatia zao.[100] Wakati ujumbe wa FIDH ulipokuwa nchini kulikuwa na maonyesho ya wasio na makosa na umma Mwanza, ambapo waonyeshaji waliomba serikali kuanzisha tena askari wa kikabila, *Sungusungu.* Katika majibu, Mkuu wa mkoa Njoolay aliahidi kwamba serikali ingefanya kila kinachowezekana kuthibiti makosa yaliyoenea katika mkoa.[101]

Ingawaje huu kama mfumo wa jeshi uliisha mwanzoni mwa mwaka 1990 ilikuwa na matokeo yafaayo katika akili za watu kuvunja maangamizi/uharibufu mkubwa. Imani za watu kwamba wanaweza kuchukua sheria katika mikono yao bado ipo kwa kiwango fulani katika Tanzania. Hili liliwekwa lilifafanuliwa wazi na matukio kadhaa ya umwagaji damu, ambayo yalielezewa katika magazeti ya Tanzania katika miezi ya hivi karibuni kwamba kumeripotiwa mauaji kwa makosa madogo au mashaka yasiyo bayana. Januari mwaka 2003, Abasi Magwizi (mwenye umri wa miaka 47) na Kagembe Saleh (mwenye umri wa miaka 45) waliuawa huko Lushoto na kundi la wenye hasira lenye kati ya watu 200. Waathirika waliuawa juu ya wasiwasi kwamba walihusika katika mauaji ya mtu mwingine. Kabla ya kuwaua, kundi hilo liliwaingilia na kuwavunjia na kuwasha moto makazi yao.[102]

Mwezi Novemba mwaka 2003, watu watatu Mashaka Hassani (mwenye umri wa mwaka 51), Juma Pazia (mwenye umri wa miaka 32) na mtu mwingine ambaye hakutambulika, waliuawa na kundi la watu huko Manispaa ya Tanga juu ya wasiwasituhuma ya kuiibia shule ya msingi Masiwani. Watuhumiwa walipigwa kwa mapanga, rungu, fimbo na mawe na mwisho waliwashwa moto.[103]

Siku moja mwezi Desemba mwaka 2003, ajali mbili zilitokea Dar es Salaam. Watu wawili waliohisiwa kuwa wezi wa gari walipigwa hadi kufa na watu wa eneo la Mbezi, katika Wilaya ya Kinondoni, na mmoja aliyehisiwa kuwa mwizi alipigwa hadi kufa kando kando ya barabara ya Mandazi Msasani.[104] Kwa mujibu wa taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2004 ya LHRC iliyochapishwa baadaye kidogo, haki ya kundi la watu wenye fujo dhidi ya wanaohisiwa uhalifu yanaendelea ingawaje serikali imetoa onyo dhidi yao. Katika mwaka mzima vyombo vya habari

---

[99] Makosa haya yanajumisha wizi wa ng'ombe, unyang'anyi wa barabarani, udanganyifu, wizi wa chakula na nguo, makosa yanayohusishwa na ulevi.

[100] Mahakama Kuu ya Tanzania huko Mwanza, Rufaa ya makosa ya Jinai Na. 72 ya mwaka 1987. katika uungaji mkono wa uamuzi huu aliongeza kuwamba " utetezi wao kwamba walikuwa katika mwendo wa kawaida wa wajibu wao kama maafisa wa amani na kwamba walikuwa wanatekeleza maelekezo ya serikali na chama ilipuuzwa katika jicho ---- Na wote wanaotetea kufanya kazi nje ya utawala wa sheria na hususani kamishina wa wilaya ambayo ni makamanda wa majeshi ya kabila katika wilaya wangefanya vizuri kukumbuka ukweli huu wa kihistoria".

[101] Angalia Mwanza wanashikilia/wana maonyesho ya wasio na makosa. Gazeti la Citizen, la tarehe 15 Oktoba mwaka 2004.

[102] "Mauaji ya kutisha Lushoto" (Horrible killings at Lushoto), Mwananchi ya tarehe 10, Januari mwaka 2003.

[103] Wakazi watatu wa Tanza wameuwawa katika ghasia ya watu" The African, tarehe 17, Novemba mwaka 2003.

[104] Watu wenye hasira waua wezi Dar es Salaam, The Guardian ya tarehe 23 Desemba, 2003.

vimeripoti matukio kadhaa ambayo kwayo ghasia ya watu walikuwa na wasiwasi wa makosa ambao walipigwa mawe, waliuawa kiholela/walinyongwa au kupigwa hadi kufa. Kwenye tarehe 7, Juni, 2004 kwa mfano iliripotiwa kwamba mwanfunzi wa kidato cha pili wa Sekondari ya Nronga katika Wilaya ya Hai, mko wa wa Kilimanjaro, aliyetambuliwa kuwa ni Ismail Tambwe (mwenye umri wa miaka (16) walipiga na mawe hadi kufa na wanaojulikana kama Raia waliokerwa wa mjini Tanga juu ya hisia za kuiba baiskeli na baada ya kufa ilijulikana kwamba alikuwa mwadilifu.

Mamlaka ya polisi huko Zanzibar waliwaambia wajumbe wa FIDH kwamba watuhumiwa aghalabu wanafikishwa kituo cha polisi tayari wakiwa wameumizwa kwa sababu wamepigwa na wanajamii. Chini ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Polisi ya mwaka 1953, Amri ya polisi inaaminika na uhifadhi wa amani, udumishaji wa sheria, amri na kuzuia na upelelezi wa makosa, ukamataji wa ulinzi wa wahalifu na ulinzi wa mali. Sheria hiyo lazima itekelezwe na ulipaji kisasi binafsi hautavumiliwa. Kuboresha utendaji kazi wa mahakama itakuwa njia muafaka katika kuzuia matendo hayo.

### *Uendeshaji Mashtaka ya Watuhumiwa wa Uhalifu*

### a. Muda wa kuwekwa kizuizini kabla ya mashtaka

Mara mtuhumiwa anapopelekwa mbele ya jaji, anasomewa mashtaka na kisha hatua ya uchunguzi inaanza. Mtuhumiwa ambaye kwa sasa ni mshtakiwa anawekwa rumande.

Kutokana na kifungu cha 158 cha Sheria ya Taratibu za Kesi ya Jinai ya mwaka 1985, maombi ya dhamana hayawezi kufanywa kwa mshatakiwa mwenye mashitaka ya mauaji ya kukusudia uhaini na makosa mengine kadhaa. [105]

Kuwepo kwa makosa haya ya uvunjaji wa sheria ambayo kwayo dhamana haitolewi katika Sheria za Tanzania, ni tishio baya katika utaratibu upaswao wa mchakato wa sheria. Masharti haya yanapandikiza ufidhuli wa hatia ya kudhaniwa, na hivyo, kwenda kinyume na Ibara ya 13 (6) (b)[106] na 15 (1)[107] ya Katiba.

Makosa yasiyowekewa dhamana kwa kweli yanaruhusu mashtaka yenye sura ya mashaka, na yanaweza kuwalazimisha wapelelezi wa polisi kutafuta ushahidi utakaosaidia mashtaka kwa njia yoyote ile ili kuhalalisha ukamataji uliokwishafanyika na kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu.
Cha kushangaza ni kuwa suala la kuwepo kwa makosa yasiyowekewa dhamana halijakemewa kwa uzito unaostahili. Katika kesi kati ya *Daudi Peter dhidi ya Jamhuri ya Muungano*[108], Hakimu Mwalusanya alitoa uamuzi kuwa, dhamana kwa mtu aliyeshtakiwa ni haki yake na wala sio

---

[105] Kifungu kidogo cha 148 (5). Afisa polisi aliyepo zamu katika kituo cha polisi au mahakama ambaye mshtakiwa analetwa mbele yake, hataruhusu utoaji wa dhamana iwapo: a) mtu huyo ameshtakiwa kwa kosa la uuaji wa nia au uhaini; b) itaonekana kuwa mshtakiwa hapo awali alishawahi kuhukumiwa kifungo kwa miaka isiyopungua mitatu; c) itaonekana kwamba mshtakiwa alishawahi kupewa dhamana na mahakama na akashindwa kutimiza masharti ya dhamana au alitoroka; d) mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka yanayotuhumiwa kufanywa akiwa amekwisha achiwa kwa dhamana ya Mahakama ya Sheria; e) tendo au matendo yoyote yanayounda kosa ambalo kwalo mshtakiwa anashtakiwa nalo linatokana na shambulio au tishio la kutumia nguvu kwa mtu mwingine, au, anamiliki bunduki au mabomu; f), itaonekana mahakamani kuwa upo umuhimu au ulazima wa mshtakiwa kuwekwa kizuizini kwa usalama wake.

[106] "Hakuna mtu mwenye mashtaka ya makosa ya jinai atachukuliwa kuwa ni mhalifu wa kosa mpaka atakapothibitika kuwa na hatia ya kosa hilo".

[107] "Kila mtu anayo haki ya uhuru na kuishi akiwa yu mtu huru"

[108] Mahakama Kuu ya Tanzania yaliyopo Mwanza, katika kesi mchanganyiko ya jinai kesi namba 80 ya mwaka 1989 (ambayo haikuripotiwa). Mshtakiwa alishtakiwa kwa kosa la wizi wa kutumia nguvu.

upendeleo. Alisisitiza kuwa kifungu cha 148 cha Sheria ya Taratibu za Kesi za Jinai sio suala la kikatiba, kwa kuwa linachukua nafasi ya kanuni ya uadilifu ya mshitakiwa na linaondoa uamuzi wa mahakama katika masuala ya dhamana na kwa kufanya hivyo, inakiuka kanuni ya mgawanyo wa madaraka. Aliendelea kusisitiza kuwa pingamizi katika kuweka dhamana halina budi kuthibitishwa na sababu thabiti na isiwe woga wa mashaka au wasiwasi. Mahakama ya Rufani ilitetea uamuzi huu.[109]

Suala hili lilitokea tena katika kesi ya mauaji ya kukusudia, kwa Anjelina Ojare,[110] wakati Hakimu mkazi alipotoa dhamana, aliposema kuwa kifungu cha 148 (5), (a) cha Sheria ya Taratibu za Kesi ya jinai inakiuka Kifungu cha 13 (6) (b) na cha 15 (1) vya Katiba. Uamuzi huu kisha ulithibitishwa na Jaji wa Mahakama Kuu.

Mkurugenzi wa Uendeshaji mashtaka ya serikali alikata rufaa dhidi ya uamuzi huo, lakini Mahakama ya Rufaa ilikataa kulitangaza suala hili na ikafuta uamuzi wa Mahakama, ikishikilia "kuwa Hakimu wa mashtaka hakuwa na umilisi au mamlaka ya kusikiliza na kufanya maamuzi yanayohusu uwezo wa kikatiba wa kifungu cha 148 (5) (a) cha Sheria ya Taratibu za Kesi ya Jinai iliyoletwa mbele yake. Hilo lilikuwa ni suala la kupeleka rufaa kwenye Mahakama Kuu kwa uamuzi, jambo ambalo halikufanyika. Kushindikana kwa kiwango hicho au kosa hilo kulifanya taratibu za uendeshaji mashauri kwenye Mahakama ya Wilaya kuwa batili".[111]

FIDH inarejelea Ibara ya 9 aya ya 3 ya ICCPR kinachoeleza kwamba "Haitakuwa kanuni kuu kwamba, watu wanayengojea shitaka watawekwa kizuizini, lakini kuachiwa huru kunaweza kutolewa kwa masharti ya kuhudhuria shitaka katika hatua nyingine yoyote ya mashauri ya mahakama, na kuwa mara nyingi atokee siku za utekelezaji wa hukumu". Kwa nyongeza, kanuni ya 39 ya Bodi ya Kanuni ya Umoja wa Mataifa kwa ulinzi wa watu wote walio katika aina yoyote ya uzuizi au kifungo inasema kwamba, "isipokuwa katika kesi maalumu zilizoruhusiwa kwa sheria, mtu aliyefungwa kutokana na kosa la jinai atastahiki, labda mahakama au mamlaka nyingine iamue vinginevyo kwa maslahi ya usimamiaji wa haki, kuachiwa huru kwa mtu ambaye shitaka linasubiri kutategemea hali ambazo zinaweza kuamriwa kulingana na sheria. Mamlaka kama haya itakuwa na ufahamu wa umuhimu wa kifungo chini ya uchunguzi. Uwepo wa makosa yasiyo na dhamana kunakiuka kanuni ya usafihi ya uadilifu na masharti yaliyotajwa juu.

Tume ya haki za binadamu na watu imependekeza kwa nchi wanachama katika azimio la Ougadougou na mpango wa utekelezaji juu ya kuharakisha mahakama na urekebishaji wa adhabu katika Afrika mwaka 2002, kuboresha fursa ya dhamana, kwa kupanua wigo wa uwezo wa polisi wa kutoa dhamana na kuwahusisha wawakilishi wa jamii katika mchakato wa dhamana ili kupunguza muda wanaokaa wafungwa gerezani kusubiri shitaka.

Kushindwa kupata dhamana kumehusika zaidi kwa kutazama muda mrefu wa uchunguzaji wa kesi za jinai katika Tanzania na hali ya vizuizi vya wafungwa kwenye mahabusu.

Wafungwa wawili waliotajwa juu wote walikuwa wametiwa mbaroni Novemba mwaka 1998, lakini kesi zao zilisikilizwa mwaka 2001. Kwa hiyo wote wamekaa mahabusu kama miaka mitatu, kipindi

---

[109] Mkurugenzi wa kuendesha mashtaka ya serikali (DPP) dhidi ya Daudi Peter, katika mahakama ya Rufaa Tanzania, Rufaa ya Jinai namba 28 ya mwaka 1990. Iliripotiwa mwaka 1991 ..... (Katiba) 533.

[110] Mkurugenzi wa uendeshaji na mashtaka ya Serikali dhidi ya Anjelina Ojare, Mahakama ya Rufaa Tanzania, tarehe 24 Machi 1997, Rufaa ya Jinai namba 31 ya 1996.

[111] Hii ni picha dhahiri ya vipengele vinavyopingana na utekelezaji wa Sheria ya Haki na Wajibu wa msingi wa kikatiba ya mwaka 1994, iliyokosolewa na Chris Peter Maria, Human rights in Tanzania uk. 711 na zinazofuatia.

ambacho hakuna hata mmoja kati yao aliyepokea habari yoyote kuhusu maendeleo ya uchunguzi wa kesi zao.

Wafungwa wote watano ambao FIDH iliwatembelea, walithibitisha kwamba, mara tu unapopelekwa gerezani, hawapati kabisa taarifa zozote kuhusiana na kesi zao, mpaka siku wanapopelekwa kwa jaji kwa uchunguzi wa awali, hatua ya lazima kabla ya kusikilizwa mahakama kuu.

Mamlaka ya Polisi ya Muungano iliamua mwaka 2003 kutekeleza utaratibu wa urekebishaji binafsi kupunguza ucheleweshaji katika kukamilisha uchunguzi. Chini ya utaratibu huu uchunguzi unalazimika kuchukua miezi 6 hadi 9 na kisha kuendelea na shitaka badala ya kipindi cha miaka mitatu kinachotumika sasa. Hakuna mamlaka hata moja iliyotemelewa na FIDH iliyoweza kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa sera hii.

FIDH inaweza tu kusifu sera hii, ambayo inaweka bayana uzito wa bunge katika kushughulikia tatizo hili. Hata hivyo kadirio la uhakika zaidi, lipatikanalo kupitia stadi, lingeweza kuwa na ufanisi zaidi katika kushughulikia viporo vya mahakama.

Takwimu za hivi karibuni za serikali kuhusiana na hali hiyo zilipatikana tarehe 1 Aprili mwaka 2003.[112] Kwa kipindi hicho kulikuwa na wafungwa 19117 waliokuwa wanasubiri mashitaka. (Angalia chati nzima katika kiambatisho, sehemu ya 2).

| **Kipindi cha kukaa jela kusubiri shitaka.** | **Idadi ya wafungwa wanaosubiri mashitaka (kwa makosa yote)** | **Idadi ya wanaume wenye mashitaka ya mauaji ya kukusudia miongoni mwao.** | **Idadi ya wanawake wenye mashitaka ya Mauaji ya Kukusudia miongoni mwao.** |
|---|---|---|---|
| Kipindi kati ya miezi 6 na miaka miwili. | 4667 | 2334 | 227 |
| Kipindi kati ya miaka miwili hadi miaka minne. | 2085 | 1633 | 143 |
| | | | |
| Miaka zaidi ya mitano | 1171 | | |
| Miaka zaidi ya kumi | 34 (Wote wana mashitaka ya kukusudia). | | |
| Kutoka miaka nane hadi kumi | 93 (wote wana mashitaka ya kukusudia). | | |

Kwa hali yoyote uchangamani, utata na ugumu wa uchunguzi wa makosa unavyoweza kuwa hakuna kinachoweza kuhalalisha ucheleweshaji mrefu wa kiasi hiki.

[112] Jedwali na. 11 kutoka kwenye hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Omari Ramadhani Mapuri (Mbunge), iliyowasilishwa kwa Wabunge wakati wa kikao cha wabunge cha bajeti mwaka 2003/2004 p. 52
Chat no 11 from the speech of the Minister of Home Affairs, Hon. Omar Ramadhan Mapuri (MP), presented to the Parliament during the Parliament Budget Session 2003/2004, p.52.

Ukweli kwamba kipindi cha kupita miaka 6 ya kizuizi, wafungwa 366 kati ya 368 walishitakiwa kwa makosa ya mauaji ya kukusudia yaliyoelezwa bila kipingamizi chochote cha upendeleo kuelekea kwenye utendewaji wa wahalifu hawa katika mfumo haki wa Tanzania, kwani tayari walishachukuliwa kama wahalifu, kama si kuishi kama watu wafu mara tu wanavyokatiza dirisha la gereza.[113]

Lazima pia ikumbukwe kwamba, hali hii inakiuka viwango vya Haki za Binadamu kitaifa na kimataifa pamoja, hususani kifungu cha 9 (3) cha ICCPR.[114] kanuni ya 11[115] ya Bodi ya Kanuni ya Umoja wa Mataifa ya Ulinzi wa Watu Wote Wenye Uzuizi wa Aina Yeyote au Kifungo, inakiuka Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu, (Ibara ya 7)[116] na Mwongozo wa Afrika kuhusu shitaka halali.[117]

Kwa kuzingatia falsafa ya sheria ya Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa juu ya kifungo kabla ya shitaka, William Schabas alikisia kwamba kadri ya miezi 21, kiwango cha uvumilivu wa kamati kinaanza kutoweka na kwa ujumla inalaani ukiukaji ambao unazidi kiwango hiki kuwa ni mkubwa mno.[118] Kutokana na idadi rasmi iliyotolewa na serikali ya Tanzania, Wafungwa 3256 walioko mahabusu tayari walishakaa kifungoni miezi zaidi ya 24 (Ni kama asilimia 17 ya wafungwa wote, lakini asilimia 41 ya wafungwa hao wameshitakiwa kwa mauaji ya kukusudia), hivyo inajumuisha ukiukaji wa viwango vilivyokubalika vilivyowekwa na Kamati.[119]

**b. Hali ya kizuizi ya wafungwa walioko mahabusu**

Wafungwa walioko mahabusu/kizuizini wanavyotakiwa kutendewa imeelezwa katika sehemu ya XII ya Sheria ya Gereza ya mwaka 1967. Ingawaje wajumbe wa FIDH hawakupata fursa ya kufika vyumba vya mahabusu, walipata maelezo ya kutisha kutoka taasisi dhahiri: Tume ya Tanzania ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, katika ripoti yake maalumu kuhusu hali ya magereza ya Tanzania bara, mwaka 2002/2003.

Katika maelezo ya wafungwa na mahabusu kwa jumla (ukurasa wa 19), Ilielezwa kwamba matandiko yanayotolewa kwa wafungwa hayatoshi na yako katika hali mbaya hususan kipindi cha baridi, hasa Arusha. Sio wafungwa wote wamepewa matandiko yanayotakiwa kwani ni machache na idadi ya wafungwa inazidi mgao.

---

113 Haishangazi kwamba katika kulinganisha hakuna mshitakiwa na aliyekuwa kifungoni kwa kipindi hicho aliyekuwa amekaa zaidi ya mwaka mmoja jela, ingawaje kwa kawaida uhalifu wa kiuchumi unataka uchunguzi changamani sana.

114 Yeyote aliyekamatwa au kufungwa kutokana na mashitaka ya jinai atapelekwa mara moja mbele ya jaji au kwa afisa mwingine aliyeidhinishwa kisheria kutekeleza mamlaka ya mahakama na atastahiki kuendesha mashtaka katika kipindi kifaacho au kumwachia.

115 "Mtu hatawekwa rumande bila kuwa amepewa nafasi ifaayo kusikilizwa kwa ghafla na mahakama au mamlaka nyingine.

116 "Kila mtu atakuwa na haki ya kesi yake kusikilizwa. Hii inajumuisha --- (d) Haki ya kushitakiwa katika muda muafaka kwa mahakama adilifu au baraza.

117 Kifungu N (5) (a). "Kila mtu aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai ana haki ya kushitakiwa pasipo ucheleweshaji usiopasa.

118 William Schabas, katika Uondoaji wa adhabu ya kifo, ukurasa 127. Alitaja kesi ya Everton Morrison dhidi ya Jamaica, ambayo kwayo uchelewaji wa miezi kumi na nane haukuchukuliwa kama usiopasa lakini ulielezwa kama swala lipasalo. Katika kukadiria ucheleweshaji kabla ya shitaka, kamati inapima kipindi cha toka mtu akamatwe mpaka kuanza kwa shitaka.

119 Miongoni mwa wahalifu waliokutwa Zanzibar, watatu kati ya watano walikuwa wamekaa zaidi ya miezi 24 wakisubiri shitaka, na wawili tu ambao hawakukaa kifungo kirefu kabla ya shitaka walikuwa warusi wawili wenye hatia, ambao walifuata kwa kiasi fulani utaratibu usio wa kawaida, kutokana hasa na utaifa wao, na kitendo cha balozi wa Urusi wa wakati huo, ambaye alisisitiza juu wa taharifu ya adhabu zao.

Kurundikana katika vyumba ni suala kubwa la kusikitisha. Uwezo wa magereza 45 yaliyotembelewa na Tume ni ya wafungwa 12,540 tu, lakini kwa kipindi walichotembelewa kulikuwa na wafungwa 26,078 katika magereza haya.

Hata takwimu hizi hazitoshi kueleza hali katika baadhi ya sehemu za jela. Wakati Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Ndugu John Chiligati alipotembelea gereza la Bangwe huko Kigoma, Magharibi ya Tanzania, mwanzoni mwa mwaka 2003, iliripotiwa kwamba alishtushwa na msongamano wa kuzidi kiasi. Uongozi wa gerezani hapo ulimwambia kwamba jela ambayo ina uwezo wa wafungwa 67, ilikuwa na wafungwa 500. Gereza la Sumbawanga lilikuwa na wafungwa 350 ingawaje uwezo wake ni wa wafungwa 92[120]

Hali hii ya hatari inaweza tu kusababisha matokeo ya maafa, kama yale yaliyoripotiwa na afisa mwandamizi wa afya manispaa ya Mbeya ndugu Danford Kamenya, aliyeeleza kwamba, mwaka 2003 jumla ya wafungwa 101 walikufa katika gereza la Ruanda Mbeya kutokana na magonjwa ya kuambukiza na kipigo katika miaka miwili iliyopita.[121]

Idadi ya vifo katika magereza ni ya kutisha na inaongezeka jinsi muda unavyosonga. Uchunguzi wa nyuma unaonyesha kwamba mwaka 1962 wafungwa 28 walikufa (kwenye idadi ya wafungwa 10,108). Mwaka 1972. 74 (kati ya 21,968), na mwaka 1982, 331 (kati ya 33,979). Tarehe 17 Novemba mwaka 2002, katika mkoa wa Mbeya mahabusu watuhumiwa 17 walikufa kwa msongo wa pumzi huko kituo cha polisi Mbarali ikiwa ni matokeo ya msongamano.[122]

Wakili wa mahakama kuu, ndugu Rweyongeza, aliuambia ujumbe wa FIDH juu ya kesi aliyokuwa anaiendesha mwaka 1988, iliyohusisha watuhumiwa kumi ambao walipelekwa gerezani. Wakati shitaka lilipoanza miaka kumi baadaye, sita walikuwa wameshakufa.

Vifo hivi vingi katika vifungo vinasababishwa na magonjwa kama vile kipindupindu, kuhara, kuhara damu, malaria na VVU/UKIMWI, lakini hakuna mashaka kwamba msongamano wa magereza unayafanya kuwa sehemu kamilifu kwa magonjwa ya maambukizo ya mguso.

Pia kumeripotiwa kuwepo kwa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama, tatizo lililopo katika magereza mengi ya bara. Kwa mujibu wa ripoti ya Tume, na kama ilivyoelezwa na mhamasishaji wa haki za binadamu, Ally Saleh huko Zanzibar, wakati FIDH ilipotembelea visiwani; majengo ya gereza yamezeeka na hayakarabatiwi mara kwa mara, ambayo pia yanapelekea mazingira yasiyo ya afya. Ingawaje kuna huduma za afya, kiwango cha huduma hakiridhishi na kinategemea fedha inayopatikana, ambayo kwa kawaida haitoshi.

Katika gereza lililotembelewa na FIDH huko Zanzibar, wafungwa walioko mahabusu walisema kwamba, duka la dawa la gereza limekuwa tupu kwa siku nyingi, na kwamba wamepokea dawa mpya za vidonge kabla ya ujio wa wajumbe wa FIDH. Wafungwa walioko mahabusu wameachwa bila huduma ya dawa kwa muda achilia mbali matatizo ya afya yanayoonekana wazi. Kama ilivyosisitizwa/ilivyowekewa sharti katika kanuni za gereza,[123] ni wafungwa fukara ambao

---

[120] "Hatua moja kuelekea kwenye kuondoa msongamano usiofaa magerezani" iliyopatikana katika mtandao http://allafrica.com/stories/20031220817.html

[121] "Mahabusu 164 wafia gerezani Mbeya kwa kipindi cha miaka miwili" (164 detainees have died in prison in two years), Mwananchi ya tarehe 23 Januari 2003.

[122] LHRC's, Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2002, p.21.

hawajapatikana na hatia watakaopewa mavazi, matandiko na chakula. Hili baadaye liliharibu hali/mazingira.

Kwa nyongeza, kukataa kwa mamlaka ya gereza kuzungumzia suala la VVU/UKIMWI katika magereza kunasababisha kuteketea kwa idadi ya watu walioko gerezani. Kuzuia usambazaji wa VVU miongoni mwa wafungwa baadhi ya asasi zisizo za kiserikali zimetoa mwito kwa serikali kuruhusiwa kusambaza kondomu magerezani. Serikali imekataa mwito huo. Kamishna Mwandamizi wa Gereza la Mkoa wa Morogoro, ndugu Ally Mgalla alijibu kwa kusema kwamba, licha ya nia nzuri ya mashirika katika juhudi ya kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI, kusambazia wafungwa kondomu kungeashiria jamii kwamba wafungwa wanashiriki katika shughuli za kingono miongoni mwao. Alisema, "*Kufanya hivyo ni sawa na kuhalalisha vitu ambavyo havipo katika magereza*"[124]

Hata hivyo ripoti kutoka magerezani zinaonekana kupingana na msimamo wa serikali juu ya shughuli za kingono magerezani. Kwa mfano, mfungwa kijana aliyekuwa mahabusu katika gereza la Segerea Dar es Salaam alimwomba hakimu mkazi David Asajile wa mahakama ya wilaya ya Ilala Dar es Salaam kumuhamisha kwenda jela nyingine kwa sababu wafungwa wenzake wanamlawiti kila usiku.[125] Huko Musoma, mtoto mwingine aliiambia mahakama kwamba siku moja msimamizi alimpiga sana, kama inavyodaiwa eti kwa sababu alikataa kusafisha/kudeki sakafu. Mtoto alisema baadaye kwamba, ukweli ni kwamba "*Alitaka kunilawiti lakini nilikataa. Wanatulawiti kwa nguvu, wakihatarisha maisha yetu kwa UKIMWI.*"[126]

Katika ngazi ya kikanda, kifungu cha 16 cha mkataba wa Afrika kinaeleza kwamba "nchi wanachama katika mkataba uliopo wachukue hatua muhimu kulinda afya za watu wao na kuhakikisha kwamba wanapata huduma za kitibabu wakati wanapoumwa," na Tume ya Afrika inaamini kwamba wajibu wa serikali ni kuzidisha katika kesi ambayo mtu yupo katika usimamizi wake na kwa hiyo mtu fulani ambaye uadilifu na ustawi wake unategemea kabisa kwenye matendo ya mamlaka.[127]

Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Haki za Watu iliridhia azimio juu ya miongozo na Sheria za Makatazo na Uzuiaji wa Mateso/Ukatili, unyama au utendewaji wa udhalilishwaji au adhabu katika Afrika (2002). Azimio lilitaka serikali kuhakikisha sheria hizo zilizo ndani ya ufafanuzi wa mateso kulingana na sheria namba 1 ya makubaliano ya Umoja wa Mataifa dhidi ya mateso ni makosa ndani ya mfumo wa sheria wa taifa.

Tanzania haifuati masharti hayo ya kikanda na kimataifa. Sheria ya Magereza ya mwaka 1967 imenyamaa kuhusu utendewaji mbaya wa wafungwa, ingawaje inayo katika sehemu ya XIV ya

---

[123] Kifungu cha 77 (3) kama raia au mfungwa ambaye hajaonwa na hatia hatoweza kupata huduma ya mavazi, matandiko au chakula, au kama chakula hicho kwa maoni ya afisa aliyeko zamu hakitoshi, mfungwa atapokea mlo wa kawaida, mavazi na matandiko. (4) Hakuna raia au mfungwa ambaye hajaonwa na hatia atapewa au atalazimishwa kuvaa nguo za gereza labda (a) nguo za wafungwa hazitoshi au zimechakaa au ziko katika hali ya uchafu, au (b) nguo ya mfungwa inatakiwa kama kizibiti; na (c) Hawezi kupata nguo nyingine zinazofaa kutoka chanzo kingine chochote.

[124] Ripoti ya Haki za Binadamu ya Tanzania, ya mwaka 2003 Kituo cha Haki za sheria na za Kibinadamu (LHRC), ukurasa 16

[125]Hatua moja kuelekea kwenye kuondoa msongamano usiofaa gerezani iliyopatikana katika mtandao http://allafric.com/stories/20031220817.html

[126]Katika kitabu (msitari, kifungu, ukurasa) kilekile kilichotajwa.

[127]*Mawasiliano 137/94, 139/94, 154/96 na 161/97 International Pen, Mradi wa haki za kikatiba, Interights kwa niaba ya Ken Saro-Wiwa Jr na Chama cha Haki zaRaia dhidi ya Nigeria, aya 112.*

tuhuma ikilinganishwa na magereza, wafungwa pamoja na adhabu mbalimbali. Hali kadhalika, kanuni ya adhabu haibainishi mateso katika vifungu vyake[128].

Mwisho wa hatua ya uchunguzi, mshitakiwa wa kesi ya mauaji ya kukusudia anapelekwa kwa jaji (hakimu mkazi) kwa uchunguzi wa awali, baada ya hapo hakimu ataamua aidha kuthibitisha kesi na kuihamishia mahakama kuu kwa shitaka.

## 2. Hatua za shitaka

Katika Tanzania, wakili wa kisheria kwa mshitakiwa ni haki ya kikatiba na sheria halali. Katiba inadhamini haki ya kusikilizwa kusikokuwa na upendeleo katika kifungu cha 13 (6) (a) [129] na Mahakama Kuu hutoa uamuzi kama sharti hili uwakilishi wa kisheria.

Kifungu cha 310 cha Sheria ya Taratibu za Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985 kinaeleza kwamba, ‘mtu yeyote aliyeshitakiwa mbele ya Mahakama ya Jinai, zaidi kuliko Mahakama ya Mwanzo anaweza kuwa na haki ya kutetewa na wakili wa Mahakama Kuu’.

Kifungu cha 3 cha Sheria ya Msaada wa Kisheria, ya mwaka 1969 kinaeleza kwamba, “palipo na mashauri yoyote yanayoonekana kwa mamlaka idhinishi kwamba yafaa, kwa maslahi ya adili/haki, kwamba mshitakiwa lazima awe na msaada wa kisheria katika maandalizi na ujengaji wa utetezi wake au rufaa, kama kesi itakavyoweza kuwa, na kwamba, uwezo wake hautoshelezi kumwezesha kupata msaada huo, mamlaka idhinishi inaweza kuidhinisha kwamba mshitakiwa anatakiwa kuwa na msaada huo wa kisheria na kwenye cheti hicho kitakachotolewa, msajili ataonyesha ni wapi kitatumika kufanya hivyo, kumpangia wakili mshitakiwa kwa lengo la maandalizi na ujengaji wa utetezi wake au rufaa kama kesi inavyoweza kuwa’.

Utetezi wa kisheria lazima atolewe mapema iwezekanavyo, katika kipindi alichokamatwa au angalau kipindi cha kuhojiwa na polisi. Sheria ya Taratibu za Jinai inatoa msaada huo chini ya kifungu namba 54 (1) kinachoeleza kwamba: “kwa mujibu wa kifungu kidogo, (2), Afisa Polisi kwa maombi ya mtu ambaye yuko kizuizini anahitaji kumtafutia nyenzo zifaazo zinazotolewa kumwezesha kuwasiliana na mwanasheria, ndugu au rafiki kwa uchaguzi wake”.[130]

Hata hivyo kwa hali halisi, inaonekana kwamba ofisa polisi aliye zamu aghalabu anakataa kuruhusu mawasiliano na watu wa nje, ikijumuisha wanasheria. Mfungwa aliyekuwa mahabusu aliyekutwa katika gereza la Zanzibar alisema kwamba, baada ya wiki akiwa kizuizini hakuweza kuwasiliana na yeyote. Hili lilikuwa pia tatizo kwa wafungwa walio wengi waliotembelewa na FIDH. Wakati wafungwa Emmanuel na Geredje walipoletwa kwa mara ya kwanza mbele ya jaji, hawakuwa na uwakili wa kisheria.

---

[128]“Wakati haki na wajibu wa mtu yeyote inakuwa inaukiliwa na mahakama au wakala yeyote atakayekuwa, mtu huyo ataitwa/atapewa haki katika usikilizaji wa haki/usio na upendeleo na katika haki ya kufungua rufaa au sheria rekebishi dhidi ya uamuzi wa mahakama au wa ajenti mwingine aliyehusika.

[129] Haruna s/o Said R., dhidi ya Mahakama Kuu ya Tanzania huko Dodoma, Rufaa ya Jinai Na.10 ya mwaka 1991 (Haijaripotiwa).

[130] Kifungu cha pili kidogo cha sharti kinasema kwamba “Afisa wa Polisi anaweza kukataa ombi chini ya kifungu kidogo (1) kwa utabiri wa nyenzo za mawasiliano na mtu aliye ndugu wa rafiki wa mtu aliye kizuizini, kama afisa polisi anaamini kwenye mazingira yanayofaa kwamba ni muhimu kumkinga mtu aliye kizuizini kutowasiliana na mtu kwa lengo la kulinda: (a) utorokaji wa mshiriki wa mtu aliye kizuizini; au (b) hasara, uharibifu au ugushaji wa ushahidi kuhusiana na kosa”.

Kuna hata kesi za washitakiwa wenye hatia ya mauaji ya kukusudia na waliohukumiwa kifo na jaji wa mahakama kuu ingawaje hawakutetewa na wakili wa kisheria. Huu ni ukiukaji wa wazi wa sheria za ndani na viwango vya kikanda na kimataifa. Kwa mfano, miongoni mwa wafungwa waliokutwa na FIDH huko Zanzibar, wawili kati yao, Emmanuel na Geredje walikuwa wamekata rufaa dhidi ya hatia zao bila msaada wa wakili wa kisheria. Wakati FIDH walipowatembelea, walikuwa wakiandaa mihutasari ya rufaa zao kwa msaada wa walinzi wao wa gereza, hali inayoonekana kuwa ya kawaida, kama ilivyoelezwa na ndugu Mahadi Juma Maalim, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Sheria cha Zanzibar. Utendaji huu unapaswa kushawishi majaji kuonyesha kiasi cha huruma wakati wanaposikiliza kesi.

Emmanuel alimkodi mwanasheria toka mwanzo wa shitaka lake, lakini mwanasheria alimwacha bila ushauri wa kisheria baada ya kutiwa hatiani. Hili ni tokeo la ukweli kwamba, Serikali haitoi wakili mtetezi wakati mshitakiwa si fukara. Hata hivyo, tatizo linaanza wakati mshitakiwa anapokuwa fukara katika hatua za mbeleni za utaratibu. Katika kesi yoyote, yeyote kama Emmanuel ni mstahilifu kwa wakili wa kisheria kwa kuzingatia gharama anazopata. Baadaye alihukumiwa kifo, na kwa maslahi ya adili/haki angefaidika kutokana na msaada ufaao wa kisheria kukata rufaa dhidi ya hatia yake.[131]

FIDH inarejelea aya ya 5 ya Vyombo vya Ulinzi vya UN Inayohakikisha Ulinzi wa Haki za wote wenye adhabu ya kifo inayorejelea "Haki ya kila mmoja anayehisiwa au kushtakiwa kwa kosa ambalo adhabu ya kifo inaweza kulazimika kuwa na msaada wa kisheria ufaao katika hatua zote za mashauri". Ibara ya 14 ya ICCPR pia inahifadhi haki ya wakili wa kisheria.

Miongozo juu ya Haki ya Kesi Isiyo na Upendeleo/Kesi ya Haki na Msaada wa Kisheria katika nchi za Afrika inasema kwamba "Mtu yeyote aliyekamatwa au aliyefungwa atakuwa na fursa ya papohapo ya mwanasheria na labda kama mtu ameisamehe haki hii katika maandishi, hatashurutishwa kujibu maswali yoyote au kushiriki katika mahojiano yoyote bila mwanasheria wake kuwepo. Kifungu namba 2 (a) kinaongeza kwamba "Haki hii inatumika katika hatua zote za kuendesha mashitaka yoyote ya jinai, ikijumuisha mahojiano ya awali ambayo kwayo ushahidi unachukuliwa, kipindi cha usimamizi wa kifungo, mashauri ya mashitaka na rufaa".

### a. Ubora wa huduma ya kutetewa kwa washitakiwa Wasio na uwezo kifedha katika kesi za Mauaji Tanzania

Jaji Mwalusanya alieleza wazi katika kujenga hoja katika kesi ya *Mbushuu* "Hatari ya [kumnyonga mtu asiye na hatia] inatwaa uwiano mkubwa wakati mtu fulani anapozingatia ukweli kwamba watu wengi maskini hawapati wakili wa kisheria mzuri kwani wanapata wanasheria wanatoa maelezo mafupi na yasiyoandaliwa kwa makini kizimbani ambao wanalipwa shilingi 500 tu za Kitanzania. Kutokana na ujira huo mdogo, mawakili wa utetezi hawatumii juhudi za kutosha katika kesi kama hizo"[132]

---

[131] Kanuni na Miongozo kuhusu Haki ya Shitaka Halali/Haki na Msaada wa kisheria katika Afrika unasema kwamba "maslahi ya hakimu lazima yaukiliwe kwa kuzingatia yafuatayo katika swala la makosa ya jinai: (i) uzito wa kosa (11) uzito wa adhabu" Kifungu H (b)). Kwa uzingatiaji wa FIDH, yote ni muhimu sana.

[132] *Jamhuri dhidi ya Mbushuu na Sangula*, TLR (1994) katika 163

Wakati FIDH walipomuuliza Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Jaji Bahati, kama tume ilipanga kutoa mapendekezo juu ya swala hilo, alijibu kwamba, Hakukuwa na ombi rasmi kutoka kwa wanasheria la kutaka marekebisho, Tume isingeweza kufanya uchunguzi wa jambo hilo. FIDH wanaamini kwamba tume lazima izingatie tena nafasi yake juu ya jambo hilo.

Kwa mujibu wa profesa Shaidi ambaye ni wakili, utetezi unaofaa katika kesi inayohusisha shitaka la uuaji wa nia unagharimu kama shilingi za Kitanzania 3,000,000.[133] Hata hivyo, kikomo cha msaada wa kisheria ni shilingi 100,000/= za Kitanzania kwa kesi yote.

Mwanzoni, kiasi kilikuwa cha kudumu cha umasikini wa shilingi 500 katika Sheria ya msaada wa kisheria ya mwaka 1969, na ilibaki katika kiwango hiki cha chini mpaka hivi karibuni, wakati kilipobadilishwa katika Sheria ya Marekebisho Mchanganyiko ya mwaka 2003 hadi shilingi za Kitanzania 100,000/= [134]

Ingawaje hili linadhihirisha juhudi kubwa kutoka serikalini, bado kiwango hicho kiko mbali katika kupunguza pengo kati ya msaada wa kisheria na haki ya kuwakilishwa mahakamani.

Kwa kawaida wanasheria vijana na wasio na uzoefu wanapangiwa kesi hizi, na baadhi wanaweza kushindwa kuendelea kuwashauri wateja wao baada ya kutiwa hatiani, kama ilivyotokea kuhusiana na ndugu Geredje huko Zanzibar.

Ibara ya 5 ya Vyombo vya Ulinzi vya UN kinanukuu "msaada wa kisheria ufaao"[135] na ibara ya 14 ya ICCPR pia inahifadhi haki hiyo miongoni mwa dhamana ya shitaka halali. Katika kesi ya *Reid dhidi ya* Jamaika Tume ya Haki za Binadamu ilichukulia kwamba "mfumo huu, katika muundo wake wa sasa, hauonekani kufanya kazi kwa namna ambayo ingewezesha mfumo wa kuwakilisha wananchi kufanya kazi kulingana na wajibu wa msaada wa kisheria kujitoa wenyewe kwenye kazi na wajibu wao alimradi ni wa kufaa kwa maslahi ya haki. Kamati ilizingatia kwamba katika kesi zinazohusisha hususan adhabu ya kifo, msaada wa kisheria lazima umwezeshe wakili kuandaa utetezi na mteja wake katika hali ambayo itamwezesha kupata haki. Hili linajumuisha masurufu kwa ujira ufaao kwa wanayetoa msaada wa kisheria".

Kifungu H (e) cha Mwongozo kuhusu Haki ya Shitaka la Haki na Msaada wa Kisheria katika nchi za Afrika kinasema kwamba "Wakati msaada wa kisheria unapotolewa na vyombo vya mahakama, mwanasheria aliyeteuliwa … (2) atakuwa na mafunzo muhimu na uzoefu kulingana na asili na ukubwa wa jambo, … (5) kufidiwa kunakoridhisha kutoa motisha na hivyo kutoa uwakili wa kutosha na ufaao kwa mshitakiwa".

---

[133] Takribani Euros 260

[134] Rekebisho hili ni matokeo ya uamuzi wa mahakama ya rufaa ya Tanzania, katika kesi iliyoendeshwa na *Jaji, Mahakama Kuu ya Arusha na Anor dhidi ya N.I.N. Munuo Ng'uni*, ya tarehe 5 Machi mwaka 2002, Wakati majaji walipoamua kwamba ujira wa shilingi mia tano za Kitanzania kwa kutetea kesi kubwa ya jinai kama vile uuaji wa nia kusingeweza kuchukuliwa kuwa na haki na usawa, na kubadilisha kiasi hicho kwa ada mpya ya shilingi za Kitanzania 100,000/=.

[135] "Adhabu ya kifo inaweza tu kutolewa kwa kufuata hukumu ya mwisho kutolewa na mahakama yenye umilisi baada ya mchakato wa kisheria unaotoa ulinzi unaowezekana kuhakikisha shitaka halali, angalao sawa na zile zilizopo kwenye kanuni/ kifungu cha 14 ya Mkataba wa Kimataifa Juu ya Haki za Raia na Haki ya Kisiasa, ikijumuisha haki ya kila mmoja anayehisiwa au kushitakiwa kwa kosa ambalo kwalo adhabu ya kifo inaweza kutolewa kwa msaada wa kisheria wa kutosha katika hatua zote za mashauri".

Kuongezeka kwa ujira wa msaada wa kisheria kungeweza bila shaka kuboresha ubora wa uwakilishi wa kisheria unaotolewa kwa washitakiwa hawa, na matokeo yake, utapelekea uwezekano wa kwamba mshitakiwa alikuwa na shitaka la haki.

**b. Jukumu la kuthibitisha na ushahidi unaokubalika na mahakama**

Hatia ya mshitakiwa inaegemea kwenye uletaji wa ushahidi katika shitaka. Kuonekana na hatia, lazima kuwe kumethibitika bila kuacha shaka yoyote kwamba, mshitakiwa amepatikana na kosa aliloshitakiwa.[136]

Ushahidi utakaotolewa katika shitaka lazima utolewe kulingana na Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1967. Unaweza kuwa muundo wa ushahidi wa mdomo (kifungu cha 61), ushahidi ulioandikwa (Kifungu cha 63), Vitabu vya Benki (kifungu cha 76) na nyaraka za serikali (kifungu cha 83).

Ushahidi wa kimazingira (kwa maana ya ushahidi uliojengwa kwa kutokana na mazingira ya tukio) unatumika katika mahakama kumtia mtu hatiani pamoja na mshitakiwa aliyeshitakiwa kwa kosa la uuaji wa nia. Kwa kufuata kifungu cha 122 cha Sheria ya Ushahidi, "Mahakama inaweza kuhitimisha uwepo wa jambo lolote ambalo inafikiria linaelekea kuwa lilitokea, kwa kuzingatia sababu za kawaida za tukio halisi, tabia ya kibinadamu na shughuli za jumuiya katika kuhusiana kwake na ukweli na kesi hiyo". Dhana hizi ni ngumu kukanusha, kama kifungu cha 5 cha Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1967 kinavyosema kwamba "popote inakotolewa kwa sheria hii au kwa sheria nyingine yoyote iliyopo, mahakama itakisia ukweli au itachukulia kama ukweli huo uliothibitishwa, labda au mpaka jambo lithibitike vinginevyo". Hivyo basi, ushahidi wa kimazingira unaweza kusababisha adhabu ya kifo pasipo ushahidi makini uliojengwa.

Wafungwa wawili wa Kirusi ambao ujumbe wa FIDH ulikutana nao huko Zanzibar walionyesha wasiwasi mkubwa kwa ushahidi uliotolewa dhidi yao, wakionyesha ukweli kwamba, ushahidi wa macho tu uliotolewa na upande wa mashitaka ulijitokeza zaidi ya miezi sita baada ya tukio husika, na alikuwa ni mtoto wa miaka 12. Kwa nyongeza ingawaje baadhi ya mashaka kama ya kusababisha kifo, hakuna uchunguzi sahihi wa mwili uliochukuliwa, mchunguzi anaunda maoni yake kwa kuuangalia mwili pasipo uchunguzi zaidi wa mahakama. Hakuna hata picha ya mwili inayochukuliwa kama ushahidi na kuwasilishwa mahakamani.

Ilielezwa kwa wajumbe wa FIDH na viongozi wa ngazi ya juu ikiwajumuisha ndugu Mapunda, Kamishina Mwandamizi wa Polisi au ndugu Werema, mwendesha mashitaka wa zamani, kwamba hawakuwa na taarifa kwamba watu wasio na hatia wanahukumiwa na mahakama kuu ya Tanzania. Hata hivyo uthibitisho huu umeibusha mashaka makubwa.

Rejelea maneno ya Jaji Mwalusanya, *"Hatari ya kumnyonga mtu asiye na hatia ni kubwa chini ya mfumo wa sasa"*, tena matatizo yanapelekea mashauri katika kila hatua. Kwa nyongeza, kutokukubarika kwa ushahidi uliopatikana kinyume cha sheria haufanyiki pasipo kufikiri, kwani Sheria ya ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai"[137] inasema kwamba "mahakama, kwa hiari yake

---

[136]"Inaonekana kwetu kwamba ujengwaji mzuri juu ya mamlaka kwamba madaraka/wajibu na wajibu wa kuthibitisha kama ilivyo katika mashitaka yote jinai yameegama kwenye uendeshaji mashitaka kujenga kesi zao bila shaka yoyote" *John Nyamhanga Bisare dhidi ya Jamhuri, Mahakama ya rufaa ya Tanzania, Rufaa ya Makosa ya Jinai* namba 29 ya mwaka 1979 TLR (1980), ya 6.

[137]Kifungu cha 169 (1), Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985.

inaweza kutoruhusu ushahidi labda iwe katika kipimo cha mwelekeo, imeridhika kwamba kuukubali ushahidi kungefaidisha maslahi ya umma bila kuleta athari kwa haki na uhuru wa mtu yeyote”[138]

Majaji wanashauriwa kuwa makini kwa “uzito wa kosa wakati wa uchunguzi ambao kwao masharti yanavunjwa, kutokanana umuhimu na ugumu wa upelelezi wa kubaini Kosa la mhalifu na ugumu wa kuhifadhi ushahidi wa jamboambao unapelekea uwezekano wa kukubali ungamo linalopokelewa chini ya matumizi ya nguvu au hata mateso, wakati maslahi ya serikali/umma yanapohitaji hivyo.

Ilielezwa kwa nyongeza chini ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Ushahidi kwamba “Hakuna ungamo litolewalo katika ushahidi litakataliwa kwa msingi kwamba ahadi au tishio lililochukuliwa kutoka kwa mtu anayeungama labda Mahakama iwe na maoni kwamba, kushawishi kulifanywa katika mazingira hayo na yalikuwa katika mtazamo huo kwani yalielekea kusababisha uongo katika kukubali kosa.

Masharti haya hayana chochote lakini utambuzi rasmi wa uletaji wa ushahidi ”kwa namna yoyote muhimu”, haiachi nafasi ya kuharibu utaratibu wa kukusanya ushahidi.

Hili kwa hakika linapingana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya mateso (bado haujaridhiwa na Tanzania), ambayo kwayo Ibara ya 12 inabainisha nchi wanachama kuruhusu uchunguzi wa tuhuma zozote za mateso, na Ibara ya 15 inawalazimisha kuhakikisha kwamba “taarifa yoyote iliyopatikana kwa njia ya mateso zimefanyika kama matokeo ya mateso hai hazitaletwa kama ushahidi katika mashauri yoyote”.

Kwa nyongeza, Maoni ya Jumla 13 ya Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (katika Ibara ya 14 ya ICCPR) kinasema kwamba, sheria lazima ieleze kwamba “Ushahidi unaotolewa kwa mbinu hizi au njia nyingine yoyote ya masharti haukubaliki kabisa” (aya ya 14). Maoni ya Jumla 20 yanafanana na yale Ibara ya 7 ya ICCPR kinachosema pia ni muhimu kwamba “Sheria lazima izuie kukubalika katika mashauri ya mahakama kwa maelezo au maungamo yanayopatikana kutokana na mateso, au njia nyingine zilizokatazwa” (aya ya 12).

Zaidi ya hapo, katika ngazi ya Kikanda, kanuni hii inaelezwa na Miongozo na Hatua za Uzuiaji Mateso, Ukatili, Uonevu usio wa kibinadamu au utendewaji wa udhalilishwaji au Adhabu katika Afrika, kuridhiwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Watu Oktoba mwaka 2002: Nchi zinatakiwa kuhakikisha kuwa kanuni za ushahidi zinatambua ugumu wa kuthibitisha tuhuma za matendo maovu kwa watu waliofungwa” (aya ya 16). Mwisho, Nchi hizo lazima “zihakikishe kwamba kauli zozote/maelezo yoyote yanayopatikana kutokana na mateso, ukatili, uonevu/utendewaji usio wa kibinadamu au matendo ya udhalilishwaji au adhabu hayakubaliki kama ushahidi katika mashauri yoyote” (aya ya 29).

Mwongozo na Kanuni juu ya Haki ya Shitaka la Haki na Msaada wa Kisheria katika Afrika yaliyoridhiwa na Tume mwezi Machi 2003 yanaeleza kwamba “Ushahidi upatikanao kwa njia zisizo za kisheria ambao una ukiukaji mkubwa wa haki za kibinadamu zitambulikanazo kimataifa haziwezi kutumiwa kama ushahidi wa uendeshaji mashitaka dhidi ya mshitakiwa au dhidi ya mtu mwingine yoyote aliyehusishwa katika mashauri, isipokuwa wote waliofanya ukiukaji” (aya ya F (6) (g)).

[138] Kifungu cha 169 (2) (a), Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985.

## c. Rushwa

Rushwa imetapakaa kwa polisi na katika mahakama[139] na kwa hakika inazuia sana mchakato wa sheria upasao[140] hata katika kesi ambazo adhabu ya kifo ipo kwa wadau. Utoaji wa adhabu ya kifo kunaweza kwa hiyo kutokea kwa shitaka lisilo halali.

Kulingana na Ibara ya 6 (2) ya ICCPR, adhabu ya kifo inaweza tu kutolewa kufuatana na sheria "siyo kinyume kwa masharti ya Mkataba uliopo" ikijumuisha haki ya shitaka halali.

Katika kesi ya Reid dhidi ya Jamaika, Kamati ya Haki za Binadamu ya UN iliongeza kwamba "Katika kesi za adhabu ya kifo. Wajibu wa nchi wanachama kuchunguza kwa makini/kwa kufuata sheria dhamana/hakikisho la shitaka halali/haki lililopo katika kifungu cha 14 cha Mkataba kuwa la lazima zaidi" [141]

Mwaka 1996, Rais Benjamini Mkapa alinukuliwa akisema "Kilicho muhimu ni pesa – Wale wenye pesa wanashinda kesi zao"[142] Kauli kama hiyo hivi karibuni ilitolewa na mtu mwingine wa serikali ya Tanzania, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, aliyesema kwamba rushwa ni moja ya matatizo yanayozuia usimamiaji wa haki wa haki katika nchi.[143]

Upungufu wa majaji ni tatizo lingine kubwa, kwani linasababisha uchelewaji katika kusikiliza kesi. Shitaka la Emmanuel na Geredje lilianza mwaka 2001 na walionekana kuwa na hatia mwezi Juni mwaka 2004. Warusi wawili Wafungwa walionana na ujumbe wa FIDH walitakiwa kusubiri kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kutiwa hatiani kabla ya adhabu kutolewa.

Katika Ibara ya 14 (3) (c) ya ICCPR, ni kwamba mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai ana haki "Kusikilizwa/kushitakiwa pasipo uchelewaji usiostahili" Kamati ya Haki za Binadamu ilieleza katika Maoni yake ya Jumla 13 (21) kwamba, "hususani katika kesi za vifo, mshitakiwa atafunguliwa mashtaka na rufaa kusikilizwa pasipo uchelewaji usiopasa, bila kujali matokeo ya uamuzi wa Mahakama.

Kwa nyongeza, FIDH ilishangaa kwamba, majaji watatu wanaamua juu ya kesi za haki za Msingi wakati mmoja anaweza kupitisha adhabu ya kifo. Mahitaji ya majaji watatu katika Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Sheria ya Wajibu ya mwaka 1994, ikizingatia upungufu mkubwa

---

[139] Christina John, Kaimu Mkuu wa Shirika la Uzuiaji wa Rushwa Tanzania wakati alipowasilisha mada katika warsha ya Uzuiaji wa Rushwa iliyofanyika Dar es Salaam tarehe 2 Desemba mwaka 2003, aliporipoti kwamba kati ya Idara zote za Serikali, Polisi wana kiwango kikubwa cha tuhuma za rushwa ukilinganisha na Mahakama na Serikali Kuu. "Polisi waongoza kwa Rushwa" Nipashe ya tarehe 3 Desemba mwaka 2003.

[140] Rushwa kwa mujibu wa taarifa inasemekana kuwa inaongoza katika kufungua majalada ya kesi, kupanga tarehe za kusikiliza kesi, kutafuta majalada ya kesi; matumizi ya hati ya kusitisha utekelezaji wa kusubiri hukumu ya mahakama ya dharura; kupata nakala ya hukumu na mashauri ya koti; utafutaji wa dhamana; kutoa kiambatisho cha maelekezo ya mahakama; maombi ya chumba katika mahakama (kwa ajili ya kusikiliza kesi zisizohitaji kusikilizwa mahakamani) n.k.

[141] Reid dhidi ya Jamaika (no. 250/1987), aya ya 12.2.

[142]Utangulizi wa hotuba ya Rais ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, iliyotolewa katika semina ya majaji na mahakimu wakazi, Ukumbi wa Karimjee Dar es Salaam, tarehe 16 Desemba 1996. Tuliambiwa kama mfano kutoa ruhusa ya dhamana kwa mama Anjeline Ojare, mke wa wakili maarufu wa Mahakama Kuu, ingawaje alishitakiwa kwa kosa lisilokubaliwa dhamana, na wakati dhamana hii ilipotanguliwa, mwendesha mashitaka aliandikisha kufuta mashitaka na kufunga kesi.

[143] Hitimisho lilifanywa na waziri wa Adili/haki na Mambo ya Katiba katika mkutano siku ya Jumamosi tarehe 9, Oktoba 2004, Dar es Salaam. Mkutano ulilaumiwa/shutumiwa kwa ukosefu wa utambuzi juu ya haki za msingi, rushwa, utegemezi wa uhisani na siasa, sababu za kiuchumi na kiteknolojia kama changamoto kikwazo kikuu katika utekelezaji wa marekebisho ya huduma za umma. Taz. The Citizen, ya tarehe 11 Oktoba, 2004.

wa majaji, inaonekana kama mbinu tu. Inaweza kuwa na manufaa zaidi kuwapanga hawa majaji wachache katika mahakama nyingine au katika kesi nyingine zinazosubiri.

Serikali ya Tanzania ina jukumu la kuzingatia jambo hilo na kuongeza idadi ya majaji katika Mahakama Kuu au/na Mahakama ya Rufaa na kesi za jinai hususani kesi za uuaji wa nia isiamuliwe na majaji pungufu ya watatu. Na zaidi, bajeti kwa mfumo wa haki kwa makosa ya jinai lazima iongezeke.

Kulingana na habari zilizopokelewa na FIDH, uchelewaji wa kusikiliza kesi za madai Mahakama Kuu ni mfupi zaidi kuliko ule wa mashauri ya kosa la jinai, ambayo inaweza kuonyesha kwamba kuna zaidi kuliko tatizo la fedha, kuna matatizo mengine zaidi ya fedha, kuna kuachwa kwa maksudi maswala ya haki za kosa la jinai.

Mara tu jaji anaporidhika kwamba hatia imejengwa katika sababu zinazofaa pasipo mashaka, mshitakiwa ana hatia ya kuua kwa kusudio la kufanya uovu, atamhukumu mshitakiwa wa uuaji wa nia na kutangaza adhabu ya kifo.[144]

Wakati mshitakiwa anapopewa adhabu ya kifo, mahakama inamhabarisha juu ya kipindi ambacho rufaa yoyote lazima ifunguliwe. Uwezekano wa kukata rufaa dhidi ya adhabu ya kifo inatolewa lakini kupitiwa tena huwa hakufanyiki ipasavyo. Kama hakuna rufaa iliyofunguliwa na mshitakiwa au na *wakili wake*, Hatia itachukuliwa kuwa imekubaliwa.

Aya ya 6 ya ulinzi vyombo vya ulinzi vya Umoja wa Mataifa inayodhamini ulinzi wa haki za wote wenye hatia ya adhabu ya kifo inasema kwamba “yeyote aliyehukumiwa kifo atakuwa na haki ya kakata rufaa katika mahakama ya mamlaka kuu ya sheria, na hatua lazima zichukuliwe kuhakikisha kwamba rufani hizo zimekuwa za lazima” Utungaji wa sheria Tanzania lazima hatimaye ufuate hitaji hilo.

## 3. Rufani na Msamaha wa Rais

Wafungwa na maafisa wa Magereza mara kwa mara wamewaeleza bayana wachunguzi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Tanzania kwamba haki ya kufungua rufani mara kwa mara inakandamizwa, inadhoofishwa, kutokana na sababu kuu tatu: (i) Mahakama kuchelewa kuwapa wafungwa hukumu zao, na hivyo kuzuia mchakato wa kufungua rufani; wakati mwingine hawapati kabisa hukumu; (ii) Mahakama haipangi tarehe ya kusikiliza rufani, (iii) Wafungwa hawapewi taarifa juu ya maendeleo ya wakati huo ya rufani zao.[145]

Tunarejelea kesi ya Emmanuel na Geredje, wafungwa wa Zanzibar, ambao sasa wanashughulikia rufani zao wenyewe, katika ukiukaji wa taratibu za makosa ya jinai (kifungu cha 310 cha Sheria ya Mwenendowa Makosa ya jinai kimeweka masharti kwamba “mtu yeyote aliyeshtakiwa mbele ya mahakama ya jinai, ukiacha mahakama ya mwanzo anaweza kuwa na haki ya kutetewa na wakili wa mahakama kuu”).

---

[144] Chini ya kanuni ya 314 ya Sheria ya Taratibu za Makosa ya Jinai, kama jaji amemtia hatiani mtu aliyeshitakiwa, au kama amekiri kosa, itakuwa wajibu wa msajili au afisa mwingine wa mahakama kumuuliza kama ana kitu chochote cha kusema kwa nini adhabu isitolewe juu yake kwa mujibu wa sheria, lakini kuachwa hivyo kumuuliza hakutakuwa na matokeo juu ya uhalali/udhibiti wa mashauri. Inaonekana kwamba washitakiwa wanaulizwa mara chache kama wana chochote cha kusema, kama tulivyoambiwa na wafungwa huko Zanzibar.

[145]Taarifa Maalum ya Ukaguzi wa Magereza Tanzania Bara ya Wwaka 2002/2003, Uk. 28.

Bunge pia limerekebisha sheria ya mwaka 1985 ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai hivyo kwamba "hakuna chochote kitakachochukuliwa kuizuia Mahakama Kuu kubadilisha hukumu ya kumwachia huru na kumtia hatiani pale inapochukuliwa ni kwa ajili ya matakwa ya haki", Kupingana na falsafa ya sheria ya sheria iliyopo kwamba, "Mahakama kuu haiwezi kubadilisha hukumu iliyotolewa kwa mhalifu katika zoezi la kutekeleza mamlaka ya marejeo kwa kumwachia huru mtu aliyetuhumiwa".[146]

Hili ndilo jambo liliwapata Warusi wawili walionana na FIDH (rejea maelezo yaliyotangulia) walionekana kuwa na hatia ya kuua bila nia na mahakama kuu, na kuhukumiwa miaka 15 ya kufungwa jela, wakiwa bado kwenye rufaa, mahakama ya rufaa iliwaona kuwa na hatia ya kuua kwa nia na kutangaziwa hukumu ya kifo.

Wakati hukumu inatenguliwa na mahakama ya rufaa, jaji mwongoza kesi alipeleka kwa Rais wa Tanzania nakala ya hati ya ushahidi uliochukuliwa wakati wa mashtaka pamoja na ripoti ya maandishi iliyosainiwa naye ikiwa na pendekezo lolote au uchunguzi juu ya kesi hiyo anayofikiri inafaa kuchukuliwa.[147]

Kuupa utekelezaji uamuzi uliotajwa, Rais angetoa hati ya kifo. Angeweza pia kutoa amri kuhafifishwa adhabu ya kifo au kusamehewa, kwa mkono wake na muhuri wa Jamhuri ya Muungano.[148]

Kwa pamoja Rais Mkapa kwa upande wa Tanzania bara na Rais Karume wa Zanzibar walikataa kutoa hati ya kifo katika miaka kumi iliyopita na wamehafifisha adhabu za vifo kuwa kifungo cha maisha katika fursa mbalimbali.[149]

Chini ya utawala wa Rais Nyerere, idadi maalumu ilitolewa na watu wote walionana na FIDH isipokuwa mmoja ni kwamba alisaini hati mbili za vifo. Hata hivyo, kutokana na maelezo ya ndugu Chipaka, adhabu nyingi za vifo zilitolewa chini ya rais Nyerere. Ndugu Chipaka alifungwa kutoka mwaka 1969 hadi 1980, alikuwa kiongozi wa kuhudumia sehemu za kunyongea za magereza, na hivyo aliweza kushuhudia zaidi ya vifo viwili vya kuning'inizwa ingawaje hawezi kukumbuka ni ngapi zilifanyika miaka hiyo. Alikuwa mtu pekee aliyepinga mtazamo wa viongozi na sera ya Nyerere kuhusiana na hukumu/adhabu ya kifo, lakini kwa sababu ya kupata kwake habari za kwanza kwa wakati huo, tamko/azimio lake lilipinga makubaliano haya kwa nguvu.

Rais wa pili imeripotiwa kwamba alitoa hati nyingi za vifo. Ingawaje kadirio linaonekana kuwa 'zaidi' bila usahihi zaidi wa makini, Jaji Bahati, kaimu jaji wa mahakama kuu, chini ya utawala wa Mwinyi, aliwapa wajumbe wa FIDH kadirio lililo kati ya vifo vya kunyongwa 50 hadi 100. Wakili

---

146 Angalia/ Rejea Wachira Njenga dhidi ya R. (1954), E.A. C.A. 398, walithibitka kaika kesi ya Selemani Rashid na wengine dhidi ya Jamhuri Rufaa ya Jinai Namba. 117 ya mwaka 1975. TLR (1981) 252.

147 Kifungu cha 325 (1), cha Sheria ya Taratibu za Makosa ya Jinai/ Taratibu za Jinai ya mwaka 1985.

148 Msamaha unamaanisha kuachiwa huru kabisa, wakati kuhafifishwa / kupunguziwa adhabu kama mbadala wa kurefusha muda wa kukaa jela.

149 Mwezi April mwaka 2002, Rais Mkapa alipunguza / alihafifisha adhabu ya kifo ya wafungwa 100 kuwa kifungo cha maisha. Kwa mujibu wa Mohamedi Seif Khatibu, Waziri wa Mambo ya Ndani, Rais alifanya hivyo "kuonyesha kuhusika kwake na haki za binadamu, hasa haki ya kuishi. Mmoja wa wahalalifu amekuwa akizubiri katika vyumba vya wanaosubiri kunyongwa kwa miaka 18. Mwaka huohuo Rais Karume alipunguza adhabu ya Warusi wawili waliohukumiwa kufa na mahakama ya rufaa, na pia Mtanzania mmoja, wote waliokutwa katika gereza la Kilimani kati huko Zanzibar. Adhabu zao zilipunguzwa kuwa kifungo cha maisha

Rweyongeza aliwaambia FIDH kwamba wahalifu kadhaa walinyongwa mwaka 1994 kabla ya shitaka la *Mbushuu,*[150] kwani serikali ilikuwa kigeugeu wa hukumu gani ingechukuliwa.

Hakuna hati ya kifo iliyotolewa chini ya rais Mkapa, na anaonekana kufuata sheria hii. Hata hivyo, wahamasishaji wa haki za binadamu wamekatishwa tamaa kwamba, baada ya miaka kumi bunge halijarekebisha ili kubaini aina ya makosa yanayostahili adhabu ya kifo, ingawa ni ukweli kwamba rais Mkapa ameonekana kuunga mkono badiliko wakati walipokuwa rais miaka 1995.

Ni lazima pia kukumbukwa kwamba chini ya sheria ya Tanzania, hafifisho la rais au msamaha ni upendeleo na si haki ya wafungwa walio kwenye orodha ya vifo. Hawawezi kuhusika katika msamaha huo au hafifisho, kwani rais ni yeye peke yake wa kuamua kuchukua uamuzi huo ambayo kwayo hawawezi kuweka pingamizi.

Vyombo vya Ulinzi vya UN vinahifadhi haki ya kila mmoja anayehukumiwa adhabu ya kifo "kuomba msamaha, au kupunguzwa kwa adhabu ya kifo". Msamaha au kupunguziwa adhabu kunaweza kutolewa katika kesi zote za adhabu ya kifo. Kwa nyongeza Mwongozo wa Shitaka haki katika Afrika inaweka sharti kwamba "Mtu yeyote anayeonwa na kosa la jinai ana haki ya kuomba msamaha au kupunguziwa adhabu. Huruma, upunguzaji wa adhabu, au msamaha unaweza kuruhusiwa kwa kesi zote za adhabu ya kifo" (Kifungu N (10) (d). FIDH kwa hiyo inachukulia kwamba sheria za Tanzania lazima zihuishwe ili kuruhusu watu wanaohukumiwa kifo kuomba msamaha wa Rais.

Jaji Mwalusanya anaamini kwamba sheria hii haina mshiko kwa kuwa haitoi madaraka yafaayo dhidi ya utumiaji mbaya wa madaraka wa Rais. Hafungwi/halazimiki na mapendekezo ya jaji aliyetoa hukumu/aliyeadhibu au yale ya Kamati ya Ushauri. Hakuna uangalizi au usimamizi wowote wa lolote katika utekelezaji wa madaraka hayo na uamuzi unategemea haja/wazo la rais na tabia yake".[151] Inaongezewa kwamba, wakati adhabu itakapobadilishwa kuwa kifungo cha maisha, watatolewa kutoka mipaka ya madaraka ya sheria ya mwaka 1994 ya Bodi ya Kifungo cha nje kwa Wafungwa ambayo inatoa utaratibu wa Wizara na taratibu za kuwaachia wafungwa ambao wana stahili chini ya sheria kuachiwa kabla muda wao wa kifungo kufikia mwisho.[152]

Baada ya kuonekana na hatia na kutamkwa hukumu/hukumu, mshitakiwa/mwenye hatia anachukuliwa kwenda gerezani katika sehemu tofauti mahali ambapo atasubiri kunyongwa au kupunguziwa adhabu.

## 4. Hatua inayofuata baada ya kuonekana na Hatia

### *Kusubiri muda mrefu na usiojulikana*

Katika kifungu cha 72 ya Sheria ya Magereza ya mwaka 1967, mfungwa mwenye adhabu ya kifo atatengwa na wafungwa wenzake katika seli au wodi maalumu. Atapewa unifomu tofauti na kusubiri siku ya kunyongwa kwake.

---

[150] Kesi ya Mbushuu

[151] TLR (1994), Uk. 172

[152] 153 Sheria ya Bodi ya Kifungo cha nje kwa wafungwa ya mwaka 1994, sehemu ya 4. Mfungwa nayetumikia adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka 8 au zaidi, atastahiki kifungo cha nje kama: hatumikii kifungo cha maisha, (b) hatumikii adhabu kwa kosa la wizi wa kutumia silaha , hashughuliki na madawa hatari au unajisi, (c) adhabu yake haiwezi kupungwa vinginevyo.

Mwezi wa Aprili mwaka 2003, kulikuwa na wafungwa 370, (wanaume 359 na wanawake 11) waliokuwa wakisubiri kunyongwa katika magereza ya Tanzania bara.[153]

Zanzibar katika kipindi cha mwezi Oktoba mwaka 2004, kulikuwa na wafungwa wawili waliohukumiwa kifo, ingawaje wote wana rufani zao zinazosubiri uamuzi.[154]

FIDH hawakupata fursa ya kufika magereza ya Tanzania bara. Uongozi wa Magereza Makao makuu Dar es Salaam, waliosema kwamba, “Mamlaka ya magereza siyo sehemu inayofaa kujadili na kukampeni dhidi ya adhabu ya kifo, hasa kwa sababu ndiyo watekelezaji kwa mujibu wa sheria”.[155]

Wakati wajumbe wa FIDH walipouliza kama wanaweza kuonana na baadhi ya wakazi waliohukumiwa kifo, Jibu la ndugu N.P. Banzi, Kamishina Mkuu wa Magereza, lilikuwa kwamba, “Ni maoni yangu kwamba zoezi kama hili sio muhimu kwa malengo ya wajumbe. Kuna sehemu nyingi bora katika kampeni zifaazo na za moja kwa moja dhidi ya adhabu ya kifo kuliko ndani ya magereza” [156]

Achilia mbali kufika mara kadha wa kadha makao makuu ya gereza la Dar es Salaam, Ujumbe wa FIDH ulishindwa kukutana na viongozi kujadili suala hilo. FIDH kwa dhati wanasikitikia kile wanachokichukulia kuwa ni ukosefu wa ushirikiano kutoka kwa mamlaka ya Tanzania.

Magereza haya yamekuwa yakitembelewa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Tanzania katika mwaka 2002/ 2003. Ripoti ya mwaka 2002 /2003 ilitaja wafungwa 360, wakati ile ya aprili mwaka 2003 walikuwa 371 kulingana na takwimu rasmi/takwimu za serikali, Hili linaonyesha kwamba mahakama kuu bado zinaendelea kuhukumu watu kifo katika kesi za uuaji kwa nia.

Katika kesi maarufu kuhusu adhabu ya kifo, *Jamhuri dhidi ya Mbushuu na Sangula*, Jaji Mwalusanya alijumuisha maelezo yanayotishia ya hali ya jela kwa wafungwa wanaosubiri kunyongwa: Kutoka kipindi ambacho mtu anahukumiwa kifo, mara moja anawekwa katika sehemu za wanaosubiri kunyongwa akiwa na unifomu ya bluu. Anawekwa sehemu ya peke yake kweli, katika chumba/seli kidogo cha mtu mmoja ambacho ni kidogo kiasi kwamba anaweza kugusa kuta zote kwa kunyoosha mikono yake. Kitu cha kusoma kama kipo, ni biblia au kitabu kingine kinachohusu mambo ya dini. Kila usiku huvuliwa nguo zake zote na kubaki uchi katika chumba/seli chake hadi asubuhi nyingine. Taa katika chumba chake haizimwi na anabaki katika uangalizi wa walinzi. Baadhi ya walinzi wanawaanisi kwa kuwabaka wafungwa, siku zote wakiwakumbusha juu ya majaliwa yao yaliyo karibu na kuwaambia hadidhi za kuogofya kuhusu vifo vya kunyongwa vilivyofanyika vibaya,[157].

Kuhusiana na upatikanaji wa matibabu, Alieleza kwamba yanapatikana kwa wafungwa iwapo tu idara ya magereza ina fedha za kutosha kulipia matibabu yao, kwani hospitali za serikali zinadai malipo kwa matibabu ya wafungwa. Haikumalizika pasipo kusema kwamba fedha hizi aghalabu hukosekana.

---

[153] Chati namba 10 imepatikana katika hotuba ya waziri wa mambo ya ndani, bwana Omar Ramadhan Mapuri (mbunge), iliyowasilishwa mbele ya bunge katika makadirio ya bunge ya mwaka 2003/2004. P.51

[154] Hawa ni Emmanuel na Gereje.

[155] Barua ya tarehe 6 oktoba mwaka 2004, kutoka kwa ndugu A. N. Nanyaro, Kamishina Mkuu/ Msaidizi wa Magereza.

[156]Barua ya tarehe 1 Oktoba 2004

[157]Jamhuri dhidi ya Mbushuu alias Dominic Mnyanje na Kalai Sangula, Mahakama kuu ya Tanzania, kipindi mahakama inaendesha kesi za makosa ya jinai namba 44 ya mwaka 1981, tarehe 22 mwaka 1994, TLR (1994) ukurasa 155.

Alihitimisha kwa kusema kwamba “kwa ufupi” Wafungwa walio kwenye orodha ya kunyongwa wanatendewa kama watu wasio binadamu, ambao haki yao hutendwa kwa kufuata haja ya utawala unaowasimamia katika magereza inayohusika”.

Tunahitaji kusema hapa kwamba hali iliyoshuhudiwa na ujumbe wa FIDH katika gereza la Kilimani kati huko Zanzibar ilikuwa tofauti kabisa. Sehemu za kukaa wafungwa wanaosubiri kunyongwa zimewekwa katika sehemu tofauti ya gereza. Vitanzi vya kunyongea vipo chumba cha kwanza kabla ya varanda. Kulikuwa na vyumba/seli viwili vilivyokuwa na wakazi (Emmanuel na Geredje), wakati sehemu hiyo ina uwezo wa kuwaweka watu sita katika vyumba tofauti. Seli zilikuwa kubwa, safi, na zina magodoro na mashuka, lakini hakuna samani nyingine. Kulikuwa hakuna taa katika seli hizo. Wafungwa waliuambia ujumbe wa FIDH kwamba, wana milo mitatu laini kwa siku, yenye ugali na maharage, na kwamba wana fursa ya huduma za matibabu, ingawaje watoa huduma hiyo walikuwa masikini kwani maduka yalikuwa aghalabu matupu.

Inaonekana kwamba Zanzibar hawajazoea msongamano kama uliopo Tanzania bara, ambao unapelekea matokeo ya chini kuliko itakiwavyo ya kupeleka wenye hatia Zanzibar, Inayosababisha matatizo kwa familia zao kwenda kuwatembelea, kwani ni wachache wanaoweza kugharamia kivuko kuvuka kutoka bara.

Kwa namna yeyote, kuhusiana na hali mbaya katika seli za wanaosubiri kunyongwa ilivyoelezwa katika hukumu ya Mbushuu, mwanasheria wa serikali, Ndugu Mwambe, aliimbia FIDH kwamba, Wafungwa wanatendewa kulingana na na nini uchumi wa Tanzania unaweza kugharamia.

Hoja hii ilikataliwa na Kamati ya Haki za Binadamu ya UN, ambao walilichukulia kama hoja isiyofaa kwa kweli, kamati imeweka sheria za kiwango cha chini cha utendewaji wa wafungwa[158] kama alama teule katika utekelezaji wa kanuni/kifungu cha10 ya ICCPR.

Kwa kamati, haya ni mahitaji ya kiwango cha chini/cha kuanzia ambayo kamati iliyafikiria kuwa ya lazima wakati wote, hata kama uchumi au hali ya bajeti inaweza kufanya masharti haya kuwa magumu.[159]

FIDH inafikiria kwamba Tanzania lazima irasimishe kwa vitendo/hasa kipindi juu ya unyongaji kwa kuridhia sheria halali ya kipindi kinachoruhusiwa na sheria kucheleweshа utekelezaji hivyo kufikia mwisho kwa ukosaji na hakika/mashaka ya wafungwa wanaosubiri kifo. Hili litachukuliwa kama hatua za kwanza kufikia ukomeshaji, ambayo lazima ibaki kama lengo la msingi.

Kwa mtazamo wa ndugu Francis Stolla mwenyekiti wa Kamati ya Haki za Binadamu wa Chama cha sheria cha Tanganyika, wenye hatia wanaweza kutarajia kupunguziwa adhabu na rais wa Tanzania baada ya miaka mitano ya kukaa kizuizini kwenye vyumba vya wanaosubiri kunyongwa. Lakini, hakuna sheria iliyo wazi na ya serikali. Hata hivyo, kizuizi hiki cha muda mrefu kinachounganishwa na kukosa hakika ya wafungwa walio katika orodha ya kuuawa juu ya majaliwa yao inaweza kuhesabiwa utendewaji usio wa kibinadamu, Kinyume na Ibara ya 7 ya ICCPR na ya 13 (6) (e) ya Katiba ya Tanzania.

---

[158]Azimio la ESC. 663 C (XXIV), 2076 (LXII)

[159]Mukong dhidi ya Cameruni (Na. 458/1991), UN Doc. CCPR/C/JI/D/458/1991, aya 9.3; Potter dhidi ya Nyuzilandi Zealand (Na. 632/1995), UN Doc. CCPR/C/60/D/632/1995, aya ya 6.3

Wafungwa walionana na FIDH walikuwa kwa hakika wanaishi katika uchungu kuhusiana na hatma yao. Warusi wawili walikiri kuwa waoga kuanzisha hatua nyingine yeyote ya kisheria, kwani wanaogopa kwamba taharifu inaweza kufutwa na adhabu ya kuuawa kuthibitishwa. Wakazi walio katika vyumba vya wanaosubiri kunyongwa katika jela ya Maweni walitoa hoja inayofanana na hiyo kwa wachunguzi wa Tume ya Haki za Binadamu, wakakiri kwamba, wamepata mateso ya kisaikolojia kwa kuwekwa katika vyumba/seli za wanaosubiri kunyongwa kwa muda mrefu bila kujua ni lini, au kama, watauawa.[160]

Kwa ujumla, wafungwa wote walionana na FIDH, wawe wakazi waliopo kwenye vyumba za wanaosubiri kunyongwa au wafungwa walioko mahabusu waliokutwa gereza la Kilimani kati, walielezea hofu ya kudumu kuhusu majaliwa yao. Wanaishi katika mtengo kamili bila kujua nini kitawatokea na jinsi kesi zao zinavyoendelea.

Kila mtu anaonekana kukubaliana na ukweli kwamba hali ya magereza za Tanzania ni mbaya, lakini utashi na fedha za kurekebisha hali hii zinakosekana.

### *Unyongaji wenyewe*

Ingawaje unyongwaji haujafanywa hivi karibuni katika magereza ya Tanzania, masharti yanabaki katika kifungu cha 25 cha kanuni ya adhabu, "adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa kisheria na mahakama: (1) Kifo; (2) Kifungo (3) adhabu ya viboko;… " imesemwa katika kifungu cha 26 kwamba "wakati mtu yeyote atakapohukumiwa adhabu ya kuuawa, adhabu itaelekeza kwamba atauwawa kwa kuning'inizwa."

Jaji Mwalusanya alitoa maelezo ya kuogofya ya unyongaji uliofanywa siku za nyuma: mfungwa hudondoka kupitia mlango wa sakafuni/darini, kwa hatua nane na nusu akiwa na kamba kuzunguka shingo yake. Lengo ni kuvunja shingo yake hivyo kwamba afe mapema/kwa haraka. Urefu wa angukounategemea vitu kama vile uzito wa mwili na mifupa au unene wa shingo ya mfungwa. Kama mnyongaji amekosea na mfungwa akaanguka mbali, shingo ya mfungwa inaweza kukatika kabisa na kichwa au uso wake unaweza kuchanika: Kama anguko ni fupi sana hivyo kwamba shingo haitakatika lakini badala yake mfungwa atakufa kwa msongo wa kunyongwa. Kuna kesi nyingi zilizonukuliwa za kuning'inizwa kulikoborongwa katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania. Kuna kesi chache ambazo kuning'inizwa kulileta purukushani na mlinzi wa gereza alitakiwa kuvuta mguu wa mfungwa ili kuharakisha kifo chake au kutumia nyundo kugongwa kichwa chake. Shoku katika mfumo inasababisha mfungwa kukosa kujitawala hisia zake za huruma na kujizika mwenyewe. Kwa ufupi, mchakato mzima ni dhali kuwa ni wa kudhalilisha.[161]

Ndugu Chipaka aliwapa wajumbe maono yake juu ya mchakato huo. Aliwaambia namna, asubuhi, wafungwa walivyochukuliwa kwa afisa wa zamu, ambaye alitangaza adhabu, baada ya hapo alifungwa pingu kupelekwa sehemu ya kupumzikia, mahali ambapo alikaa kwa siku yote hadi usiku. Alinyongwa siku iliyofuatia asubuhi, majira ya 1.30 asubuhi. Alisema kwamba, kila mtu alijua kwamba unyongaji umefanyika katika gereza, kwani maafisa waliokuwa zamu walisaidiwa na wafungwa, na siku zote hizo, "wingu jeusi" lilikuwa likitokea mbele ya gereza.

Kanuni inayozuia mateso na utendewaji usio wa kibinadamu pia inahusika katika utaratibu wa unyongaji. Maoni ya Jumla 20 (44), Kamati ya Haki za Binadamu ilibaini. "Wakati adhabu ya kifo

---

[160]Taarifa Maalum ya ukaguzi wa Magereza ya Tanzania Bara 2002/ 2003, Uk.28.

[161]TLR (1994), Uk. 152

inapotimizwa na chama cha serikali kwa makosa makubwa ya jinai, isiwe lazima ilazimishwe kuendana na kifungu namba 6 lakini ni lazima ufanyike kwa namna ambayo itasababishia mateso kidogo ya mwili na akili". Sharti hilo limejumuishwa katika Vyombo vya ulinzi "mahali adhabu ya kifo inapotokea, zifanyike kwa namna ambayo itasabbaisha mateso kidogo" kiasi kinachowezekana vya Umoja wa Mataifa vya kulinda haki za wale wenye adhabu ya kifo, kifungu cha 9 kinachoeleza "mahali adhabu ya kifo inapotokea, zifanyike kwa namna ambayo itasababisha mateso kidogo"kiasi kinachowezekana.

Jaji Mwalusanya alisema kwamba, mchakato wa unyongaji kwa kuning'iniza hasa ni wa kuogofya, kwa ujumla ni dhalili/duni, unaodhalilisha na kwa ujumla ni katili, na inakiuka Ibara ya 13 (6) (e) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.[162]

## VI. Harakati kuelekea kwenye ukomeshaji wa Adhabu ya Kifo

Miaka kumi baada ya kuendesha kesi ya Mbushuu iliyoanzisha hoja kwamba adhabu ya kifo ilikuwa katili/dhalimu na utendevu kinyume cha haki za binadamu, na miaka tisa baada ya uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi Tanzania mwaka 1995, uliopelekea rais Mkapa kupewa madaraka (amekuwa akikataa mara zote kusaini hati ya idhini ya kunyonga), FIDH ilitegema kukuta nchi pia imesonga mbele katika hatua za kufuta adhabu hiyo. Inaonekana kwamba itachukuwa muda kabla ya kufikia hali hiyo.

Watu wengi kupita kiasi walionana na wajumbe wa FIDH walitamka wenyewe kutoafiki utekelezaji wa adhabu ya kifo. Hata hivyo njia wanazochukua kwa kawaida wanapotenda kulingana na cheo rasmi ni sawa: Hatuwezi kuondoa hii adhabu, kwani nchi nzima haiko tayari kufanya hivyo.

Kama mfano, wakati wa mdahalo uliandaliwa kwenye siku ya dunia dhidi ya adhabu ya kifo (tarehe 10 Oktoba 2004) wazungumzaji wote isipokuwa wawili walionekana kuunga mkono uondoaji wa adhabu ya kifo. Wawakilishi wa Vyama vya upinzani, wanafunzi wa shule mbalimbali na wengine, wote waliomba/walitaka ifutwe.

Hata hivyo, asubuhi siku iliyofuata, kulikuwa na kichwa cha habari katika gazeti la *Daily Times*, wino mweusi "Usifanye haraka kufuta adhabu ya kifo," ikinukuu sentensi ya Jaji Kiongozi Amiri Manento alivyosema "Utamaduni wa Tanzania haufanani na wa nchi za nje"[163] Kwa kweli, Jaji Manento huyo huyo alitoa mwito wa kufanyika utafiti kabla ya kuamua juu ya ama waondoe adhabu ya kifo.

Lazima ifahamike kwamba utafiti ulifanyika miaka 13 iliyopita na tume ya Nyalali. Tume hii, iliyoundwa mwaka 1991, ilikuwa chini ya uenyekiti wa Jaji Mkuu wa Tanzania, mheshimiwa Ndugu jaji Francis L. Nyalali. Ilipata wajumbe kutoka chama kinachoongoza, serikali na sekta binafsi kutoka Tanzania bara na Zanzibar na ilihitimisha kwamba adhabu ya kifo lazima iondolewe. Maelezo ya tume yalikuwa muafaka hasa na yalifikia hitimisho kwamba adhabu ya kifo ilikuwa katili, isiyo ya kibinadamu na adhabu inayodhalilisha. Pia walihitimisha kwamba sheria kadhaa

[162]TLR (1994), Uk. 146

[163] "Usiondoe adhabu ya kifo kwa haraka", Daily Times, ya Jumanne tarehe 12 mwezi Oktoba mwaka 2004.

lazima ziondolewe (hasa Sheria ya kuondosha nchini[164] Sheria ya kizuizini) lakini hakuna pendekezo hata moja kati ya mapendekezo haya lililotekelezwa.

Miaka 13 baada ya tume kutoa mahitimisho yake na miaka 10 baada ya hukumu ya Mbushuu, isingechukua muda mrefu kabla ya kufanya uamuzi wa haraka kuondoa adhabu ya kifo.
Hakuna kilichofanywa na mamlaka katika kuhamasisha umma juu ya swala la uondoaji wa adhabu ya kifo miaka 10 iliyopita. Badala yake, unyongaji, wakati unapofanywa, unafanyika kwa siri, na hakuna habari iliyotolewa kuhusu mchakato huo halisi, wala juu ya hali ya kuteseka kifungoni.

Kama wajumbe wa tume ya Nyalali walikuwa wanaunga mkono uondoaji wa adhabu ya kifo kwa sababu ya tabia ya kuogofya ya adhabu hiyo, hakuna sababu kushikilia kwamba raia wa nchi wangeweza kuonyesha hisia tofauti. Kama ilivyoelezwa na Jaji Mwalusanya, "Serikali lazima ichukue jukumu kuhakikisha kwamba raia wamewekwa katika nafasi ambayo wataweza kutoa maoni yao juu ya adhabu ya kifo kimantiki na tathimini sahihi".

Ni jukumu lake kwa raia wake, lakini pia wajibu wao chini ya vyombo vya kimataifa vilivyoidhinishwa na serikali: Tanzania lazima iondoe adhabu ya kifo. Kama ilivyoelezwa katika Maoni ya Jumla 20 (44) Ibara ya 6 ya ICCPR kinarejelea kwa jumla uondoaji wa adhabu ya kifo katika hali ambayo inashauri kwa nguvu kwamba uondoaji unatakiwa. Ni jukumu la chama cha serikali kujishughulisha katika ukamilishaji wa azima/lengo hili. Ilitamkwa tena hivi karibuni katika azimio la 2004/ 67 la Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu.

FIDH inashawishika kwamba watu wa Tanzania wanachohitaji zaidi ni mfumo wa haki usio na upendeleo unaolenga kumtia mbaroni mhalifu na kuwapa adhabu inayofaa wahalifu katika hali ya ubinadamu. Katika jamii huru na yenye amani hakuna nafasi kwa ukatili wa adhabu ya kifo.

---

[164]Tume ya Afrika hivi karibuni ilishutumu /ilitangaza/ilikana sharti kama hilo katika sheria za Zambia. Rejea Shirika la Kutetea wafungwa duniani dhidi ya Zambia, Comm. 212/98. "Mahakama pia ilishindwa kutoa uamuzi/ kuamua juu ya sababu iliyodaiwa kwa kuondosha nchini, yaani, kwamba uwepo wake ilikuwa inaelekea "kuhatarisha amani na utaratibu mzuri huko Zambia…."
Hapakuwa na uchunguzi wa mahakama kwa vigezo vya kisheria na katika kutoa haki kwa kuegemea 'hoja' hii ya Waziri wa mambo ya ndani kwa hatua zilizochukuliwa …. Kiasi kwamba siyo Banda wala Chinula walipewa sababu kwa hatua zilizochukuliwa dhidi yao, kwa maana kwamba haki ya kupata habari ilikataliwa kwao (Kifungu cha 9 (1)"

## Mapendekezo

FIDH na LHRC wameunda mapendekezo yafuatayo **kwa Serikali ya Tanzania**:

Juu ya adhabu ya kifo na viboko

- Kuridhia sheria ya muda juu ya adhabu ya kifo kama hatua ya awali kuelekea kwenye ukomeshaji.
- Kuondoa aina zote za adhabu za viboko
- Kutengeneza takwimu za serikali juu ya adhabu za viboko na juu ya idadi ya adhabu za vifo kwa kila mwaka
- Kuweka katika sheria ulazima wa kukata rufaa (au kufanyia marejeo) ya hukumu ya adhabu ya kifo.
- Kufanya mpango wa uhamasishaji wa umma juu ya umuhimu wa kuondoa adhabu ya kifo.

Mapendekezo ya jumla

- Kushirikisha vyombo vya kimataifa vya haki za kibinadamu vilivyoidhinishwa na Tanzania katika utungaji wa sheria za ndani.
- Kushirikiana na taasisi Umoja wa Mataifa kwa kupeleka taarifa za serikali yake na kutekeleza mapendekezo ya mkataba.
- Kutoa mapendekezo ya usimamiaji wa wahusika kwa Umoja wa Mataifa.
- Kuridhia Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Ukatili.

Juu ya Usimamiaji wa Makosa ya Jinai

- Kuwa na mpango wa uteteaji na utambuzi kuhusiana na rushwa katika mahakama na kuweka mbinu za kuondoa rushwa.
- Kuteua majaji zaidi na kuongeza idadi ya majaji katika mahakama kuu au/na mahakama ya rufaa ili kupunguza viporo vinavyosubiri majaji.
- Kwa jumla zaidi, bajeti kwa mfumo haki wa makosa ya jinai lazima iongezwe.
- Kushurutisha wajibu kupeleka wafungwa walioko mahabusu kwa jaji katika muda uliotengwa kisheria kwa kutamka ubatilishaji wa utaratibu wowote utakaokiuka sharti hilo.
- Kuwaachia huru wafungwa walioko mahabusu ikiwa uchunguzi haujakamilika katika muda ulioainishwa kisheria.
- Kuongeza ada ya wanasheria wanaotoa msaada kisheria wa bure .
- Kuhakikisha kwamba, katika kesi za jinai, watuhumiwa mara zote wanasaidiwa na mwanasheria na kuahirisha usikilizaji kama itakuwa vinginevyo kumchagua mwingine mara moja.
- Kuruhusu maombi ya msaada wa kisheria kufanyika ndani ya mchakato wa kisheria, kumwezesha mtu ambaye amekuwa fukara kwa kumlipa ada ya kisheria kupata bure msaada wa kisheria.
- Kurekebisha sheria kuruhusu uwezekano wa dhamana kwa makosa yote.

Juu ya hali ya Mahabusu/ Magereza

- Kuleta mabadiliko katika magereza ilikuwa hali inayoendana na ya viwango vinavyohusika vya haki za binadamu duniani, ikijumuisha vifaa vya msingi na huduma ya afya, kwa

kuongeza bajeti inayohusika na uzuiaji wa vitendo viovu / vibaya na utumiaji wa nguvu dhidi ya wafungwa.

- Huduma ya afya lazima iwepo kwa wafungwa wote walioko mahabusu.
- Kuruhusu asasi zisizo za kiserikali kutembelea magereza ikijumuisha vyumba vya wanaosubiri kunyongwa.
- Kuandaa takwimu za serikali juu ya vifo katika mahabusu/ magereza.

FIDH na LHRC pia wanazingatia kwamba, Tume ya Kurekebisha Sheria lazima wachunguze swala la kuboresha mfumo wa msaada wa kisheria.

# VII. Marejeo

Chipeta B.D, Criminal law and Procedure. A digest of cases lecture notes. Sahara Communications and Publishing, Tanzania (Mwanza), 1994

Chirs Maina Peter, Human rights in Tanzania: Selected cases and Materials, Koln: Rüdiger Köppe Verlag, 1997

Cohen-Jonathan et Schabas (dir.), La peine capitale et le droit international des Droits de I'homme, Editions Panthéon-Assas, Paris, 2003

Eteka Yemet Valère, La Charte africaine des droits de I'homme et des peuples, L'harmattan

Ouguergouz Fatsah, La Charte africaine des droits de I'homme et des peuples, Editions PUF

William A. Schabas, The abolition of the death penalty in international law, Cambridge university press, 2nd Edition, Cambridge, 2002

Sudre F., Droit international et européen des droits de I'homme, Paris, PUF, coll. Droit fondamental

# VIII. Kiambatisho

## 1. Watu  kutana na Tume

*Tanzania Bara:*

Richard Shilamba, Mratibu wa SAHRINGON - Tanzania, Mtandao wa asasi isiyo ya kiserikali ya haki za binadamu ya Afrika ya Kusini.
Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
Profesa L.P. Shaidi, wakili, Mratibu wa Somo la Makosa ya Jinai wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Ndugu Rweyongeza, wakili (mtetezi wa utetezi katika kesi ya *Mbushuu*)
Bi Anita Samuel Moshi, Katibu Mtendaji, Chama cha Sheria cha Tanganyika.
Ndugu Francis Stolla, Mwenyekiti, Kamati ya Haki za Binadamu ya Chama cha Sheria cha Tanganyika.
Ndugu Israel Magesa, Mwenyekiti, Shirika la Kutetea Haki za Wafungwa Duniani, Kitengo cha Tanzania.
Ndugu Francis Machulan, Katibu wa Kudumu, Shirika la Kutetea Haki za Wafungwa Duniani, Kitengo cha Tanzania.
Ndugu Elias M. Munganda, Mkaguzi wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani.
S A Mapunda, Kamishina wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani.
Ndugu Lukula FG, Mkaguzi wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani.
Ndugu Lifa Chipaka, Rais/ Mwenyekiti, TADEA (Chama cha Siasa)
Katibu wa TADEA
Jaji Bahati, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.
Ndugu Frederick Werema, Mkurugenzi wa Mambo ya Katiba na Haki za Binadamu, Wizara ya Haki na Mambo ya Katiba
Ndugu Shaidi, Mkurugenzi mwendesha mashtaka wa serikali, Wizara ya Haki na Mambo ya Katiba.
Wawakilishi wa Siasa waliohudhuria mdahalo ulioratibiwa na Shirika la Kutetea Haki za Wafungwa Duniani, Kitengo cha Tanzania Siku ya Dunia dhidi ya Adhabu ya kifo (tarehe 10 Oktoba 2004).
James Mapalala (Chausta), Lifa Chipaka (Tadea), Christopher Mtikila (DP), Dr. E. J E. Makaidi (NLD), Amiri Rubbea (CUF).

Ujumbe wa EU na Tume Kuu ya Uingereza, Dar es Salaam, mawasiliano ya simu yalifanywa, lakini hakukuwepo uwezekano wa kupanga siku ya mkutano.

Ujumbe wa FIDH ulikataliwa kukutana na Mamlaka ya Magereza ya Tanzania Bara, Dar es Salaam, na Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Dar es Salaam, ijapokuwa waliwafuata mara kwa mara ikiwa ni pamoja na kutuma maswali hata hivyo hayakujibiwa.

*Zanzibar:*

Ndugu Kinyogo, Msaidizi Mwandamizi wa Kamishina wa Polisi, Zanzibar.
Ndugu Simba, Kamishina Msaidizi wa Polisi (Uhusiano)
Kamishina Mwandamizi wa Polisi (Shule ya Mafunzo ya Polisi)
Kamishina Mwandamizi wa Polisi (Uchunguzi )

Ndugu Omar O. Makungu, Katibu Mkuu (Mambo ya Katiba na Utawala bora na Naibu Mwanasheria Mkuu serikali ya Zanzibar

Ndugu Ally Saleh, mwandishi wa makara wa BBC Zanzibar, Katibu Mtendaji wa Chama cha Haki za binadamu Zanzibar.

Ndugu A. O. Bai, Kamishina Msaidizi wa Magereza, Zanzibar.

Ndugu Mahadi Juma Maalim, makamu mwenyekiti wa chama cha Sheria cha Zanzibar ambaye pia mchambuzi wa programu ( UNDP)

Wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo katika gereza la Kilimani kati huko Zanzibar . Emanuel na Geredje (walihukumiwa kifo, walikata rufaa katika mahakama ya rufaa ya Tanzania, katika mahakama kuu ya Zanzibar, rufani zao zinasubiri uamuzi) na Warusi wawili wenye hatia (adhabu zao zilipunguzwa kuwa kifungo cha maisha).

## 2. Jedwari

**Jedwari 1: Idadi ya mahabusu waliona katika magereza Tanzania bara wanaongojea mashtaka/kusikilizwa na muda waliokaa gerezani.**

| **Idadi ya mahabusu waliona katika magereza za Tanzania bara wanaongoja mashtaka/ kusikilizwa na muda waliokaa gerezani. Kutoka kwa mheshimiwa Omar Ramadhani Mapuri (Mbunge), Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani aliyotoa Bungeni wakati wa kikao cha Bajeti ya Bunge 2003/2004, uk.52** | | | |
|---|---|---|---|
| Muda waliokaa gerezani | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Chini ya miezi miwili | 538 | 33 | 571 |
| Miezi 2 – 6 | 952 | 93 | 1045 |
| Miezi 6 hadi miaka 2 | 2334 | 227 | 2561 |
| Miaka 2 – 4 | 1633 | 143 | 1776 |
| Miaka 4 – 6 | 684 | 68 | 752 |
| Miaka 6 – 8 | 239 | 19 | 258 |
| Miaka 8 – 10 | 83 | 10 | 93 |
| Miaka 10 | 31 | 3 | 34 |
| **Jumla** | **6494** | **596** | **7090** |

**Jedwari 2: Wafungwa wanaosubiri kunyongwa katika magereza za Tanzania bara**

| **Wafungwa wanaosubiri kunyongwa katika magereza za Tanzania bara (kutoka Taarifa Maalum ya Ukaguzi wa Magereza ya Tanzania bara 2002/ 2003) , Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania.** | | |
|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake |
| Gereza la Maweni | 73 | |
| Gereza la Butimba | 55 | 4 |
| Gereza la Isanga | 132 | 6 |
| Gereza la Morogoro | 7 | |
| Gereza la Uyui | 18 | |
| Gereza la Lilungu | 4 | |
| Gereza la Ukonga | 61 | |
| **Jumla** | **350** | **10** |

fidh
International Federation for Human Rights

7 passage de la Main d'Or -75011 Paris
Tel: (33-1) 43 55 25 18/ Fax :(33-1) 43 55 18 80
**E-mail: fidh@fidh.org/ Internet site: http://www.fidh.org**

**Shirikisho la Kimataifa Juu ya Haki za Binadamu** [International Federation for Human Righs (FIDH)] ni Shirikisho lisilo la Kiserikali lililopo kwa ajili ya utetezi Haki za Binadamu kama zilivyoainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948. Lilianzishwa mwaka 1922, FIDH linaunganisha pamoja mashirika 141 ya Haki za Binadamu kutoka nchi 100. FIDH imeshaunda Tume za uchunguzi zaidi ya elfu moja majaribio ya uchunguzi na mafunzo katika nchi zaidi ya mia moja. Inawapatia mtandao wa kitaalam usio na kifnai na mshikamano, na mungozo wenye taratibu za mashirika ya kimataifa.
FIDHI inafanya kazi ya;

(a) Kuhamasisha Jumuiza za Kimataifa.
(b) Kuzuia vurugu, kuua, kuunga mkono vyama vya kiraia.
(c) Kuchunguza na kutoa tahadhari.
(d) Taarifu, shutumu/kana na Linda.

Kihistoria FIDH ni shirika la kwanza la kimataifa la haki za binadamu lililipea mamlaka ya kiulimwengu kutetea haki zote za binadamu. FIDH lina hadhi ya uchunguzi katika Baraza la Uchumu na Jamii la Umoja wa Mataifa [United Nations Economic and Social Council (UNESCO)], Kamati ya Kudumu ya Baraza la Ulaya [Europe’s Permanent Committee]. Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa [International Labour Organization (ILO)] na hadhi ya kiushauri na ujumbe wa Afrika kwa Haki za Binadamu na watu FIDH inawakilishwa kwenye Umoja wa Mataifa na ulimwengu wa Ulaya kupitia kwenye Ujumbe wake wa kudumu Geneva na Brussels.

Kila mwaka FIDH inafanikisha kupata na kutumia taratibu za kutunza na kutumia mambo ya kimataifa zilizopo kwa zaidi ya wawakilishi 200. Mashirika yake wanachama na kuunga mkono shughuli zao za kila siku. FIDH pia ina nia ya kuwalinda watetezi wa haki za binadamu.

---

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu [Tanzania]
S. L. P. 75254, Justice Lugakingira House
Kijitonyama, Dar Es Salaam, TANZANIA
Simu: 255 – 22 2773038, 2773048
Fax: 0255 22 2773037
Email: lhrctz@raha.com, Website: www.humanrightstz.org

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu** [The Legal and Human Rights Centre (LHRC)] ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii pamoja na kukuza, kuendeleza na kulinda Haki za Binadamu na utawala bora Tanzania.
Madhumuni ya LHRC ni kuwafanya watu wawe na uelewa wa sheria na haki za binadamu, na kuwawezesha umma kwa ujumla, wenye mamlaka (viongozi) na hasa wale sehemu ya jamii walioachwa nyuma. Walengwa wa LHRC wanajumuisha umma kwa ujumla, wasio na uwezo, viongozi wa amii, watu washuhuri, wasnasiasa, waundaji wa sera, Wabunge, watekelezaji wa sheria, mashirika ya jamii, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na mashirika anuwai ya kimataifa.
Makao makuu ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu yapo Dar es Salaam, lakini Kituo pia kinaendesha vituo vitatu vya msaada wa kisheria, viwili viko Dar es Salaam (Magomeni na Burugurni) na kimoja kiko mkoa wa Arusha.

Mkurugenzi wa uchapishaji: Sidika Kaba
Wahariri: Antoine Bernaid, Helen Kijo-Bisimba
Waandishi wa Ripoti: Eric Mirguet, Arnold Tsunga
Wachapaji wasaidizi: Céline Ballereau – Tetu
Imechapishwa na FIDH/ LHRC
Depot Legal April 2001 – Commission Paritaire No. 0904P11341 - Fichier Informatique conforme à la loi du 6 janvier 1978 (Déclaration No. 330675)